# Nipashe

Alhamisi Aprili 18, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579895

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





## UPIGAJI VYUO VIKUU

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini upotevu wa mabilioni ya...

UKURASA 3



## ATUPWA GEREZANI

ALIYEKUWA Rais wa Sudan, Omar Al-Bashir, amepelekwa gerezani baada ya kukamatwa juzi usiku...

UKURASA 25

UKURASA 13

# JPM awapa mtihani mzito mawaziri 2

UKURASA 2




## Neema upimaji ardhi sasa 150,000/-

UKURASA 2

## Shahidi aeleza mazito kesi ya kina Mbowe

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA KUIVAA SEVILLA YA LA LIGA TAIFA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Neema upimaji ardhi sasa ni 150,000/-

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza kushusha gharama za upimaji na urasimishaji ardhi kutoka Sh. 250,000 hadi Sh. 150,000 kuanzia jana.

Aidha, amewatahadharisha watumishi wa wizara hiyo ambao wanamiliki kampuni za upimaji na urasimishaji ardhi kuchagua kufanya kazi serikalini au kutumikia kampuni zao.

Lukuvi alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa wizara hiyo na kampuni za upimaji na urasimishaji ardhi jijini Dar es Salaam na kuwaeleza kwamba kazi hiyo imekuwa ikitumia gharama kubwa.

Alisema ameshusha gharama hizo baada ya kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wanaodai kutozwa gharama kubwa wakati wakitaka kupimiwa ardhi.

"Kutokana na gharama za urasimishaji ardhi, asilimia 70 ya watu wanaomiliki ardhi hawatambuliki na serikali na kusababisha kuikosesha mapato," alisema Lukuvi.

Alisema amefanya hesabu na kubaini kuwa Sh. 150,000 inatosha kupima na kurasimisha ardhi hivyo wanaotaka kumiliki ardhi kisheria wajitokeze kupata huduma hiyo kwa bei rahisi.

"Alisema maandalizi ya kupima ardhi na kuirasimisha ni kazi ya kampuni ambayo itapewa tenda na kazi ya kupata hati mmiliki inapaswa kufanywa na mmiliki mwenyewe kupitia halmashauri yake," alisema.

Kuhusu watumishi wa wizara hiyo wanaofanya kazi katika kampuni za upimaji ardhi, alisema wamekuwa wakiibia serikali kwa kufanya kazi zao binafsi na kuchelewesha kazi za serikali.

"Watumishi wa umma ambao mnafanya kazi kwenye hizi kampuni za upimaji mtenganishe maslahi ya serikali na yenu binafsi na ikiwezekana muache kazi serikalini muende mkatumikie kampuni zenu kwa sababu mnaibia serikali," alisema Lukuvi.

Pia aliwataka wananchi ambao wamelipa gharama za urasimishaji na upimaji ardhi kwa kampuni binafsi, lakini wamekaa zaidi ya mwaka bila kumaliza kazi, wawasilishe majina ya kampuni hizo ili azishughulikie.

"Kama zipo kampuni ambazo zimechukua fedha za upimaji Sh. 250,000 na wamekaa zaidi ya miaka mitatu hadi leo hawajapima, wengine wanacheza na viongozi wa serikali za mitaa, sasa nileteeni majina ya hizo kampuni nishughulike nazo," alisema Lukuvi.

# JPM awapa mtihani mzito mawaziri wawili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ametoa wiki moja kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Viwanda na Biashara, kukamilisha taratibu za uwekezaji kwa Kampuni ya Sugar Investment Trust (SIT) ya Mauritius, ambayo imecheleweshwa kuwekeza katika uzalishaji wa sukari tangu mwaka 2017.

Rais Magufuli alitoa maagizo hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mwenyekiti wa Kampuni hiyo, Gansam Boodram, aliyeongozana na Balozi wa Mauritius hapa nchini, Jean Pierre Jhumun.

Katika mazungumzo hayo, Boodram alisema yuko tayari kulima ekari 25,000 za mashamba ya miwa kwa ajili ya uzalishaji wa sukari na kwamba uwekezaji huo utawezesha kuzalishwa kwa tani 125,000 za sukari, ajira za kudumu 3,000 na ajira za muda 5,000.

Mwekezaji huyo alimweleza Rais Magufuli kuwa amekwama kuendelea kutokana na kusubiri majibu ya serikali kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu upatikanaji wa eneo la uzalishaji wa miwa na ujenzi wa kiwanda cha sukari.

Rais Magufuli aliagiza ufanyike uchambuzi wa haraka katika maeneo ya Bonde la Mto Rufiji mkoani Pwani, eneo la shamba la Mkulazi mkoani Morogoro na eneo la Kibondo mkoani Kigoma ili mwekezaji huyo apatiwe na kuanza mara moja uwekezaji.

Alisema nchi inahitaji kuongeza uzalishaji wa sukari utakaomaliza upungufu wa tani zaidi ya 100,000 ambazo kwa sasa zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Aidha, Rais Magufuli alimwagiza Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Edward Mhede, kufuatilia makubaliano ya ushirikiano katika uvuvi kati ya Tanzania na Mauritius ambayo hayajatiwa saini tangu mwaka 2017 licha ya wawekezaji wa Mauritius kuonyesha nia ya kutaka kuwekeza katika uvuvi na viwanda vya samaki.

Balozi Jhumun alimweleza Rais Magufuli kuwa Mauritius ina uzoefu mkubwa katika uvuvi na viwanda vya samaki na kwamba kwa kuitikia wito wake wa kuhamasisha wawekezaji kuja hapa nchini, amefanikiwa kupata kampuni zilizotayari kufanya uwekezaji huo baada ya makubaliano kati ya Tanzania na Mauritius kutiwa saini.

Rais alizionya taasisi za serikali kikiwamo Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kutoharakisha taratibu za kuwawezesha wawekezaji kuwekeza na amemhakikishia Balozi Jhumun kuwa atafuatilia kuhakikisha uwekezaji wa kampuni ya SIT unafanyika.

"Ndugu zangu watendaji wa serikali badilikeni, acheni kukwamisha wawekezaji, fanyeni maamuzi na kama yanawashinda toeni taarifa kwenye mamlaka za juu," alisisitiza Rais Magufuli.



Rais John Magufuli, akizungumza na Balozi wa Mauritius nchini, Jean Pierre Jhumun (kushoto) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Edwin Mhede (kulia) na Maofisa wa Kituo cha Uwekezaji na wa Ikulu, baada ya kuonana na kufanya mazungumzo na balozi huyo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Shahidi aeleza mazito kesi ya kina Mbowe

**Na Hellen Mwango**

USHAHIDI katika kesi ya uchochezi inayowakabili viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, uliotolewa na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Gerard Rich, umedai kwamba aliamuru kikosi cha mabomu ya machozi kurudi nyuma na kile cha silaha za moto kusonga mbele kupiga risasi juu kuzuia waandamanaji.

Kadhalika alidai kuwa kitendo cha washtakiwa kukiuka amri yake kupitia redio upepo iliyowataka kusitisha maandamano kwa mara ya pili, alilazimika kuamuru askari wenye silaha ya moto kusonga mbele.

SSP Rich ambaye pia ni Ofisa wa Polisi wa Operesheni Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, alitoa ushahidi wake jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimba, akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Wankyo Simon, Jacqline Nyantori na Salim Msemo.

Akiongozwa na Nchimbi shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018, aliitwa na bosi wake Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni (RPC), (wakati huo) ACP Jumanne Mlilo, akiwa na maofisa wenzake, walipewa maelekezo ya kazi kuimarisha ulinzi wakati wa kufunga kampeni pamoja na uchaguzi mdogo wa ubunge siku inayofuata Jimbo la Kinondoni.

Alidai vyama vyote vya siasa vilikuwa na mikutano katika viwanja tofauti jimboni humo, Chadema walikuwa viunga vya Buibui Kata ya Mwananyamala, Chama Cha Mapinduzi (CCM), viunga vya Biafra, Kata ya Kinondoni, Chama cha Wananchi (CUF), viunga vya Vegas, Kata ya Makumbusho.

Alidai kuwa mkuu wa ulinzi Chadema, alikuwa SSP Dotto, CUF alikuwa Mrakibu (SP) Batseba na CCM alikuwa SP Magai na wote watatu walitoa taarifa kwake kwa njia ya simu kuhusu hali ya ulinzi.

"Ilipofika saa 11:30 alipata taarifa kutoka kwa SSP Dotto kwamba katika jukwaa la Chadema, viongozi wamepanda jukwaani wametoa kauli zenye dalili ya uvunjifu wa amani ikiwamo kuhamasisha wafuasi kufanya maandamano," alidai shahidi na kuongeza.

"Hamasa iliongezeka wakazuia makutano ya barabara ya Kawawa na Mwananyamala kwa madai ya kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa Kinondoni, nilimwamuru dereva awashe king'ora, walitawanyika kutupisha, lakini walivyoona gari ya polisi walirejea kwenye barabara ya mwendo wa haraka na kusababisha magari kushindwa kuendelea na safari yake."

"Nilitoa ilani kuwataka wasitishe maandamano hayo kwa sababu si halali, nilimwona Salum Mwalimu, akiwa kwenye gari ya wazi, Mbowe akiwa ameongozana na viongozi wengine walioko kizimbani wakihamasisha, huku wakiimba 'haya twende Mbowe anatisha, hatupoi, hatishwi lazima tufike kwenye mkurugenzi," alidai shahidi.

Akifafanua zaidi alidai kuwa maandamano hayo yalisababisha wahalifu kupora kwenye maduka, watoto na wazee kukimbilia vituo vya polisi.

Alidai alitoa amri askari kuwarushia mabomu ya machozi waandamanaji, lakini upepo

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akiwa ameshikana mikono na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo, ambaye pia ni Katibu Mkuu wa Wizara, Doto James (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu Fedha, Dk. Khatibu Kazungu, wakishiriki kuimba wimbo wa mshikamano kwenye kikao cha baraza la wafanyakazi wa wizara hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CAG avianika UDSM, Udom, Muhas, Muce upigaji kutisha

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini upotevu wa fedha na matumizi mabaya ya mabilioni ya shilingi yanayofanywa na baadhi ya vyuo vikuu nchini.

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18 iliyowasilishwa bungeni Aprili 10, mwaka huu, Prof. Assad anabainisha kuwapo kwa changamoto hiyo ya upotevu na matumizi mabaya ya mabilioni, huku akipendekeza serikali kuchukua hatua kudhibiti mianya ya upigaji.

CAG Assad, katika ripoti ya ukaguzi wa hesabu za mashirika ya umma, anasema kwenye Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (Muce), alibaini chuo kilingia mkataba na Kampuni ya MNM Engineering kisha M/s. CATIC International Engineering Limited kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa mihadhara kwa gharama ya Sh. bilioni 3.62, lakini baadaye ziliongezeka mpaka Sh. bilioni 9.1.

Anabainisha kuwa ujenzi huo ulikosa ufanisi, kwa kuwa kazi ilipaswa ikamilike Septemba 2011, lakini mpaka Mei 10, 2018, ujenzi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 80.52.

Anasema tathmini ya ukaguzi maalum ilizingatia mikataba iliyoingiwa kati ya Muce na M/s. MNM Engineering Ltd, Epitome Architects Ltd, CATIC, International Engineering Ltd, Epitome Architects Ltd (ilijulikana awali kama Land Plan Icon Limited) kwa ajili ya ushauri na ujenzi wa majengo pacha ya mihadhara ambayo yangebeba wanafunzi 1,000 kila moja na kuongeza wanafunzi hadi 2,000.

Prof. Assad anabainisha kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi, mnamo Julai 2010, Muce iliingia mkataba wa ujenzi wa mradi na M/s. MNM Engineering Services Limited wa jumla ya Sh. bilioni 3.62.

INAENDELEA UK. 8

## WWF yaipa tano sasa Tanzania mifuko plastiki

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Kimataifa wa Kulinda Viumbe wa Asili (WWF), umeipongeza serikali kwa kupiga marufuku matumizi ya plastiki na kuahidi kushirikiana nayo kutoa elimu na udhibiti.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na WWF, Tanzania imefanya uamuzi mgumu na mzuri kwa mustakabali wa mazingira na uoto wa asili kwa kuwa plastiki inachangia uharibifu mkubwa wa mazingira. Mkurugenzi Mkuu wa WWF, Dk. Marco Lambertin, alisema viongozi wa Tanzania wanastahili pongezi kwa kuchukua hatua ya kulinda mazingira kwa kuzuia matumizi ya plastiki.

"Tumeshuhudia zaidi ya tani milioni nane zinaingia baharini kila mwaka na nyongeza ya tani milioni 104 ya plastiki inatarajiwa kuharibu uoto wa asili ifikapo 2030 kama hatua madhubuti hazitachukuliwa," alisema na kuongeza:

"Ina matokeo hasi kwa uhifadhi, maisha ya watu, afya ya binadamu na wanyamapori na kwa sasa uthibitisho wa kisayansi unaanza kueleweka, kwa uamuzi huu tunatangaza kuendelea kusaidiana na serikali katika kukabiliana na uchafuzi wa mazingira kwa kutumia plastiki."

Naye Mkurugenzi Mkazi wa WWF Tanzania, Dk. Amani Ngusaru, alisema wamefurahishwa na uamuzi wa serikali kuyaokoa mazingira na kwamba ni hatua kubwa ya kuigwa katika kulinda mazingira Tanzania.

"Plastiki inashika nafasi ya kwanza duniani kwa kuchafua mazingira na inaua kimya kimya uhifadhi wetu na rasilimali ya viumbe hai kuliko watu wanavyoelewa. Inachukua zaidi ya miaka 100 kwa mfuko wa plastiki kuoza na hivyo kusababisha matatizo makubwa," alisema na kuongeza: "Tuna furaha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizopiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki, tunaahidi kushirikiana na serikali kupambana na uharibifu wa mazingira kwa plastiki."

Hivi karibuni, katika hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2019/20, Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, alitangaza uamuzi wa kupiga marufuku matumizi ya plastiki ifikapo Mei 31, mwaka huu na itakapofika Juni mosi hawataruhusiwa kuzalisha mifuko hiyo na kwamba muda uliotolewa ni kuwawezesha wenye viwanda kujipanga na kuuza mzigo walionao.

## Jaji asitisha kesi mauaji mwanafunzi kwa siku 12

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KESI ya mauaji ya kukusudia ya mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Scholastica, Humphrey Makundi (16), inayowakabili watu watatu akiwamo mfanyabiashara maarufu katika Wilaya ya Moshi, Edward Shayo 'itasimama' kwa takribani siku 12, baada ya Jaji Firmin Matogolo, kuahirisha usikilizwaji wake.

Jaji Matogolo anayesikiliza shauri hilo namba 48 la mwaka 2018 katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Moshi, alitangaza uamuzi huo baada ya shahidi wa 17 wa upande wa mashtaka kumaliza kutoa ushahidi wake kizimbani.

Kwa mujibu wa Jaji Matogolo, kesi hiyo sasa itaendelea kusikilizwa tena Aprili 29, mwaka huu, kutokana na muda uliopangwa kusikiliza kesi hiyo kumalizika.

Jaji Firmini ameeleza: "Muda uliopangwa kusikilizwa kesi hii umemalizika na upande wa mashtaka bado haujamaliza kuleta mashahidi wao mahakamani hapa kwa ajili ya kutoa ushahidi wao, hivyo tutaendelea na kesi hii Aprili 29."

Mpaka sasa, upande wa mashtaka katika kesi hiyo inayovuta hisia za wakazi wa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, umeshawaita mahakamani mashahidi 17 kati ya 39 wanaoijenga kesi hiyo.

Kabla ya kuahirisha kesi hiyo kwa siku 12 mbele Jaji Matogolo, alisikiliza ushahidi wa shahidi wa 17 wa upande wa mashtaka, F. 1157 Detective (mpelelezi) Hashim Ally.

Akitoa ushahidi mbele ya Jaji Matogolo, shahidi huyo alidai kuwa Novemba 11, mwaka 2017, alipewa maelekezo na RCO (Mkuu wa upelelezi wa mkoa) kumhoji mtuhumiwa wa mauaji hayo, Hamisi Chacha aliyekuwa mahabusu ya polisi katika Kituo Kikuu cha Polisi Moshi Mjini.

Aliendelea kudai kuwa alimchukua mtuhumiwa huyo na kwenda kuchukua maelezo yake katika ofisi yake ya chumba cha upelelezi na kwamba wakati anafanya hivyo, mshtakiwa huyo alikuwa na afya nzuri.

Shahidi huyo alidai zaidi kuwa, baada ya kumfikisha Hamisi Chacha, katika chumba hicho alimpatia maelezo ya onyo na kumtaka kuwa na shahidi ama wakili wake wakati anatoa maelezo yake majira ya saa 5:25 hadi saa 8:40 za usiku.

Alidai baada ya kumpatia maelezo hayo mshtakiwa huyo alimweleza kwamba yupo tayari kuandika maelezo yake mwenyewe na alipoanza kuyatoa alikiri kufanya mauaji ya Humphrey Makundi.

Katika maelezo yake, shahidi huyo amedai kuwa baada ya mtuhumiwa kukiri kosa hilo, alimsomea mshtakiwa maelezo na kuyakubali na kisha alitia saini kwa hiari yake mwenyewe na pia alimweleza maelezo yake hapo siyo mwisho wake na kwamba anaweza kuyatoa kwa mlinzi wa amani.

Aidha, shahidi huyo wa upande wa mashtaka, ameeleza zaidi kwamba baada ya kumaliza kumhoji mshtakiwa alimrudisha rumande kituo kikuu cha polisi na kwamba hakuna wakati alimpiga wala kutoa vitisho kwa mshtakiwa.

Hashimu alidai mahakamani hapo akiwa Ofisi ya RCO (Mkuu wa upelelezi wa mkoa) kama mtunza vielelezo, alipokea simu saba zikiwamo simu za mshtakiwa wa kwanza na watatu, nguo za marehemu Humphrey Makundi ikiwamo bukta, tshirt na soksi.

Mahojiano hayo kati ya shahidi huyo ambaye ni mpelelezi (Hashimu) na jopo la mawakili wa

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 17/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 20/04/2019 kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea KAGERA gari hilo lenye namba za usajili: **T776 CAD/T220 DCT.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   **Urefu - mita 18.00**
   **Upana - mita 2.84**
   **Kimo - mita 4.90**

3. NJia itakayotumika **DAR** hadi **KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215185802

HABARI KITAIFA

# Wizara wafundwa usimamizi wa fedha

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

NAIBU Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, amewataka wafanyakazi wa wizara hiyo kusimamia rasilimali fedha zinazokusanywa na serikali pamoja na matumizi yake.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa hotuba yake kwenye ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wafanyakazi pamoja na kikao cha kujadili bajeti ya wizara hiyo kilichofanyika jijini hapo jana.

Dk. Kijaji aliwataka wafanyakazi wa wizara hiyo, kuhakikisha wanasimamia rasilimali fedha zote zinazokusanywa na serikali katika maeneo yote nchini.

"Haiwezekani wewe ni mhakiki mali wa serikali katika eneo lako, lakini hujui mapato halisi ya serikali kwenye eneo lako, basi utakuwa hunamaana ya kuitwa mhakiki wa serikali," alisema.

Alisema Wizara ya Fedha imebeba majukumu makubwa ya kuhakikisha kuwa utekelezaji wa maagizo ya serikali kwenye ukusanyaji mapato na matumizi ya rasilimali fedha yanasimamiwa kwa kila eneo.

Aliyataja majukumu mengine ya wafanyakazi hao nchini kuwa ni kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya ndani pamoja na kupanua wigo wa walipa kodi, kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, Dk. Doto James, akitoa taarifa yake alisema kikao hicho kitatumika kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na kupitia mwelekeo wa makadirio ya bajeti ya mwaka 2018/2019.

Dk. James alisema pia kutakuwa na mkutano wa kawaida wa baraza la wafanyakazi utakaojadili utekelezaji wa maazimio ya vikao vilivyopita, kupokea na kujadili hoja mpya za watumishi na mada mbalimbali kutoa ndani na nje ya wizara.

Alisema vikao vya baraza hilo vimekuwa na umuhimu mkubwa mahala pa kazi wizarani na kutokana na mkataba baina ya wizara na Chama cha Wafanyakazi Serikalini na Afya (TUGHE), vikao hivyo vinatakiwa kufanyika mara mbili kwa mwaka.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 17/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 20/04/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR kuelekea KAGERA gari hilo lenye namba za usajili: **T794 DFQ/T 394 ADH.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 19.00**
**Upana - mita 3.20**
**Kimo - mita 5.20**

3. NJia itakayotumika **DAR** hadi **KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215185802




Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Hamis Lisu (kulia), akipata maelezo kuhusu mfumo wa umeme wa betri unavyoweza kutumika majumbani kutoka kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbezi Beach, wakati wa mahafali ya 14 ya shule hiyo, jijini humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Talaka 122 zatoka miezi 9

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, amesema Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) umefanikiwa kusajili ndoa 26,953 na talaka 122 katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka huu wa fedha.

Kwa takwimu hizo za wizara, ina maana kwamba kila mwezi kuna talaka 14 zinazosajiliwa nchini, sawa na talaka moja kila baada ya siku mbili.

Akiwasilisha hotuba bungeni jijini Dodoma jana, kuhusu mpango na makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Dk. Mahiga alisema wakala huo pia wamefanikiwa kusajili vizazi 1,271,372, vifo 28,285 na hati 28 za watoto wa kuasili.

Alisema kuwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu na Takwimu, wizara yake iliendelea kuimarisha shughuli za usajili huo wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi ya utambuzi na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo.

"Kupitia utekelezaji wa mkakati huo, serikali imefanikiwa kuongeza kiwango cha usajili kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kutoka asilimia 13, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 38 kwa mwaka 2019.

"Vilevile, wizara iliendelea na usimamizi wa mirathi, usajili wa bodi za wadhamini, uandishi na uhifadhi wa wosia, ambapo wosia 38 zimeandikwa na kuhifadhiwa katika kipindi cha mwaka 2018/19," Dk. Mahiga alibainisha.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho, jumla ya majalada 234 ya makosa ya rushwa yalipokewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru). Kati yake, 56 yaliandaliwa hati za mashtaka na kupatiwa vibali vya kushtaki.

Alisema majalada 94 yalirudishwa Takukuru kwa upelelezi zaidi, huku jalada moja likifungwa na 83 yanaendelea kufanyiwa kazi.

Dk. Mahiga alibainisha kuwa mashauri ya wanyamapori yaliyoshughulikiwa ni 1,293. Kati yake 204 yalihitimishwa na mengine yanaendelea katika hatua mbalimbali. "Kesi za dawa za kulevya zilizoshughulikiwa ni 2,545 na kati ya hizo 756 zilihitimishwa, ambapo mashauri 591 ya uhujumu uchumi yalishughulikiwa na mashauri 113 kati ya hayo kuhitimishwa," alisema.

# Watoto wafia kwenye dimbwi

Na Christina Haule, MOROGORO

WATU watatu wamefariki dunia baada ya kuzama kwenye maji ya dimbwi na maporomoko maeneo tofauti mkoani hapa, wakiwamo watoto wawili wa Kijiji cha Mngeta wilayani Kilombero waliokufa maji wakati wakicheza kwenye dimbwi lenye kina kirefu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, aliwataja watoto hao ni Lumbango Kurwa (5) na Musa Alfonce (4), wakazi wa kitongoji cha Kilulusha wilayani humo.

Alisema tukio hilo lilitokea Aprili 15, alasiri katika kitongoji cha Kilulusha kiichopo Kijiji cha Mngeta wilayani Kilombero, ambapo watoto hao walikuwa wakicheza kwenye dimbwi la maji lenye kina kirefu na ndipo wakazama na kufariki dunia. Kamanda huyo alisema miili yao imehifadhiwa katika Kituo cha Afya Mngeta kwa uchunguzi zaidi.

Wakati huo huo, Baraka Jacob (17), mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari SUA, amefariki dunia baada ya kusombwa na maji baada ya kuingia kwenye kina kirefu wakati akiogelea katika maporomoko ya maji kwenye milima ya Uluguru.

Kamanda Mutafungwa alisema, tukio hilo lilitokea Aprili 15, saa 10 jioni katika kijiji cha Kilala Kata ya Luhungo Manispaa ya Morogoro, ambapo Jackob akiwa na mwenzake, Samuel Glozad, wakiogelea katika maporomoko ya maji kwenye milima hiyo ndipo maji yalimzidi nguvu na kuingia kwenye kina kirefu na hatimaye kufariki dunia.

Alisema, mwili umehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani mkoani hapa kwa uchunguzi zaidi.

Katika tukio lingine Jeshi la Polisi mkoani hapa linamsaka mwanamke aliyetupa mtoto mchanga mwenye umri wa siku moja na kuokotwa akiwa hai katika Kata ya Kilakala Manispaa ya Morogoro.

Kamanda Mutafungwa alisema tukio hilo lilitokea Aprili 15, asubuhi eneo la Mzambarauni, ambapo mtu asiyefahamika alitupa mtoto mchanga wa jinsia ya kiume mwenye umri wa siku moja.

Alisema mtoto huyo alikutwa amefungwa kwenye mfuko wa rambo, na amehifadhiwa Hospitali ya Mtakatifu Thomas Kilakala kwa uangalizi na anaendelea vizuri.

## HABARI KITAIFA



Mafundi wakiweka lami kwenye mzunguko wa Barabara ya Maramba Mawili, eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Bil. 1.6/- kuboresha usalama watetezi haki za binadamu

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Asasi za Kijamii (Foundation for Civil Society), umesaini mkataba wa zaidi ya Sh. bilioni 1.6 na Mtandao wa watetezi wa haki za binadamu kwa ajili ya kuboresha mifumo na kuimarisha usalama wa watetezi wa haki za binadamu kwa miaka mitatu.

Akizungumza wakati wa kusaini mkataba huo, Mkurugenzi wa Foundation For Civil Society, Francis Kiwanga, alisema kila mwaka watatoa Dola za Marekani 100,000 (sawa na Sh. milioni 231), kwa viwango vya kuadilishia fedha jana.

Alisema lengo ni kuchangia jitihada za THRDC kuwalinda, kuimarisha mifumo ya ulinzi na utetezi wa haki za binadamu nchini.

Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema usalama wa watetezi wa haki za binadamu unazidi kuwa mashakani kutokana na kuongezeka kwa vitendo vya mashambulizi dhidi yao.

"Hivi karibuni tulizindua ripoti ya kuonyesha hali ya watetezi wa haki za binadamu nchini na tuliona hali inazidi kuwa mbaya na kwa kipindi hiki tunachoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu Oktoba mwakani, ni lazima watetezi wapate msaada ili wafanye kazi zao vizuri," alisema.

Mkataba huo utaanza Aprili, mwaka huu hadi Machi 2022, ukiwa na jumla ya Sh. 1,610,642,669 sawa na Dola za Marekani 714,286.

Mwanzoni mwa mwezi huu, THRDC ilizindua ripoti ya hali ya watetezi wa haki za binadamu na bango kitita la sheria na sera zinazoathiri nafasi ya asasi za kiraia mwaka 2018, iliyoonyesha watetezi wa haki za binadamu 52 walishambuliwa, kukamatwa, kunyanyaswa na kuteswa mikononi mwa vyombo vya dola wakati wakitekeleza majukumu yao.

# Askofu Kilaini ahimiza umuhimu kusoma vitabu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WATANZANIA wameshauriwa kujenga utamaduni wa kusoma vitabu ili kujifunza na kuutumia ujuzi huo kufanya mambo ya maendeleo, hivyo kuachana na utegemezi wa mataifa ya kigeni.

Ushauri huo ulitolewa na Askofu Msaidizi wa Kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba, Dk. Methodius Kilaini, wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Mtazamo wa Mwalimu Nyerere enzi za uhai wake katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Muadhama Laurian Kardinali Rugambwa, katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera.

Alisema wananchi wamekuwa na tabia ya kutosoma vitabu ambavyo vitawafanya kuelewa zaidi mambo ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Askofu Kilaini, elimu inayotolewa sasa bado ni ya Waingereza ambayo haiwezi kumfanya mtu kujitegemea, hivyo kuwafanya wengi kusubiri ajira.

"Bado tuko na elimu ya Waingereza ambayo ina muundo wa nadharia isiyomfanya mtu kufanya vitendo vya kujitegemea kama mtazamo wa Mwalimu Nyerere uliolenga kuondoa umaskini, ujinga na utegemezi," alisema Askofu Kilaini.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Juvenalius Baitu, alisema lengo la kuhimiza elimu ya vitendo kupitia kitabu cha Mtazamo wa Mwalimu Nyerere ni kusaidia jamii kuondokana na mambo yaliyokuwa akiyasimamia na yakihimiza Mwalimu Nyerere.

Alisema kupitia utafiti mbalimbali waliofanya kabla ya kuandika kitabu hicho ambacho kiliandaliwa kwa miezi 16 hadi kukamilisha, wamebaini jamii haijaweza kujitegemea kwa kupigana na ujinga na umaskini.

Hatuna mambo yanayotufanya kuwa na maendeleo yetu wenyewe, bali tuna elimu ambayo inahitaji ajira. Watanzania tuna fursa ambazo wageni wanapeleka kwao kujinufaisha," alisema Prof. Baitu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jeneral Marco Gaguti, alisema ameandaa klabu shuleni ambazo zinalenga mtazamo bora wa elimu ya nadharia na vitendo kwenye shule nane.

Gaguti alisema kupitia mtazamo wa kitabu cha Mwalimu Nyerere uliondaliwa na kwa mambo ya kuiendeleza elimu ya taifa kwa kuwa ya vitendo na kuacha kutegemea ajira pekee, utasaidia wanajamii kujiinua zaidi.

# Norway waipa LHRC bil. 5/-

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Norway nchini umetoa msaada wa Dola za Marekani milioni 2.2 (sawa na Sh. bilioni 5.08) kwa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa ajili ya kusaidia mambo mbalimbali ikiwamo kuujengea umma uwezo katika haki za binadamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano na Ubalozi wa Norway, Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, alisema msaada huo utaenda kutekeleza yale waliyokubaliana.

Henga alisema Serikali ya Norway kupitia ubalozi wake nchini ni mhisani wa muda mrefu na imeanza kuwafadhili tangu mwaka 2004.

Alisema sambamba na ufadhili wao, Serikali ya Norway imekuwa mfadhili wa Serikali ya Tanzania kwa kuwa ni moja ya mataifa 10 wanufaika wa miradi ya maendeleo kutoka nchini Norway.

"Norway wamekuwa wakifadhili miradi mbalimbali ya maendeleo hususani miradi ya kuendeleza sekta binafsi, nishati, uchimbaji mafuta petroli, uhamasishaji wa ongezeko la mapato kupitia usimamizi wa fedha pamoja na miradi ya utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa," alisema.

Aidha, alisema lengo kuu la kituo hicho kupatiwa msaada huo ni kufikia jamii yenye haki na usawa na tayari wameandaa malengo mkakati ya kuratibu kazi zao.

Alisema katika kipindi cha miaka sita ijayo wamejiwekea malengo mkakati matano ambayo ni kufanya uhamasishaji kwa lengo la kuboresha, kubadilisha sheria, kupanua ushiriki wa wananchi, kukuza na kudumisha demokrasia na kuchochea mabadiliko ya Katiba.

Henga alisema watakwenda kudumisha haki za kijamii pamoja na haki za kiuchumi na kuhakikisha haki ya kila mwananchi kuishi katika mazingira safi na salama zinazingatiwa.

"Kuchochea maboresho ya sheria na sera zinazosimamia haki za wanawake, watoto na watu wenye ulemavu pamoja na kuimarisha utendaji wa kituo chao," alisema

Alisema malengo hayo yanawawezesha kujipima na jamii kwa ujumla na kuona ni kiwango gani wanapiga hatua katika kulinda, kutetea na kudumisha utawala wa sheria na kupendekeza namna bora ya kutatua changamoto katika jamii.

Kwa upande wake, Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alisema serikali yake inaunga mkono juhudi za serikali katika kufikia uchumi wa kati.

Alisema juhudi hizo zitakwenda sambamba na kuona Tanzania inakuwa na watu wanaojua haki zao za msingi na kuzidai.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fao kukosa ajira siyo msaada, lipo kisheria

**KATIKA** gazeti la jana tulichapisha habari kuhusu malalamiko ya baadhi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kupigwa danadana ya kulipwa fedha za mafao ya upotevu wa ajira na michango yao ya kujitoa uanachama kwa muda mrefu bila mafanikio.

Wanachama hao walitoa madai yao jinsi ambavyo wamekuwa wakisumbuliwa na mwisho wa siku wamebaini kwamba wote wamekuwa wakiambiwa yanayofanana ya kucheleweshewa kulipwa mafao hayo.

Miongoni mwa majibu hayo ya pamoja ni wanachama hao kuelezwa kuwa walikosea kuweka alama ya dole gumba, kuwapo kwa tatizo la mtandao na wanasimika mfumo mpya kwa kushirikiana na Hazina. Wanachama hao wameitaja ofisi ya NSSF Ubungo, jijini Dar es Salaam ndiyo imekuwa ikiwasababishia usumbufu kila siku wa kupewa sababu mpya za kuchelewa kulipwa haki yao kisheria.

Mmoja wa wanachama hao alibainisha kuwa mkataba wake wa kazi ulikwisha tangu Julai mwaka 2018, alifungua maombi ya malipo na ilipofika Novemba mwaka huo.

Baada ya kuwasilisha maombi hayo licha ya kupokelewa alijibiwa kwamba hawezi kulipwa michango yake yote, badala yake alitakiwa kufungua fao la upotevu wa ajira ambalo alifungua Desemba 11, mwaka huu, lakini ajabu ni kwamba hadi juzi hakuwa amelipwa chochote.

Tunatambua hali ya maisha inavyokuwa ngumu hasa kwa mtu ambaye alikuwa ni mwajiriwa, alikuwa na uhakika wa kipato, lakini sasa anaweza kuishi kwa kubahatisha, kwa hiyo ni wazi mwanachama huyo na wenzake kadhaa wamejikuta kwenye wakati mgumu. Kucheleweshwa kulipwa kwa mafao hayo ni jambo ambalo limetushangaza kwa kuwa inazidi kuwaongezea ugumu zaidi wa maisha kwa kuwa ukifuatilia kwa karibu unaweza kubaini wana madeni yamewaelemea ambayo mengine yameongezwa na gharama za nauli wanazotumia kufuatilia madai yao.

Tunafahamu kwamba fao la kukosa ajira halitolewi kama msaada, bali lipo kwenye sheria mpya ya mifuko ya hifadhi ya jamii na kuunganishwa kwa baadhi ya mifuko hiyo, hivyo wana haki kabisa ya kulipwa kama ilivyoelekezwa.

Awali kabla ya sheria hiyo, hakukuwa na fao hili la kujitoa, badala yake wanachama walijitoa kwenye uchangiaji walipopoteza ajira kisha wakarejeshewa amana zao hatua hii haikuwa kisheria. Wanachama waliaminishwa kuwa fao la kutokuwa na ajira ni zuri, kwa kuwa mwanachama anaanza kupewa pensheni ya kutokuwa na ajira pale anapowasilisha maombi kwa mfuko husika ndani ya wiki sita. Sheria hiyo inautaka mfuko husika kushughulikia maombi ya mwanachama ndani ya wiki sita, baada ya kukamilisha atakuwa anapewa asilimia 33.3 ya mshahara wake wa mwisho kwa kipindi cha miezi sita.

Tunatamani tuone mifuko ya hifadhi ya jamii ikiwa ni faraja kwa wanachama wake kwa kuhakikisha wanapata haki zao za msingi zinazoainishwa na sheria mpya, likiwamo fao la kujitoa ambalo tunaamini linaweza kumsaidia kumsogeza kujipanga upya katika kujitafutia kipato.


Tunawasihi viongozi husika kuona umuhimu wa kuwasimamia watendaji wa mifuko hiyo kuhakikisha wanachama wanalipwa mafao yao kwa mujibu wa sheria, badala ya kuwa wasumbufu na kuwafanya wajute kuwa wanachama wao.

Kikubwa ikumbukwe kuwa wahusika licha ya kukosa ajira na kukumbana na hali ngumu ya maisha, bado wanategemewa na familia zao, ikiwamo kutoa huduma za msingi za elimu na matibabu kwa watoto wao na wategemezi, kwa kutaja baadhi.

Katika kusimamia haki za wanyonge, serikali isikubali wananchi wake hao wakateseka bila sababu za msingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Wazazi, tusiwaendekeze watoto kupitiliza, watatusumbua sana

**KUNA** usemi kwamba mtoto umleavyo, ndivyo akuwavyo. Ni usemi wenye maana kubwa katika vizazi vilivyopo na vijavyo na huko nyuma tulikotoka.

Iko wazi kwamba usemi huo ukifuatiliwa katika nyayo zake, utazaa jambo lenye kubeba maana fulani katika vipindi tofauti.

Hiyo inafanya kuwapo kila sababu ya mzazi kuivalia miwani na kufungua masikio zaidi, kufuatilia usemi huo, kwa faida binafsi, pia kizazi cha sasa na baadaye.

Kumekuwapo baadhi ya wazazi ambao wamewadekeza watoto wao kupitiliza na hali hiyo imechangia mzazi au mlezi kukumbana na aibu au sura ya kashfa .

Moja ya matendo ya aibu hizo, ni pale mtoto anawaona wageni, ndipo anapoanza kufanya mambo ambayo hayana ama staha au maana na ya aina yoyote inayoangukia katika kumtia aibu mzazi.

Unakuta mgeni kaja kukutembelea, nawe unamuandalia soda, badala ya kunywewa na mgeni, unaona mtoto anaichukua na kuanza kuidai kwa namna atakayo yeye.Tafsiri ya 'karibu mgeni' inakufa papo hapo.

Kuna wakati mzazi unaangalia taarifa ya habari au tukio flani kwenye televisheni, basi hapo ndipo naye mtoto anachachamaa kudai haki ya kupewa rimoti au hata kuinyang'anya aweke muziki wake.

Matukio hayo yanatokea sana majumbani. Mzazi katika nafasi yake anashindwa hata kumkanya mwanawe na anaishia kutoa sauti ya unyonge ya kumwambia mtoto "acha kufanya hivyo..."

Matukio hayo sio kuwa yanafanywa na mtoto mchanga, labda utasema ni mdogo sana. Wengine

**Matukio hayo sio kuwa yanafanywa na mtoto mchanga, labda utasema ni mdogo sana. Wengine wafanyao ni watoto wanaojitambua kimwili na kiakili wameshakua, wanaopaswa kuwajibika kinidhamu.**

wafanyao ni watoto wanaojitambua kimwili na kiakili wameshakua, wanaopaswa kuwajibika kinidhamu.

Kuna mkasa mwingine, mathalani mgeni wa kike anakuwa kajipamba, lakini mtoto katika utundu wake, muda wote anafanya michezo ya kumrukia huku na kule hadi kumkosesha raha.

Hayo yote bila ya aibu nasema yanaangukia katika kundi la malezi mabaya kwa watoto wetu na chanzo chake ni wazazi na walezi. Sasa matendo hayo ambayo ni matokeo ya ulezi, yanakuwa katika hatua ya kubeba sura ya karaha kwa kumkosesha raha mzazi.

Wapo watoto ambao wazazi wanapoamua kuwachukulia hatua au kwa utovu wa nidhamu mbele ya mgeni, ndio ulingo wao wa kujibu mapigo kwa kumtolea lugha mbaya, mbele ya mgeni. Ni aibu tupu.

Nini kifanyike, ili kuepukana na aibu za aina hizo? Kunatakiwa kuwapo malezi bora kwa watoto wetu na kuchukua hatua kali pasipo kuwaonea haya au huruma, wanapoenda kinyume.

Mtoto akikosa aonywe bila ya chembe ya kuogopwa na kama tutamuogopa, tunakaribisha tabu za kila siku, hasa ile aibu mbele ya wageni wanaotembelea nyumbani kwetu.

Tuwapende watoto, lakini tusipitilize mipaka hadi kujikuta tunaogopa kuwakaripia, kuendana na makosa wanayoyafanya.

Unapompenda mtoto kupitiliza na kumdekeza kupitiliza, basi tujue nao, baadaye wakikua watakusumbua kupitiliza na hutakuwa na uwezo wa kuwadhibiti.

BARUA/MJADALA

# Sikonge tunalilia ardhi

*Mhariri,*

*SISI wakazi wa Wilaya ya Sikonge, tunaomba kutumia fursa hii kupatiwa msaada wa kiongozi katika ngazi ya serikali, kuhusu kero hii ya ardhi inayotukabili bila ya majibu sahihi hapa kwetu.*

*Tunasema hayo kwani kilio chetu kimeachwa katika ukimya, bila ya majibu kamili au sahihi inayotufaa.*

*Hivi sasa kuna kazi ya upimaji ardhi inayofanyika katika mazingira yetu, inayoendana na aina ya kero dhidi ya kupunguzwa ukubwa wa viwanja hivyo na cha kushangaza, baadhi ya wamiliki wa viwanja wanaporwa maeneo yao wakiachwa patupu. Hii kweli ni sahihi?*

*Ninachoshangaa ni kwa wawekaji bikoni hizo, kwamba namna wanavyofanya kazi hawataki kutolewa maelekezo yoyote, ilhali sisi ndio wamiliki wa ardhi na ndio tunaofahamu ukweli ulivyo kwa hatua ya kuwa msaada mkubwa kwao.*

*Tunafahamu vyema serikali imechachamaa katika uwajibikaji wake kuhusiana na maboresho yanayohusu sekta yetu ya ardhi na nia iliyoko ni nzuri sana. Lakini, baadhi ya hao watendaji waliopewa jukumu wanaonyesha kasoro.*

*Katika hilo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, tunafahamu vizuri namna unavyowajibika kila upande wa nchi kusukuma maboresho katika sekta ya ardhi. Niseme, namshauri aje Sikonge achuke hatua inayostahili kuhusu kinachoendelea kwetu.*

*Tunaongea hayo kwa uchungu, kwa maana ya ardhi ndio inashika roho ya umma maana ardhi ina unyeti katika yanayotusimamia maishani. Aina hiyo ya maamuzi kutoka kwa wapimaji ni mtihani sana.*

*Nikutajie baadhi ya maeneo yanayohusika na adha hii kuwa ni: Ugolole. Mazinge, Usega na Majengo, hapo ni rahisi kukiona tunachokilalamikia sisi wakazi.*

***Wananchi,***
***S.L P 64,***
***Sikonge.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Tujifunze kwa wengine kudhibiti Ukimwi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Jenista Mhagama, akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi, Dk. Leonard Maboko, kitabu chenye taarifa ya utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi cha mwaka 2016-2017, mara baada ya uzinduzi wa taarifa hiyo jijini Dodoma, Jumapili iliyopita. Kulia kwa waziri ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Dawa za Kulevya Osca Mukasa(Mb) na kushoto ni Naibu Waziri wa Afya, Serikali ya Zanzibar, Harusi Said Suleiman. **PICHA: TACAIDS.**

**Na Sabato Kasika**

**MAAMBUKIZI** ya ugonjwa wa Ukimwi visiwani Zanzibar, yanaelezwa kuwa chini ya asilimia moja. Ni mafanikio makubwa, kulinganisha na Tanzania Bara, ambako katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara maambukizi hayo yako juu.

Kwa Tanzania Bara, mikoa inayotajwa kuongoza kwa maambukizi ya ugonjwa huo ni Njombe kwa asilimia 11.6. Zingine zikiwa na asilimia zake katika mabano ni Iringa (11.2%), Mbeya (9.2%) na Kagera (6.8%).

Pia, kuna mikoa michache yenye maambukizi ya chini inayotajwa kuwa ni: Lindi (0.3%), Manyara (1.8%), Arusha (1.9%) na Mtwara asilimia (2.1%).

Kwa hali kama hiyo, ni wazi kwamba kuna jambo la kujifunza kutoka Zanzibar, pia mikoa ya Lindi, Mtwara, Manyara na Arusha, kwa zilivyoweza kuwa na asilimia ndogo ya maambukizi kuupata uzoefu huo.

Tujulize, kama Zanzibar wameweza na wana nini hadi maeneo mengine yashindwe? Jambo la msingi ni kubadili tabia tu ili kuepuka kuingia kwenye janga hilo.

Ukimwi ni ugonjwa unaoendelea kuangamiza watu duniani tangu ulipoibuka mwanzoni mwa miaka ya 80 na hadi leo bado wataalamu wanaendelea kutafuta dawa ya kukabili, hivyo muhimu ni kujilinda.

Takwimu zinaonyesha kuwa maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi nchini yameshuka kutoka asilimi 5.1 kwa mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 4.7 katika mwaka 2016/2017.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uratibu, Bunge, Sera, Ajira, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhangama, alipokuwa jijini Dodoma akizindua taarifa ya utafiti wa viashiria na matokeo ya Ukimwi kwa mwaka 2016/2017, alisema katika matokeo ya mwaka huo, maambukizi kwa wenye virusi vya Ukimwi kwa wenye umri katu ya miaka 15 hadi 49, ni asilimia 4.7.

"Wanawake ni asilimia 4.7 na wanaume ni asilimia 3.1, lakini kwa ujumla maambukizi yamepungua kutoka watu 80,000 mwaka 2012 hadi 72,000 mwaka 2017. Pia, vifo vitokanavyo na Ukimwi vimepungua," anasema Waziri Mhagama.

Akifafanua kuhusu vifo hivyo, Waziri Mhagama anasema, hadi sasa vimepungua kutoka watu 70,000 kwa mwaka kuanzia mwaka 2010 hadi kufikia vifo 32,000 kwa mwaka, katika kipindi cha mwaka 2017.

Kwa upande wa maambukizi ya vijana kuanzia umri wa miaka 15 hadi 24 ni asilimia 1.4 kwa wasichana na asilimia 0.6 kwa wavulana.

Pia, anaongeza kuwa maambukizi kwa vijana wa kike yako juu kuliko wa wanaume na hasa wenye umri wa miaka 15 hadi 34.

"Nitoe wito kwa Taasisi ya Kudhibiti Ukimwi (Tacads) na wadau wote wa mapambano ya Ukimwi kuendelea kuweka mikakati na kusimamia utekelezaji wa afua za Ukimwi kwa vijana kwa msisitizo mkubwa zaidi," anasema.

Kwa takwimu hizo, ni wazi kwamba waathirika wakubwa ni vijana ambao kimsingi ni nguvukazi ya taifa. Kwa maana hiyo, nikasema kuna haja ya kujifunza kwa wengine waliofanikiwa, jinsi ya kupambana na ugonjwa huo.

Hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali na wadau wa mapambano ya Ukimwi ni muhimu ziungwe mkono ili Watanzania wasiendelee kuugua na kufa kwani huathiri ustawi wa jamii, nguvu kazi muhimu ikipotea.

Kimsingi ni kwamba, vita dhidi ya VVU na Ukimwi, inahitaji dhamira ya dhati na tafakuri ya kina katika kujilinda dhidi ya maambukizi mapya.

Hilo likifanyika na inaweza kufanikisha Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi 2018/19 - 2022/23 unaotarajia kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa asilimia 75, ifikapo mwaka 2020 na asilimia 85 ifikapo mwaka 2023.

Ikumbukwe kuwa, matokeo mengine yanayotarajiwa kufikiwa kwa mkakati huo, ni kupungua kwa maambukizi mapya ya VVU miongoni mwa watoto, chini ya asilimia tano ifikapo mwaka 2023 na chini ya asilimia mbili, ifikapo mwaka 2030. Aidha, mkakati huo pia utawezesha kupungua vifo vinavyohusiana na Ukimwi kwa asilimia 50, ifikapo mwaka 2020 na asilimia 70, ifikapo mwaka 2023.

Lingine linagusa kupunguza unyanyapaa na ubaguzi ifikapo mwaka 2023, vilevile kuelekea kuutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2030.

Inaelezwa kwamba, hadi sasa ni asilimia 60.9 ya watu wanaoishi na VVU ndio tu wanaofahamu hali zao.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**



# CAG avianika UDSM, Udom, Muhas, Muce upigaji kutisha

INATOKA UK. 3

Anasema ujenzi huo ulitarajiwa kuanza Julai 4, 2010 na kukamilika Septemba 30, 2011, lakini wakati wa utekelezaji, kiwango cha kazi kilibadilika kutokana na jiografia ya eneo na kusababisha nyongeza ya Sh. bilioni 1.08, ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

"Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 30 ya bei ya awali ya mkataba na kufanya jumla ya gharama ya mkataba kuwa Sh. bilioni 4.71. Kiwango hiki cha nyongeza hakikuidhinishwa na Bodi ya Chuo.

"Tofauti hizi zingeweza kuepukika endapo tu suala hili la taarifa ya kijiografia ya eneo hilo iliyotolewa na mhandisi mshauri lingeshughulikiwa kama lilivyokuwa limewasilishwa katika mapendekezo yake na ilivyoelezwa katika mkataba wa ushauri," Prof. Assad anasema katika ripoti yake hiyo.

Anaongeza Novemba 28, 2012, mkataba ulivunjwa kwa sababu ya kushindwa kwa mkandarasi na alistahili kulipwa Sh. bilioni 2.67 kulingana na kazi halisi iliyofanyika.

Katika ripoti yake hiyo, Prof. Assad anabainisha Mei 9, 2013, mkandarasi mpya M/s. CATIC International Engineering Limited aliingia mkataba wa bei ya Sh. bilioni 4.74.

"Wakati wa utekelezaji, kulikuwa na kusimamishwa kwa kazi kwa muda wa siku 582 ambazo ziliongeza gharama ya jumla ya Sh. milioni 991.7 ambazo zingeweza kuepukwa kinyume cha kifungu 22.1 cha mkataba wa ushauri.

"Gharama ya kazi chini ya kiwango zilizofanywa na mkandarasi aliyepita, pia zilisababisha ongezeko la Sh. milioni 259.67 na riba ya Sh. milioni 178.64 kwa kuchelewesha malipo.

"Jumla ya bajeti ya mradi huu kwa CATIC ilikuwa Sh. bilioni 6.17. Gharama zote hizi zingeweza kuepukika kwa kuwa kwa kiasi kikubwa kilitokana na makosa ya mkandarasi.

"Kazi ya mhandisi mshauri pia ilibadilika mara mbili na kuongeza gharama kutoka bei ya Sh. milioni 122.84 mpaka Sh. milioni 263.07.

"Nyongeza za gharama ya mradi ilifanya uwe wa Sh. bilioni 9.1. Gharama hii iko juu kwa Sh. bilioni 4.1 (asilimia 82) ikilinganishwa na makadirio ya mhandisi mshauri ya Sh. bilioni 4.99.

"Pia, gharama ziko juu kwa Sh. bilioni 5.36 (asilimia 151) dhidi ya bei ya mkataba wa awali wa Sh. bilioni 3.75 kati ya Muce na MNM Engineering & Epitome Architects Limited.

"Napendekeza serikali ifuatilie kwa karibu miradi yake ikiwa ni pamoja na utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi kwa wakati ili kuepuka gharama zisizo za lazima zitokanazo na kusimamishwa kwa miradi na kusababisha gharama za riba na faini," Prof. Assad anashauri.

**UPOTEVU MABILIONI UDOM**

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad pia anabainisha kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kiliingia mkataba wenye namba RFQ/PA/041/2017-2018/G/14 LOT 2 na M/s. Technotrade Investment Ltd kwa ajili ya kuleta, kufunga na kuanza kufundisha utumiaji wa vifaa na mitambo ya maabara za sayansi kwa Sh. bilioni 2.33.

Anasema Kanuni ya 59(1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 inataka mkataba wowote ulio rasmi utokanao na zabuni ambayo thamani yake ni Sh. bilioni moja au zaidi, uhakikiwe na Mwanasheria Mku wa Serikali kabla ya kutiwa saini na pande mbili.

"Nilibaini kuwa mkataba huu ulitiwa saini kabla ya kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia mkataba hauonyeshi wajibu wa pande zote mbili. Napendekeza Udom ihakikishe wajibu wa kila pande unaelezwa bayana kwenye mkataba na ujulikane kwa pande zote," Prof. Assad anasema.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad pia anabainisha kuwa Kifungu namba C.7.2.3 cha Miongozo ya Kiuhasibu ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kinawataka maofisa masuhuli kutekeleza majukumu yao kulingana na bajeti waliyojiwekea.

Anabainisha kuwa wakati wa mapitio ya bajeti na usimamizi wake, aligundua kutotumika kwa moduli katika mfumo wa vifungu vya bajeti ambao unaunganisha na matumizi halisi. Pia, bajeti iliyotengwa kwa kila vifungu husika katika mfumo wa uhasibu, hakuna maelekezo ya kila shughuli ambayo inayoainishwa na kasma husika ya malipo.

"Kutohusishwa kwa vifungu vya bajeti katika kila kasma kunasababisha ugumu katika kuweka viwango vya matumizi. Kutokuwapo kwa utengwaji wa mafungu katika kasma husika kunasababisha utekelezwaji nje ya bajeti.

"Napendekeza menejimenti ya Udom ihuishe mfumo wake kwa ajili ya kusaidia usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli kama zilivyoainishwa kwenye bajeti," Prof. Assad anashauri.

**MABILIONI YA MUHAS**

Katika ripoti yake hiyo, Prof. Assad pia anabainisha kuwa Desemba 16, 2014, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (Muhas) kiliingia mkataba na Sumsang C&T Corporation ya Korea Kusini kwa ajili ya kuleta na kufunga vitu mbalimbali, ukiwamo mfumo unaojulikana kama 'OCS 121 System Viewer'.

Mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu anabainisha kuwa mfumo huo ulifungwa Julai 26, 2017 kwa mkataba wa Dola za Marekani milioni 1.42.

"Nilipotembelea kuangalia ufanisi wa mfumo huo, nilibaini kuwa ulikuwa haujaanza kutumika kwa kuwa ulikuwa haujakidhi matakwa na vigezo vilivyokuwa vimebainishwa kwenye mkataba.

"Niliona pia mfumo huo haukuwa unaendana na matakwa ya watumiaji kwa kuwa ulikosa moduli zilizokuwa zimebainishwa kwenye mkataba na hivyo haukuwa tayari kutumika kama ilivyotarajiwa. Haya yalibainika wakati wa kufanya majaribio.

"Napendekeza Muhas kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa mzabuni ili kuhakikisha vitu vinavyokosekana katika mfumo huo vinapatikana ili ufanye kazi," Prof. Assad anasema.

**UPOTEVU MABILIONI MZUMBE**

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad pia anabainisha kuwa Chuo Kikuu cha Mzumbe kiliingia mkataba Na. PA/013/2015-16/GWND/22 na M/s. Afriq Engineering & Construction Co Ltd kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika ndaki ya Mbeya. Anasema ujenzi ulianza mnamo Septemba Mosi, 2016 na ulipaswa kukamilika Julai Mosi, 2017.

Anasema kuwa wakati wa ukaguzi wa mali za chuo Oktoba 2018, alibaini ujenzi bado haujakamilika lakini cheti cha maendeleo ya kazi kilibainisha malipo ya Sh. bilioni 1.42 yalikuwa yamekwishafanyika, sawa na asilimia 50 ya jumla ya gharama za ujenzi Sh. bilioni 2.8.

"Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Mzumbe kifanye uangalizi wa karibu ili kuhakikisha ujenzi unakamilika bila kuchelewa zaidi ili kupata manufaa yaliyotarajiwa," Prof. Assad anashauri.

**DOLA ZA MLIMANI CITY**

CAG Assad pia anabainisha kuwa kifungu namba 10.1 cha mkataba wa upangaji kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Kampuni ya Mlimani Holding Ltd (MHL) kinaitaka UDSM au wawakilishi wake kupitia vitabu vya Kampuni ya MHL kwa ajili ya kuthibitisha kiwango cha upangaji wanachotoza kwa wapangaji waliopo ndani ya majengo na huduma za maegesho zitolewazo.

Anasema kwa kipindi cha mwaka ulioishia Juni 30, 2018, imebainika UDSM haikutimiza majukumu yake ya kimkataba kwa kushindwa kupitia viwango vya tozo, hivyo kutegemea taarifa zitolewazo na Kampuni ya MHL.

Anabainisha kuwa jumla ya kiasi cha Dola za Marekani 10,869.9 na Dola 8,204.73 ziliwasilishwa kwa chuo kikuu kama kiwango cha gawio la mwaka kutokana na mgawanyo wa hisa katika mapato ya eneo la matangazo na maegesho ya magari.

Hata hivyo, Prof. Assad anabainisha kuwa amethibitisha UDSM haijafanya uhakiki wowote wa kujiridhisha na usahihi wa hesabu za mapato hayo na alibaini chuo hakina idadi kamili ya vikao na makongamano yaliyofanyika ndani ya Ukumbi wa Mikutano wa Malimani City, hivyo kutokuwa na uwezo wa kujua kiwango halisi cha mapato yaliyopatikana na kushindwa kumsimamia mpangaji.

"Ni dhahiri UDSM haiwezi kuthibitisha thamani halisi ya hisa zilizopo na kiwango cha gawio kinachostahili kulipwa. Napendekeza menejimenti ya chuo ifanye utafiti wa karibu na wa mara kwa mara, ikiwamo ukaguzi wa vitabu ili chuo kipate stahiki zake kwa usahihi kutoka kwenye mradi wa Mlimani City," Prof. Assad anasema.

**MAMILIONI YA ARU**

CAG Assad pia anabainisha kuwa mnamo Desemba 29, 2017, Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU) kilikopa Sh. milioni 601.73 kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

Anasema alibaini Kifungu XI(i) cha mkataba wa mkopo kinaitaka ARU ianze malipo ya mkopo Novemba 30, 2017, ambayo ni tarehe ya nyuma ikilinganishwa na tarehe ya mkopo.

"Malipo mengine yanapaswa yafanyike kila mwaka kwenye tarehe ya malipo ya mkopo wa kwanza. Kuchelewa kutolewa kwa mkopo kumeongeza riba na kupungua muda wa kulipa mkopo. Ninapendekeza ARU ifanye mawasiliano na TEA ili kubadilisha muda wa kulipa mkopo huo," Prof. Assad anashauri.

## Jaji asitisha kesi mauaji

INATOKA UK. 3

upande wa utetezi yalikuwa kama ifuatavyo:

**Wakili Shilatu:** Ulielezwa na nani Chacha amefanya mauaji?

**Shahidi:** RCO

**Wakili:** Kielelezo kinapotokakwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kuna fomu namba 16 ya kujaza?

**Shahidi:** Ndio

**Wakili:** Hujaileta hapa mahakamani?

**Shahidi:** Sijui kama imeletwa sio kazi yangu

**Wakili:** Uliona mshtakiwa wa kwanza akimuua?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Mshtakiwa wa pili na wa tatu uliwaona wakiua?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Ulikuwa eneo la tukio la mauaji?

**Shahidi:** Hapana, Chacha alikueleza wewe ni Polisi wa tofauti na wengine?

**Shahidi:** Ndiyo

**Wakili:** Chacha alikueleza askari wengine walimpiga?

**Shahidi :** Ndiyo

**Wakili:** Unashughulika na watu wakiwa mahabusu Kituo cha Polisi?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Chacha alikueleza aliteswa na askari na kuingizwa kitu kigumu ndani ya mwili wake?

**Shahidi:** Hapana

**Wakili:** Ulimnyima Chacha nafasi ya kungea na Wakili wake?

**Shahidi:** Sio kweli

**Wakili:** Ulimhoji Chacha usiku?

**Shahidi:** Ni kweli

**Wakili:** Ni kweli mawakili hawafanyi kazi usiku?

**Shahidi:** Sijui.

## Shahidi aeleza mazito kesi ya kina Mbowe

INATOKA UK. 2

uliwarudia na moshi wake uliwarudia askari, wawili kati yao walianguka chini kwa kujeruhiwa akiwamo Konstebo Fikiri na Koplo Rahmu kujeruhiwa.

"Nililazimika kutoa ilani kwa mara ya tatu, nikawaamuru askari wenye silaha ya moto kusonga mbele wakapiga risasi juu kuwatawanya, katika tukio hilo pia alijeruhiwa Akwirina na baadaye alivyopelekwa hospitali ya Mwananyamala alifariki," alidai bosi huyo wa Jeshi la Polisi.

Alidai kuwa baada ya zile risasi kuanza kupigwa hewani, alimwona Mbowe akitimua mbio na kutawanyika.

"Mheshimiwa nilikuwa sijui kama Mbowe anajua kukimbia alitimua mbio mpaka miwani yake ilianguka," alidai SSP Rich.

Aidha, shahidi alidai kuwa anawatambua washtakiwa na kwamba aliwaona siku ya tukio.

Jopo la mawakili wa utetezi liliongozwa na Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, Hekima Mwasipu, Jeremia Mtobesya na John Mallya.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya wakili Kibatala na shahidi:

**Kibatala:** Je, shahidi uliwahi kufanya mahojiano na wenye maduka baada tukio na ulichukua maelezo?

**Shahidi:** Hapana.

**Kibatala:** Katika ushahidi wako umemtaja Akwilina unaweza kumtaja majina yake yote mawili?

**Shahidi:** Sijui.

**Kibatala:** Kuhusu kufyatua risasi, je, zilitumika ngapi?

**Shahidi:** Risasi baadhi zilienda hewani na nyingine sifahamu.

Kesi hiyo itaendelea ushahidi wa Jamhuri Mei 13, 14 na 15, mwaka huu.

Mbali ya Mbowe, wengine ni, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Bunda Ester Bulaya, Mbunge wa Tarime Mjini Esther Matiko, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu Taifa, Vicent Mashinji, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na John Heche.

HABARI KITAIFA

# Wakulima walia kwa RC vanila yao kuibwa usiku

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya wakulima wa vanilla wilayani Missenyi mkoani Kagera wamesema wanalala katika mashamba yao kulinda vanila yao isiibwe.

Wakitoa malalamiko yao mbele ya mkuu wa mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, katika Shule ya Sekondari KADEA Kata ya Kanyigo, Mwalimu Jovin Mbanga alisema wizi wa vanila changa na marando ya zao hilo unafanywa usiku na Watanzania wasio wazalendo kwa kushirikiana na walanguzi kutoka nje ya nchi.

Walisema pia wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwapo kwa soko rasmi la kuuza vanila inapokomaa na baadhi ya wanunuzi kutosajiliwa ili kutambuliwa na serikali kwa lengo la kuwawezesha kuuza vanila kwa mnunuzi rasmi.

Walisema Watanzania wanaoshirikiana na wafanyabiashara wa nje ya nchi wanapewa fedha kwa ajili ya kulangua vanilla yao inayovunwa usiku ikiwa changa pamoja na marando, ambavyo huuzwa katika nchi jirani.

Akijibu malalamiko hayo baada ya kutembelea shamba la Mwalimu Mbanga, Gaguti aliagiza kuwa kuanzia sasa vanila itakuwa na muda maalum wa kuvunwa mashambani na kutakuwa na vituo maalum kama masoko ya kununulia, na kuwa wafanyabiashara ni marufuku kwenda moja kwa moja kwa wakulima kununua zao hilo likiwa shambani.

Alisema mtu atakayekamatwa na vanilla kabla ya tarehe ya kuvunwa kutangazwa, atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani na kufunguliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Aidha, aliwataka wakulima wa vanilla kujiunga katika ushirika wa vyama vya msingi, ili iwe rahisi kubaini wezi, na kuwa na soko la uhakika.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia kuuza vanilla imeongezwa thamani ili kupata bei nzuri zaidi, na kuweka urahisi zaidi wa serikali kuwasimamia wakulima kama ushirika kuliko mwananchi mmoja mmoja.

Pia aliwataka wafanyabiashara wote au makampuni yote yanayojihusisha na ununuaji wa vanila, kujisajili na kupewa leseni, kwa kuwa kwa sasa baadhi ya wanunuzi hawajasajiliwa, na kusisitiza taasisi au kampuni ambayo yanatoa ruzuku kwa wakulima wa zao hilo, wanunue vanilla kulingana na bei ya soko na si kuwanyonya wakulima.

"Natoa rai kwa watendaji wa vijiji na kata kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu kama wanataka kuendelea kubaki kazini, hasa jukumu la ulinzi na usalama, kwa mfumo wa Nyumba Kumi Bora za Usalama ambao utasaidia kuwabaini kirahisi wezi wa vanilla na wahalifu wengine," alisema Gaguti.

Mwaka 2017/18 bei ya vanilla mkoani Kagera ilifikia kati ya Sh. 100,000 hadi 150,000, na siku za nyuma iliwahi kuzalishwa mkoani Kagera hadi kufikia tani 103, lakini kwa sasa zinazalishwa tani 10 hadi 12.



Wachuuzi wa matunda wakisaka wateja katika eneo la Gerezani, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# WB yawekeza asilimia 50 kwenye nguvu kazi

**Na Salome Kitomari**

BENKI ya Dunia (WB) imesema kuwa itawekeza kwa zaidi ya asilimia 50 kwenye miradi yenye kuongeza ujuzi kwa wananchi wa nchi za Afrika Tanzania ikiwamo, katika kukuza uchumi wao na nchi zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Benki hiyo hivi karibuni na Naibu Rais wa Benki ya Dunia kwa Afrika, Hafez Ghanem, mpango wa sasa ni kuwekeza kwenye nguvu kazi kwa zaidi ya asilimia 50.

Taarifa hiyo ilizinduliwa wakati wa mikutano ya Spring-iliyoandaliwa na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF ya Spring), na mpango huo pamoja na mambo mengine unalenga kuwawezesha wasichana kukabiliana na ndoa za utotoni.

Alisema kiwango hicho ni sawa na Dola za Marekani bilioni 15 hadi kufikia mwaka wa fedha wa 2021 hadi 2023, lengo likiwa ni kuongeza uelewa, uwezo na utambuzi wa mambo mbalimbali kwa wananchi.

"Benki ya Dunia itaangalia wale wanaoweza kuleta mabadiliko kwenye maeneo husika ikiwamo kwenye ubunifu na tekonolojia," alisema. Ghanem alisema lengo la mpango huo ni kusaidia nchi za Afrika kuimarisha mitaji yao ya kibinadamu, na hasa kuwawezesha vijana wa Afrika kukua na afya bora na wenye uwezo wa ujuzi wa kushindana katika uchumi wa kimataifa.

Alisema Pato la Taifa kwa kila mfanyakazi Kusini mwa Jangwa la Sahara linaweza kuwa mara mbili zaidi, ikiwa kila mtu atakuwa na afya na elimu nzuri kuanzia ngazi ya msingi. "Kiwango cha uzazi wa vijana Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ni wazaliwa 102 kwa wasichana 1,000 - mara tatu kama vile Kusini mwa Afrika.

Makamu huyo alisema benki hiyo iko tayari kuzisaidia nchi za Afrika kuja na mikakati mipya ya kuwekeza kwa watu wao kwa ubora zaidi.

Naye, Makamu wa Rais wa Maendeleo ya Binadamu, Annette Dixon, alisema nchi 23 za Afrika zitanufaika kwa asilimia 60 na utazifikia kaya mbalimbali.

# DC aagiza vigogo h/shauri kukamatwa

**Na Consolata Evarist,** GEITA

MKUU wa Wilaya ya Chato mkoani Geita, Mtemi Msafiri, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mganza, Daud Mazoya na Afisa Manunuzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Salum Madunda kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa kituo hicho.

Alitoa agizo hilo kufuatia agizo lililotolewa hivi karibuni na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, aliiagiza Taasisi ya kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kuuchunguza mradi akidai kuna ubadhirifu wa fedha.

Mkuu wa wilaya alisema viongozi hao wamefanya ubadhirifu wa zaidi ya Sh. milioni 27, ambazo walifanya udanganyifu katika ubebaji wa lori la mchanga badala ya kubeba kwa Sh. 25,000 walikuwa wanabeba kwa Sh. 35,000 ambazo zimepelekea fedha kuisha na jengo kutokamilika.

"Iweje leo kwenye kituo cha afya ipelekwe elfu 35, ni haki hiyo, niliwaambia hizi fedha za serikali awamu hii ni kama sumu, mtu ambaye atajaribu kuzigusa hawezi kuwa salama, OCD watu wako hawa waweke ndani," aliagiza Msafiri.

Diwani wa Kata hiyo, Mwita Tagata, aliwaondoa hofu wananchi ambao walishiriki kwa nguvu zao kujenga kituo hicho kwa kuwahakikishia atasimamia kikamilifu ili waweze kuondokana na adha ya ukosefu wa kituo cha huduma ya afya.

"Matatizo yote yanaenda kufutika, tunachohitaji kituo chetu kifanye kazi kwa hiyo kituo kitakamilika na kitaanza kufanya kazi, muondoe zile hofu," alisema Tagata.

Rose Kidiku, mkazi wa kata ihiyo, alimuomba DC Msafiri kuhakikisha anafuatilia kwa ukaribu ujenzi huo ili ukamalike kwa kuwa wajawazito wanateseka kufuata huduma katika hospitali zingine wakati wa kujifungua.



Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, akijibu swali bungeni jana. **PICHA: WIZARA YA KILIMO**

# Tumbaku sasa mbioni kuuzwa Algeria, Misri

BUNGE limeelezwa kuwa mazungumzo ya kupeleka tumbaku kwenye nchi za Misri na Algeria yamefikia hatua nzuri na yanatarajiwa kufungua milango ya soko la zao hilo.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Kilimo, Innocent Bashungwa, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo (CCM), Edwin Ngonyani.

Katika swali lake, Ngonyani alihoji wizara hiyo inashirikianaje na wizara nyingine zinazohusika na uwekezaji wa mambo ya nje kutafuta soko la tumbaku nchini Misri badala ya kulazimika kutumia nchi za Uganda na Kenya peke yake. Akijibu swali hilo, Bashungwa alisema makubaliano hayo yakikamilika Tanzania inaweza pia kuuza chai nchini Misri na Algeria kwa faida kuliko ilivyo hivi sasa au badala ya kuuza chai kupitia mnada wa Mombasa nchini Kenya. Alifafanua kuwa mwaka 2014/15 uzalishaji wa tumbaku ya Moshi ulisimama mkoani Ruvuma kutokana na kukosa soko.

"Jitihada za serikali ikawezesha Kampuni ya Premium Active Tanzania Limited(PATL) kuonyesha nia ya kununua tumbaku hiyo ya DFC ambayo hapa nchini huzalishwa Namtumbo na Songea Vijijini mkoani Ruvuma," alisema.

Bashungwa alisema kampuni hiyo ilieleza kuwa lipo soko kubwa la tumbaku aina hiyo nchini Misri na Algeria, lakini tumbaku ya Tanzania inauzwa kwa bei ya juu kutokana na kodi inayotozwa ikilinganishwa na aina hiyo kutoka nchi za Uganda na Kenya.

"Kwa kuwa nchi za Uganda, Kenya, Algeria na Misri ni wanachama wa Jumuiya ya Soko la Pamoja la Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (COMESA) na kwa hiyo kodi za kuingiza tumbaku, chai na bidhaa nchini Algeria na Misri kutoka Kenya na Uganda ni za chini," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema ili nchi iuze tumbaku, chai, bidhaa nyingine katika nchi za Algeria na Misri kwa faida, inatumia nchi zilizo kwenye jumuiya hiyo kama Uganda na Kenya.

"Kutokana na hilo, Wizara inashirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Viwanda na Biashara kuanzisha mazungumzo na nchi wanachama wa COMESA na nchi kama Misri na Algeria kupitia balozi zetu ili kuandaa makubaliano maalum yatakayowezesha nchi yetu kupeleka tumbaku katika nchi hizo kwa kodi nafuu," alisema.

# Serikali yafafanua muda kumaliza elimu ya msingi

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imesema kwa sasa hakuna haja ya kubadilisha muda wa kuhitimu elimu ya msingi na kusisitiza kuwa miaka saba iliyopo hivi sasa inafaa.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri, William Ole Nasha, wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali inasemaje kuhusu kutotekelezwa kwa eneo la sera ya elimu ya kuishia darasa la sita badala ya darasa la saba.

Pia alihoji lini serikali itapitia upya sera ya elimu kwa lengo la kuongeza tija na kuendelea na mahitaji ya sasa.

"Ni kwa kiasi gani imezingatia ubora wa elimu?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema sera sio msahafu na kwa hiyo serikali inabadilisha sera kwa kadri inapoona inafaa kwa wakati husika.

Alibainisha kuwa kwa wakati huu kwa sasa elimu kuanzia darasa la kwanza hadi la saba sio kitu kibaya.

"Hatuna haja ndio maana tumebakia na mfumo wa zamani, na hatujavunja sheria na kwa sasa tupo katika mapitio kwa mambo mapya yaliyoko katika sera ya elimu ambayo tuliona hatutaweza kutekeleza," alisema. Ole Nasha alisema serikali inazingatia ubora wa elimu ndio maana kumetokea mabadiliko makubwa katika idara ya udhibiti wa elimu.

"Umeanza mtindo mpya wa udhibiti ubora kwa ushirikishwaji ambao unawaleta wadau wote kwa pamoja na tutahakikisha wanapata vifaa na ofisi ili kuhakikisha kuwa elimu inakuwa bora," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 imebaini baadhi ya maeneo na mchakato wa kupitia upya sera hiyo unaendelea na wakati mwafaka ukifika watawashirikisha wabunge.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mtambile (CUF), Masoud Abdallah Salim, alihoji kauli ya serikali kwa kuwa imekuwa ikiahidi bungeni kuboresha maslahi ikiwamo posho ya kufundishia ni waratibu elimu na wakuu wa shule.

Ole Nasha akijibu swali hilo, alikiri kuwa maslahi ya walimu ni muhimu katika kuwaweze kufanya vizuri na serikali inapitia upya maslahi ya watumishi wa umma wote wakiwamo walimu ili tuweze kuwa na maslahi yanayoendana wakati sasa.

## Kata zaahidiwa mawasiliano simu

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, amesema serikali itakamilisha kazi ya kuzipatia mawasiliano ya simu kata za Kitanga na Kirumbi katika kipindi cha miezi sita ijayo.

Nditiye alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdalah Chikota, aliyetaka kujua ni lini kata hizo zitapatiwa huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani.

Chikota alisema kata hizo hazina huduma ya simu ingawa kazi hiyo ya kujenga minara walipewa TTCL na mpaka sasa bado.


Akijibu swali hilo, Nditiye alikiri kuwa kata hizo hazina huduma ya mawasiliano na kwa sasa mkandarasi anakusanya vifaa vya kuanza kazi hiyo ya ujenzi ili aende kwenye eneo la ujenzi.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Lulindi (CCM), Jerome Bwanausi, alitaka kujua ni lini serikali itajenga minara ya simu katika kata za Sindano, Lipumbara, Namtona, Mcharu, Chikolopola na Mkundi ikiwa ni ahadi ya serikali.

Nditiye akijibu swali hilo, alisema serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote iliviainisha vijiji vya kata za Sindano, Lipumburu, Namtona, Mchauru, Chikolopota na Mkundi kwa ajili ya tathmini kuangalia mahitaji halisi ya mawasiliano.

"Baada ya tathmini husika kukamilika serikali kupitia mfuko huo iliviingiza vijiji vya kata za Mchauru katika mradi wa Mpakani na kanda maalum unaotekelezwa unaotekelezwa na Kampuni ya simu ya Tigo (MIC)," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema vibali vya ujenzi kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) vimeshapatikana, hivyo kampuni ya Tigo inategemea kuanza ujenzi wa minara sambamba na kufunga vifaa vya mawasiliano mara moja.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# TRA wateketeza kemikali zilizokuwa zikivushwa nje

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Arusha, imeteketeza zaidi ya lita 8750 za kemikali bashirifu (ethanol alcohol) zenye thamani ya Sh. milioni 60 zilizokuwa zikivushwa kuelekea nchi jirani ya Kenya bila kufuata taratibu za kisheria.

Akizungumza na Meneja Msaidizi wa TRA Mkoa wa Arusha, anayeshughulikia Forodha, Godfrey Kitundu, alisema kemikali hizo zilikamatwa tangu Juni 2017 na Jeshi la Polisi na ilipofika Machi 2, 2018 ilikabidhiwa kwa TRA Kituo cha Forodha cha Pamoja, (OSBP).

Alisema kemikali hizo zilikamatwa na Jeshi la Polisi mpaka wa Namanga katika doria zao za kila mara na baada ya hapo walikabidhi TRA kwani walikuwa wakipita njia za panya kwa kukwepa kodi pia.

Alieleza kuwa gari hiyo ilikuwa na madumu ya lita 250 takribani 35 yenye kemikali hizo, ambazo ni hatari kwa jamii japo zinatumika kwa matumizi mbalimbali

Alifafanua kemikali hiyo hutumika kutengenezea pombe kali, manukato na hata dawa, lakini pia hutumika kutengenezea dawa haramu ya kulevya aina ya cocaine.

"Kemikali hizo zinaonekana zimetoka nchi ya Pakistani na lndia, na kwamba haikuzalishwa hapa Tanzania," alisema.

Alisema baada ya kukagua na kugundua msafirishaji wa kemikali hizo hakuwa na kibali chochote, hivyo, walichukua sampuli na kupeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya vipimo zaidi.

Aidha, alisema gari yoyote inayohusika kubeba vitu vya magendo hutozwa faini mpaka dola za Kimarekani 5000, au kutaifishwa na kuuzwa kwenye mnada wa forodha.

Gari hiyo kwa vile imebeba mzigo ambao ni wa magendo lilitolewa hati ya kushikiliwa na hivyo taratibu zą kiforodha kukamilisha adhabu stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Forodha zinakamilishwa.

Hata hivyo, aliwataka wafanyabiashara kufanya biashara kwa kufuata sheria za nchi na taratibu zake kuepusha usumbufu wa mara kwa mara.

Mkaguzi wa kemikali OSBP, Nesto Mwilonga, alisema baada ya kupeleka kemikali hiyo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ilibainika imeshaisha muda wake.

"Kemikali hii inateketezwa kwa sababu imeisha muda wake wa matumizi," alidai Mwilonga.

Naye Msaidizi wa Polisi Kituo cha Namanga, Ernesta Mwambinga, alieleza gari lililokuwa linasafirisha kemikali hiyo ilikamatwa ikipita njia za panya maeneo ya kisongo ndani ya eneo la Namanga.

Alisema Juni 28, 2017 polisi wakiwa kwenye doria za kawaida za kuthibiti wahalifu wa dawa za kulevya na magendo mpakani, ndipo walipoikamata gari hiyo ikiwa inavuka kuelekea nchi jirani ya Kenya.

Alisema walivyoikamata walikagua nakukuta imepakia kemikali hiyo na haina vibali, hivyo walilazimika kuikabidhisha TRA.

Alisema gari waliyoikamata ni mali ya Policarp Lubuva mkazi wa Arusha yenye nambari T 132 CWX aina ya Mitsubishi Canter.



Imamu Msaidizi wa Taasisi ya Masjid Noor Mji mdogo wa Mirerani Wilayani Simanjiro Mkoani Manyara, Mohamed Hassan akichangia damu kwa kituo cha afya Mirerani, kwenye maadhimisho ya miaka 1,440 ya Maulid (mazazi) ya Mtume Muhammad S.A.W juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TBS wakumbana nguo za ndani sokoni

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NGUO za ndani za mitumba zilizopigwa marufuku kuingizwa nchini na kuuzwa zimekamatwa zikiuzwa katika soko la Krokoni, jijini Arusha, huku wafanyabiashara wakijua hilo ni kosa.

Maofisa kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), walifanya operesheni ya kushtukiza sokoni hapo. Operesheni ya ukaguzi huo ilifanyika juzi na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania, (TBS).

Akizungumza katika soko hilo juzi, Ofisa Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, alisema lengo la kufanya ukaguzi huo ni kufuatilia kama katazo la serikali linazingatiwa na wafanyabiashara.

Alisema katika ukaguzi huo wamebaini baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka sheria na maagizo ya serikali yanayotolewa na kuendelea kuuza nguo zilizokatazwa.

Alitaja baadhi ya nguo walizofanikiwa kuzikamata katika soko hilo ni taulo, nguo za kulali, chupi, sidiria na soksi.

"Sasa bidhaa hizi sisi tumezikamata na tunazipeleka kuteketeza kwa gharama zetu sababu hawa wafanyabiashara wadogo hatuwatozi gharama za kuteketeza, ila wale wafanyabiashara wakubwa tukiwakamata na bidhaa hizi tunawatoza faini na pia wanalipa gharama zote zakuteketeza," alisema.

Roida aliwaomba wafanyabiashara kufuata sheria na maagizo yanayotolewa na serikali ili kuepuka kuingia gharama na kupata hasara zinazojitokeza pale wanapokamatiwa mizigo yao.

Naye Mkaguzi wa TBS, Lucas Gwila, alisema wamefanya ukaguzi huo katika Soko la Mitumba la Krokoni ili waweze kuondoa bidhaa hafifu na zisizokidhi kiwango cha 758 cha mwaka 2003.

Alisema ni vema wananchi na wafanyabiashara wakaachana na matumizi ya bidhaa hizo kwa faida ya afya zao, kwani baadhi ya nguo hizo zinamadhara mengi ikiwamo kupata magonjwa ya kuambukiza ya ngozi na kushindwa kutibika.

Alisema kutokana na nguo hizo zilizokatazwa kuingia sokoni walishatoa semina kwa wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza mitumba na mizigo na wanaelewa.

"Sasa kinachofanyika, baadhi yao siyo waaminifu wanaendelea kuagiza na kuzipitisha njia za panya na matokeo yake yanamgharimu mfanyabiashara mdogo kama huyu na sisi tukikuta tunafuata sheria ya kuziondoa bidhaa hizo sokoni hata kama hatujamkuta mfanyabiashara mwenyewe katika bidhaa zake," alisema. Mkaguzi mwingine wa TBS, January Faustine, alisema kabla ya kuanza kukamata bidhaa hizo walifanya jitihada za kumtafuta kiongozi wa soko na kuwaomba endapo wanahitaji elimu ya kufahamu zaidi bidhaa zilizozuiwa wawaeleze watakuja kuwapatia.

"Tumefanya hivi sababu baadhi yao wanadai hawakufahamu kama taulo zimekatazwa, lakini cha kushangaza wakituona baadhi yao wanazificha kama hawafahamu zimekatazwa kwanini wanazificha, ni vema wafahamu zoezi hili endelevu tutakuja mara kwa mara kukagua," alihoji.

# Waziri Kigwangalla atamani teknolojia kutangaza utalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, amesema Tanzania inahitaji kuwa na mpango imara wa kutumia teknolojia ya digitali kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini vijulikane zaidi tofauti na ilivyo sasa.

Alisema kitendo cha kutangaza vivutio hivyo kutasaidia kumudu ushindani mkali katika sekta hiyo kimataifa na hatimaye kupata watalii wengi zaidi na kuongeza pato la taifa.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika ufunguzi wa kongamano la kimataifa la kuzungumzia utalii na hatima ya baadaye lililoandaliwa na Kitivo cha Utalii cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na kuwakutanisha wadau na wasomi katika sekta hiyo.

"Bado Tanzania haijafikiwa kujitangaza katika kiwango kinachotakiwa, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anakuwa sehemu ya kutangaza vivutio hivyo ili viweze kujulikana kitaifa na kimataifa pia," alisema.

Makamu Mkuu wa OUT, Profesa Elifas Bisanda, alisema umefika wakati sasa nguvu ikaelekezwa katika kuvitangaza vivutio vya utalii ambavyo bado havijafahamika vyema hata kwa Watanzania wenyewe.

Alisema bado kuna changamoto ya kuhakikisha vivutio vya utalii vinatangazwa kwa bidii hapa nchini na kuweza kujulikana kwa kuwa bado mwamko ni mdogo hata kwa Watanzania wenzetu kuvifahamu vivutio hivyo.

Naye Mkuu wa Kitivo cha Utalii, Dk. Felician Mutasa, alisema kongamano hilo litasaidia kukuza uelewa wa uwepo wa vivutio vingine vilivyopo hapa nchini tofauti na wanyamapori.

Aidha, alisema mpango huo utasaidia pia kupanua wigo wa huduma kwa watalii wanaoingia nchini na kuongeza idadi ya watalii zaidi.



Sehemu ya watu wenye usonji na wenye mahitaji maalum kutoka maeneo mbalimbali, walipokutana katika Kituo cha Ufundi Orkolili, Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro jana, kujadili namna wanavyoweza kupata ujuzi ili kwenda sambamba na Sera ya Tanzania ya Viwanda. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Watafiti Marekani waanza utafiti mazingira ya elimu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

JOPO la watafiti 24 kutoka Chuo Kikuu cha Maendeleo ya Kimataifa cha Shiefield cha nchini Marekani, wameanza utafiti mdogo kuhusu mazingira ya elimu katika maeneo ya vijijini kutokuwa rafiki kwa wanafunzi wa kike.

Kiongozi wa msafara wa wanafunzi kutoka chuo hicho, Debra Spoton alisema pia wanafanya utafiti kuhusu tatizo la kukosekana kwa majisafi na salama na athari za uharibifu wa mazingira.

Alikuwa akizungumza wakati wa uwasilishaji wa matokeo ya utafiti na sababu walizobaini katika maeneo ya vijijini katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Akitoa matokeo hayo, Debra ameeleza kuwa mazingira ya elimu kwa mtoto wa kike siyo ya kuridhisha kutokana na wengi wao kutembea umbali mrefu na kukutana na vishawishi.

"Madhara yaliyojitikeza katika tafiti hiyo ni uchovu na kukosa usafiri vinachangia kwa kiasi kikubwa wanafunzi wa kike kupata ujauzito katika umri mdogo na hivyo kukatisha ndoto zao za masomo,"alisema mtafiti huyo.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, changamoto hizo zinaweza kutatuliwa kwa wananchi kupewa elimu kuhusu uchangiaji wa maendeleo ya elimu na ujenzi wa mabweni au hosteli.

Alisema kuna ulazima kwa watoto wa kike kupewa elimu sawa na watoto wa kiume na kuthaminiwa na jamii au koo za maeneo husika.

Kuhusu tatizo la majisafi na salama na uharibifu wa mazingira vijijini ambalo linatishia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja, watafiti hao wamedai linaweza kutatuliwa kwa serikali na wahisani kujenga miradi ya maji. Walipotafutwa kutoa maoni yao, baadhi ya wakazi wa Moshi Vijijini akiwamo Latifa Mvungi wameeleza kuwa changamoto kubwa za elimu zinachangiwa na mazingira magumu ya maisha kwa watoto wa kike kupata ujauzito.

Kwa upande wake, Meneja Mradi wa Taasisi ya Mazingira na Maendeleo Vijijini (Keda), Emanuel Mganga ameeleza kuwa kutokana na changamoto za upatikanaji wa huduma za majisafi na salama, watafiti hao wametoa vifaa vya kupima maji.

Vifaa hivyo ni kwa ajili ya kupima maji, baada ya kubainika kuwepo kwa madini mengi ili kuweza kuyatibu na kutumika kwa matumizi ya binadamu.

# Butiku awaita wazawa kukuza uchumi wao

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZAWA wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wana uwezo mkubwa kiuchumi pamoja na wasomi waliowekeza katika mikoa mingine na nchi mbalimbali duniani, wameitwa kuwekeza katika ardhi yao ili kuinua uchumi wao.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation, Joseph Butiku ametoa wito huo wakati alipokuwa akizungumza na viongozi wa dini, wanasiasa, wananchi na viongozi wa serikali katika mdahalo wa kujadili uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Mimi nadhani kuna kila sababu ya wasomi wanaotokea mkoa wa Kilimanjaro pamoja na watu wenye uwezo wa kiuchumi kurudi tena nyumbani kuangalia namna ya kuuletea maendeleo mkoa wao na waache tabia ya kutumiwa kuletea maendeleo nchi nyingine bila ya kuangalia nchi yao.

"Lakini pia kuna jambo muhimu mnapaswa kulifikiria ni aina ya siasa mnayofanya. Bila haki na amani, maendeleo hayawezi kupatikana, kwa hiyo ni lazima kuwapo na siasa safi."

Butiku ametaka viongozi wa Kilimanjaro na hasa viongozi wa serikali na watumishi wa umma kuwahudumia wananchi na kuhamasisha maendeleo kuanzia ngazi ya vijiji hadi serikali kuu kwa kufuata mfumo wa ugatuzi wa madaraka.

Katika muktadha huo, wananchi wanapaswa kushirikishwa katika mijadala na maamuzi mbalimbali ya maendeleo ili kuweka dhana ya ushirikishwaji kutatua changamoto zilizopo kwa wananchi wengi hasa maeneo ya vijijini.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, akizingumza katika mdahalo huo alisema viongozi wengi wanashindwa kuwashirikisha wananchi katika fursa za maendeleo maeneo ya vijijini.

Dk.Mghwira ameeleza: "Endapo wananchi watashirikishwa kupitia viongozi wa vijiji, wananchi watapata fursa zaidi kushiriki katika maendeleo na niwatake viongozi wote tuzingatie suala la ugatuzi wa madaraka ili kuondoa utata wa utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria za utumishi wa umma."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Michael Kilawila alieleza masikitiko yake kuwa wananchi wengi wanashindwa kushirikishwa kwa sababu ya itikadi za vyama vya siasa.

# Halmashauri yamwaga mikopo kwa vikundi 20

**Na Paul William,** SIHA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, imetoa Sh. milioni 59 kama mkopo kwa vikundi 20 vya wanawake 479 wanaotarajia kunufaika na mikopo isiyo na riba.

Akikabidhi hundi kwa vikundi hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo alisema fedha hizo ni maelekezo ya serikali kwa kila halmashauri kuhakikisha zinatenga fedha asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Hokororo aliiitaka halmashauri hiyo kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya walemavu zinawafikia walengwa ili kuhakikisha na wao wanajikwamua kiuchumi na kuondokana na kuwa tegemezi.

"Akina mama niliowakabidhi mikopo leo tulianza kwa mafunzo ya ujasiriamali, ni vyema mkatumia mafunzo hayo kujinufaisha kupitia fedha hizi ili kuonyesha matokeo ya haraka kupitia fedha hizi na sio kwenda kuchangia harusi au kununulia vitenge" alisema Hokororo.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa, wakinamama wanapopata fedha wamekuwa na tabia ya kufanya kazi kwa kufwatishana na kwa kutaka wakinamama hao kuacha tabia hiyo na kuwa wabunifu wa biashara ili kuhakikisha fedha hizo zinawakomboa kiuchumi.

Aidha aliwataka kuhakikisha wanarejesha fedha hizo kwa wakati ili ziweze kuwanufaisha vikundi vingine ambavyo havijapatiwa mkopo huo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Siha, Valerian Juwal alisema kuwa, halmashauri hiyo imekuwa ikitenga fedha asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo mwaka 2016/17 halmashauri hiyo ilishika nafasi ya sita kitaifa na ya pili kimkoa kwa kutoa mkopo wa milioni 56 huku ya kwanza ikiwa ni halmashauri ya Moshi.

Juwal aliasema kuwa, mwaka 2017/18 halmashauri hiyo ilishika nafasi ya tisa kitaifa na ya pili kimkoa ambapo jumla ya mkopo wa milioni 45 ulitolewa na kudai kuwa kwa sasa wamejipanga kuhakikisha kuwa mwaka huu inashika nafasi ya kwanza kwa utoaji wa mikopo kwa vikundi hivyo.

Naye Ofisa Maendeleo wa Halmashauri hiyo, Alfoncina Makele alisema changamoto wanayokabiliana nayo ni uhitaji wa mikopo kuwa mkubwa ikilinganishwa na fedha zilizopo ambapo vikund vingi vimekuwa vikihitaji mikopo hiyo na hii inatokana na uwepo wa mwamko mkubwa wa uundwaji wa vikundi.

Changamoto nyingine ni baadhi ya vikundi kuchelewesha urejeshaji wa fedha hali ambayo imekuwa ikikwamisha fedha hizo kusaidia vikundi vingine ambavyo havikupata mikopo hiyo.

# ama

ALHAMISI APRILI 18, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 18

**WHO: Wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume**



Ukurasa 16

Ajali ilivyompokonya mguu



Ukurasa 14

**Kila glasi ya kilevi, inakaribisha kupooza**




## DARASA LA PROF. KAISI:

# Kazi, dawa, mavazi ya wanaume kizuizi cha mimba kilichojificha

Ukurasa 19

## Kila glasi ya kilevi, inakaribisha kupooza

MTU anapoonja kilevi japo glasi moja, basi afya yake inakuwa jirani na shinikizo la damu, inaeleza matokeo ya utafiti wa miaka 10 iliyowahusu Waingereza na Wachina 500,000.

Katika tafsiri yake, inaelezwa vilevi mara zote vina hatari kubwa ya mtu kupata maradhi ya kupooza na suluhisho bora kwa wanywaji ni kuacha imapobidi au kutumia kiwango kidogo.

Vyuo vikuu vya Peking na Oxford, katika matokeo yao ya utafiti vimebaini mambo kadhaa, kwamba: Wastani wa chupa moja au mbili ya bia, au kinywaji cha kiwango hicho kwa siku, inamweka mnywaji hatarini kwa asilimia 10 hadi 15.

Pia, matumizi ya chupa nne yanamsogeza zaidi katika hatari ya kiwango cha asilimia 35 ya mwili kupooza.

Mtaaluma Profesa David Spiegelhalter, kutoka Chuo Kikuu cha Cambridge, Uingereza, anasema kadri kunakuwapo ongezeko la kinywaji cha wine japo kwa nusu glasi, basi kuna uwezekano wa shinikizo la damu kwa wastani wa asilimia 38.

Pia, utafiti huo unaeleza kwamba, hakuna kiashiria cha nafuu kwamba, kunywa kidogo kunamweka mtu salama.

**Kwa mujibu wa mtandao.**



Kilevi katika glasi. **PICHA: MAKTABA**

MAZINGIRA

PORI LA AKIBA SELOUS

# Kukomesha ujangili kumenusuru mazingira ndani ya hifadhi Rufiji

- Wahalifu waweka silaha zao chini
- Wanyama zaidi, majeruhi wafidiwa



Mandhari ya Kijiji cha Mloka, Rufiji. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Beatrice Shayo,** aliyekuwa Rufiji

ELIMU ya kirafiki ilivyowateka majangili kuwasilisha silaha zao na kuachana na vitendohivyo, baadhi yao kuwasaidia katika mapambano.

Akizungumza na Nipashe, Mhifadhi wa Wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Robert Kiondo, anasema elimu waliyoitoa imesaidia kwa kiasi kikubwa na sasa wanapatiwa ushirikiano.

Kiondo anasema, mwaka jana waliwaita watu waliodaiwa kujihusisha na ujangili na kuwajulisha kile wanachotuhumiwa nacho.

"Kabla ya kumchukulia mtu hatua, tuliona tutumie njia mbadala ya kuwaita. Tuliwaita zaidi ya 10 na kukaa nao tukawajulisha tuhuma zao, lakini na sisi tulikuwa tunawasilikiza na wao wanasemaje na baada ya hapo tukawapa onyo kwa njia ya mazungumzo," anasema.

"Wengine walionyesha ushirikiano na wengine waliahidi kutojishughulisha tena na vitendo vya ujangili. Sisi kazi yetu sio kuzui tu, ila ni pamoja na kutoa elimu na kuwajulisha vitendo vya ujangili.

"Sio vizuri na kama kuna ugumu wa maisha, mnaweza kufanya shughuli nyingine za kiuchumi kama kilimo, lakini sio ujangili," anasema.

> **"Sio vizuri na kama kuna ugumu wa maisha, mnaweza kufanya shughuli nyingine za kiuchumi kama kilimo, lakini sio ujangili.**

**USHUHUDA**

Kiondo anasema, kuna mtu aliyekuwa anajihususisha na ujangili, lakini akabadilika kwa kuwasaidia kuwapa taarifa muhimu za wanaojihusisha na uhalifu huo, baada ya kumpatia elimu na kufanyia kazi huo mtandao, ili tatizo limalizike.

"Kuna wakati tulishirikiana na wahifadhi wenzetu wa Pori la Akiba la Selous, kutoa elimu ya uhifadhi kwa vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi, ambako watu waliokuwa wanajishughulisha na vitendo vya ujangili, walibadilika kupitia elimu hiyo na kutoa ushirikiano katika shughuli ya kukabiliana na ujangili.

"Walipita katika vijiji kutoa elimu na kutangaza mtu ambaye anafanya ujangili wa aina yoyote, wajisalimishe ili wapatiwe elimu na kuwa hawatachukuliwa hatua, kama watajisalimisha. Mwitikio ulikuwa mkubwa na jamii inaendelea kuwa na mwitikio chanya," anasema.

"Tuliamua kutumia busara zaidi katika hili, tunasema mtandao wao ambao wahusika walisaidia kututajia na wengine wanaojishughulisha na ujangili. Njia hii imetusaidia kupunguza ujangili," anasema.

Aidha, anasema kutokana na jitihada zilizofanywa katika kudhibiti ujangili, tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa Kiondo, kupungua ujangili wanaupima kwa mengi, ikiwamo ongezeko la matukio ya wanyama waharibifu na hatari, pamoja na kupungua kukamatwa kwa watuhumiwa wa ujangili.

"Sisi tunapima kwa ongezeko la wanyama, halafu tunapima tena kwenye matukio ya wanyama, kwa mfano kipindi cha nyuma ujangili ulikuwa umezidi, wanyama wengi walikuwa wametoweka, lakini sasa hivi wanaonekana kwa wingi na katika makundi makubwa."

Kiondo anasema, hivi sasa ujangili umepungua na serikali imekuwa makini kutatua changamoto ya ujangili, kwa kushughulikia mtandao wa wafanyabiashara wakubwa wa nyara za serikali, hivyo utaona kuna viashiria vya ongezeko la wanyamapori.

Anasema, kipindi cha nyuma watu walikuwa hawatoi taarifa za wanyama, mfano hai tembo au viboko wanaoingia katika maeneo na wapo wanaofanya ujangili huko waliko.

"Kwa sasa hivi tembo wakiingia katika mashamba ya watu, wanatupatia taarifa na kwenda kutoa msaada. Hii inaonyesha biashara ya ujangili hasa kwa tembo imepungua sana."

**CHANGAMOTO MASHAMBANI**

"Pia, katika matukio ya mashamba na wanyama, yameongezeka na wanaonekana katika makazi ya watu," anaeleza Kiondo.

Anasema, changamoto iliyopo ni matukio ya wanyama hatari kuuawa na mali zao kuharibiwa na wanyamapori, yakiwamo mashamba.

"Wiki iliyopita, kuna mtu kauawa na mamba na mwingine kajeruhiwa na kiboko. Yapo

MAZINGIRA

# Kukomesha ujangili kumenusuru mazingira ndani ya hifadhi Rufiji

matukio mengine yametokea katika kipindi cha nyuma," anasema.

Kiondo anataja lingine ni wananchi kutoelewa kuhusu uhifadhi na hawatoi ushirikiano, wakiwaona wanyama hawana faida kwao, wakiwaacha kwa mtazamo ni mali ya serikali pekee.

Aidha, anasema kwa sasa wanafanya kazi kwa kutumia intelijensia na taarifa za simu, pia kuna Askari wa Wanyamapori wa Vijiji (VGS), wanafanya nao kazi kudhibiti ujangili na kukabili wanyama waharibifu na hatari kwa maisha ya wanadamu ndani ya vijiji mbalimbali.

Anarejea, huko nyuma kulikuwapo matukio na wananchi waliokuwa wasiri kutetea ujangili na unapofika, ambao hawakuwa tayari kutoa taarifa yoyote.

Kiondo anasema, kuna mashirika yaliyosaidia kutoa elimu ya uhifadhi na kuna fedha asilimia 25 ya uwindaji wa kitalii, zinazotolewa na Pori la Akiba la Selous kwa halmashauri, ili ziende katika vijiji kusaidia miradi ya maendeleo.

Anasema Selous na mashirika mbalimbali zimejaribu kuwawezesha wananchi kujua umuhimu wa rasilimali za wanyamapori.

Anasema, kwa sasa pori la Selous linasaidia katika uhifadhi na limekuwa likitoa elimu kwa jamii na vijiji vyote vinavyoizunguka hifadhi hiyo na kila mwaka, kuna fedha zinazotolewa kwa vijiji hivyo wilayani Rufiji.

"Zamani unaweza kukuta mnyama kauliwa au kujeruhiwa, lakini jamii kwa sasa ina mwamko katika kutoa ushirikiano katika masuala ya hifadhi.

"Tunaamini kadri siku zinavyokwenda na elimu inayotolewa itasaidia kutoa ushirikiano wa kutosha, ili kufikia malengo ya serikali kupambana na ujangili," anasema.

Kondo anasema, katika nafasi yao ya uhifadhi wanaendelea na ujirani mwema na jamii, kwa sababu rasilimali hizo zinahusu pia kizazi kijacho, nao waje wazikute salama.




> Ninamshukuru Rais Magufuli, kwa kuwa jambo hili ni zuri na hata sisi wahifadhi inakuwa ni rahisi wananchi kutuelewa, hasa lengo la serikali ni nini.



Mhifadhi wa wanyamapori wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, Robert Kiondo.



Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mloka, Ahmed Mloya.

### MALIPO KIFUTA MACHOZI

Kiondo anasema, serikali inalipa kifuta jasho au machozi kwa waathiriwa wa matukio ya wanyamapori, ambayo jumla ya watu 15 waliojeruhiliwa na wengine kuuawa na wanyamapori katika Halmashauri ya Wilaya Rufiji, walilipwa shilingi milioni 11.6. Ni fidia hiyo ya matukio yaliyotokea kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka jana.

"Sio kwamba inaondoa lile tatizo, lakini angalau inasaidia kufuta machozi. Hivyo wiki mbili zilizopita, serikali ya Rais John Magufuli, imewawezesha kutoa kifuta machozi kwa ndugu wa mtu aliyeuawa na mnyama," anasema Kiondo.

"Ndugu amepewa shilingi milioni moja na yule aliyejeruhiwa amepatiwa shilingi 200,000 kama kifuta machozi (ubani)," anadokeza mchanganuo unaowafikia waathirika, kila mmoja, akisema lengo ni kuwahamasisha wananchi watambue uthamini wa serikalini yao.

"Ninamshukuru Rais Magufuli, kwa kuwa jambo hili ni zuri na hata sisi wahifadhi inakuwa ni rahisi wananchi kutuelewa, hasa lengo la serikali ni nini.

"Maana kama huwapi kifuta machozi, wanaona wanyama ndio wanaopendwa kuliko watu, kumbe serikali inajali wananchi wake pamoja na wanyamapori," anafafanua.

Anasema, kuanzia mwaka 2005 hadi 2008, zaidi ya watu 48 walidhuriwa na wanyamapori, yakiwamo matukio ya vifo wilayani Rufiji.

"Wilaya inafanya jitihada mbalimbali kudhibiti matukio haya kwa kutoa elimu kwa wananchi, pamoja na kudhibiti matukio ya wanyama wakali kabla yakuleta madhara," anasema.

Kiondo anafafanua, ili mwananchi apatiwe kifuta machozi, taarifa zinapaswa kutolewe kupitia watendaji wa vijiji husika na baadaye kupelekwa wilayani, ambako fomu maalumu ya kifuta machozi inajazwa na kuwasilishwa wizarani kwa hatua zaidi.

Anasema, wananchi wanapaswa kutoa taarifa kwa wakati, pindi wanapopatwa matukio hayo, kwa kushirikiana na watendaji wa vijiji, ili wapate vifuta jasho hivyo mapema.

Kiondo anasema wapo ambao hukutana na madhara, ikiwamo kushambuliwa na wanyama wakali kama simba, tembo na chui, huku wananchi wengine wakiweka hisia tofauti dhidi ya wahifadhi.

"Wapo ambao huingia kwenye maeneo ya hifadhi kama mnavyoelewa, baadhi ya wanyamapori ni wakali. Kwa mfano chui wanaweza kujificha usijue. Sasa unavyopita wakakushambulia hadi kupoteza maisha," anasema.

Pia, anashauri: "Ni vizuri wana nchi wakazingatia sheria kwenye maeneo ya hifadhi kwa kutoingia ovyo kwenye hifadhi za wanyamapori."

Malalamiko ya tembo

Kwa upande wake, Asia Selemani, mkazi wa kijiji cha Mloka, katika Tarafa ya Mkongo wilayani Rufiji, anasema wamekuwa wakisumbuliwa na tembo wanaoharibu mazao yao.

Anasema, kwa sasa tembo ni wengi na wanapokuwa wanavamia mazao yao, wanashindwa kuwafukuza kwa sababu hawana uelewa na wanaogopa kuhatarisha usalama wa uhai wao.

"Tungepatiwa askari wa wanyamapori hapa kijijini, ili watusaidie katika kuwaondoa hao tembo wanapovamia mazao yetu.

"Kwa mfano lenye mpunga hatoki huwa tunajaribu kuwafukuza hawataki kuondoka, hivyo tungepatiwa hao wataalamu wangetusaidia," anasema Selemani.

### MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mloka, Ahmed Mloya, anasema kijiji hicho kipo jirani na Pori la Akiba la Selous na kwa sasa imekuwa changamoto kwao wanyama kuingia shambani, wakiwamo tembo.

Mwenyekiti huyo anasema, ni hali inayotokana na ongezeko la wanyama hifadhini na chanzo kikubwa ni matokeo ya jitihada za serikali kupambana na ujangili.

Mloya anasema, wananchi waliodaiwa kuhusika na ujangili, sasa wameacha na kuwasilisha silaha zao serikalini, hivyo sasa wanaelewa umuhimu wa kuhifadhi wanyamapori.

"Kijiji chetu kilipatiwa ufadhili wa kusomesha vijana skauti. Hawa wanatusaidia katika kupambana na ujangili na wanapoona kuna jambo ambalo sio zuri, wanatupatia taarifa na kulifanyia kazi," anasema.

"Kutunza mazingiza na kuhifadhi hii ni ajenda ambayo tunaifanya katika mikutano yetu kama unavyoona, Mloka pasipo utalii, basi hakuna Mloka. Hatuna kiwanda wala ardhi nzuri ya kilimo. Huwa tunalima kwa ajili ya kupata chakula," anasema.

Mloya anausifu umeleta maendeleo makubwa na ndio maana wameamua kukabiliana na ujangili, akianisha mbinu zao: "Wale ambao walikuwa wanamiliki silaha kinyume cha utaratibu, tumewajulisha mamlaka husika na kuja kuzichukua."

AFYA

# Ajali ilivyompokonya mguu mmoja, ndoto ya uanariadha haikumponyoka

• Miaka minne chozi la baba halijakauka

**Na Romana Mallya**

"MGUU wangu ulikatwa, baada ya kupata ajali ya gari huko Yombo Vituka, jijini Dar es Salaam. Licha ya kukatwa mguu huo haujaondoa ndoto yangu ya kuwa mwanariadha," ni sauti inayotoka kwa Abdul Hamad (10), akianika msimamo na hisia alizo nazo sasa.

Hiyo ndiyo simulizi ya awali, akiitikia swali kutoka gazeti la Nipashe, kutaka kujua alikosimama na ndoto yake anakoelekea, hivi sasa akiwa mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Mkombozi, iliyopo Yombo Vituka, jijini Dar es Salaam.

Akiendelea na simulizi kilichomfikisha hatua ya kupoteza mguu wake, anasema: "Nilipata ajali mwaka 2015, nakumbuka nilikuwa nimepakiwa kwenye baiskeli. Nilikuwa na rafiki yangu ambaye wakati huo alikuwa akiiendesha, tukiwa barabarani, ghafla gari lilitokea huko na kutufuata tulikokuwa na kutugonga.

"Nilisimuliwa kuwa baada ya kugongwa nilirushwa kwenye nguzo. Naweza kusema hapo ndipo maisha yangu yalipobadilika, badala ya kutembelea na miguu miwili ambayo Mungu alinipa.

"Nilinyanyuliwa eneo la ajali mguu mmoja ukiwa unaning'inia 'umesagwasagwa' umebaki ngozi tu ikiushikilia," anasimulia Abdul.

Mwanafunzi huyo anaeleza kuwa baada ya ajali hiyo alipelekwa katika Hospitali ya Temeke na baadaye Hospitali ya Taifa Muhimbili. Huko nako alihamishiwa katika Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (Moi), walipoamua kumkata mguu kutokana kushindikana kuungwa.

Abdul anasimulia kuwa, kabla na baada ya ajali alikuwa na ndoto ya kuwa mwanariadha. Abdul anaendeleza simulizi kwa tabasamu, akisema: "Napenda kukimbia napenda sana kuwa mwanariadha. Napenda kutambulika kitaifa, napenda kupeperusha bendera ya Tanzania kimataifa. Hii ndiyo ndoto yangu, naamini siku moja itatimia."

"Kila mtoto anapozaliwa anapokuwa kwenye safari ya ukuaji huwa na ndoto yake. Mimi napenda sana kuwa mwanariadhara na mara kwa mara huwa namwambia baba yangu," anasimulia Abdul, huku akinyoosha kidole kumwelekeza baba yake, Mzee Kipango.

"Ninaamini ndoto yangu itatimia, haijalishi nina mguu wa bandia au la. Kwanza, nikijifananisha nilivyokuwa awali baada ya kuwekewa mguu wa kwanza wa bandia na huu wa pili, najiona nipo tofauti.

"Mguu huu wa sasa niliyowekewa mwaka jana, najiona kama mtu wa kawaida. Nimeuzoea, naweza kucheza mpira na watoto wenzangu na kukimbia pia."



Abdul Hamad, akiwa na wadogo zake



amad Kipango, baba wa Abdul, akiwa kazini kwake. **PICHA ZOTE: ROMANA MALLYA**

### MGUU BANDIA

Abdul anasema baada ya kukatwa mguu mwaka 2016, aliwekewa mguu wa kwanza na MOI, anakiri katika siku za kwanza haukuzoea na ulikuwa ukimtesa.

"Niliwekewa mguu wa bandia ili uniwezeshe kutembea kama ilivyokuwa awali, lakini kwa sababu ulikuwa ni mgeni mwilini, nilipata nao tabu, hata baba nilikuwa nikimwambia," anasema.

Anasimulia kuwa mwaka jana kupitia Hospitali ya CCBRT, jijini Dar es Salaam, alipata mguu bandia mwingine, anaoamini umerejesha kwa kiwango fulani ndoto yake ya kuwa mwanariadha.

"Huu mguu bandia niliowekewa mwaka jana umenifanya niwe sawa. Naweza kupiga mpira kwa kutumia mguu huu mzima na huu wa bandia nikatumia kupata nguvu ya kusimama. Najiona nipo sawa sasa, ingawa siyo sawa kama nilivyokuwa na miguu yote miwili," anasema.

Ni mazungumzo ya Nipashe na Abdul, katika Hospitali ya CCBRT, ambako alikuwa miongoni mwa waalikwa, walioshiriki kwenye uzinduzi wa jengo la kliniki ya huduma binafsi iliyoanzishwa hospitalini hapo.

> **Alikuwa akilalamika mara kwa mara kuwa anaumia, lakini kadiri siku zilivyokuwa zinasonga, aliuzoea, ingawa haikuwa rahisi kama tunavyofikiria.**

### ANAYEMVUTIA

Abdul anamtaja kivutio kikuu chake ni mwanariadha mlemavu wa miguu yote miwili wa Afrika Kusini, Oscar Pistorius, ambaye anaamini, siku moja atafikia mafanikio ya kiwango chake.

Kwa kifupi, Pistorius ni mlemavu wa miguu yote miwili ambaye mwaka 2012 alinyakua medali ya dhahabu katika mbio za mita 400 na kuweka historia katika michezo ya Olimpiki iliyofanyika jijini London, Uingereza.

Wakati huo Pistorius alikuwa na umri wa miaka 25, alipotetea taji la mbio za mita 400 zijulikanazo kama 'T44' zilizokuwa maalum kwa watu walemavu wa ama miguu yote au mmoja. Alikuwa mkimbiaji pekee katika mbio hizo, aliyetumia muda chini ya sekunde 50.

Abdul anaeleza imani yake kuwa ni kitu ambacho kipo ndani ya hisia zake na kila mara amekuwa akikifanyia mazoezi dhamira hiyo, akifafanua: "Kama nilivyokuambia, napenda riadha. Huu mpira unaouona huwa pia nacheza mtaani, mpira wa miguu na watoto wenzangu."



Abdul Hamad akifurahia michezo.

### BABA YAKE?

Baba wa mtoto huyo, Hamad Kipango, anasimulia siku na namna taarifa za mkasa wa mwanawe ulipotokea, kwamba alikuwa eneo la Vingunguti, Dar es Salaan, akiendelea na shughuli za ujasiriamali wa kuuza mihogo.

"Nakumbuka ilikuwa ni Julai 19, mwaka 2015, majira ya saa nne asubuhi, ilikuwa sikukuu. Nilipigiwa simu kutoka nyumbani, nikifahamishwa kuwa Abdul amepata ajali akiwa kwenye baiskeli," anasema.

"Nilishtuka sana, nikaambiwa wakati huo ameshapelekwa Hospitali ya Temeke. Nakumbuka nilichukua usafiri wa pikipiki, nilipofika nilijikuta natokwa machozi baada ya kumuona Abdul mguu wake wa kushoto ni kama umekatika, imebaki ngozi tu inaning'inia."

Kipango ambaye yeye na mke wake wanajishughulisha na uuzaji mihogo, anasema baada ya taratibu zote katika Hospitali ya Temeke walihamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, ambako walipokelewa kitengo cha dharura.

"Alipofika kitengo cha dharura Muhimbili walitushauri afanyiwe kipimo cha 'CT Scan' kuangalia kama ameumia eneo la kichwani kwa sababu wakati huo alikuwa akitoka damu mdomoni na sikioni. Tunamshukuru Mungu majibu yalionyesha hakupata tatizo kichwani," anasimulia.

"Baada ya majibu hayo ndipo tulipohamishiwa Taasisi ya Mifupa MOI na ilipofika saa moja usiku majibu ya mguu yalitoka, daktari aliniambia kuwa hawawawezi kuunga watakachokifanya ni kuukata.

"Haikuwa rahisi kupokea jambo hilo," anasema Kipango, huku kumbukumbu ya simulizi hiyo ikimtoa machozi. Anaendelea: "Kiukweli baada ya kuelezwa hivyo nililia sana hadi leo hii kila nikimwangalia mwanangu huwa natokwa na machozi.

"Nakumbuka ilikuwa saa nne usiku nikaambiwa Abdul anaingia chumba cha upasuaji na baada ya muda akatolewa. Ulikuwa mtihani kwangu. Ni mtihani wa maisha ambao sijawahi kuusahau hasa kila nikimwangalia mwanangu Abdul. Siamini kilichotokea," Kipango anatamka huku akirejea hisia ya kilio.

Anasema, katika kipindi hicho chote, alitumia muda wote akiwa hospitalini, kwa sababu wakati Abdul anapata ajali mke wake (mama Abdul) alikuwa na siku ya tatu tangu ajifungue.

### MAISHA MAPYA

Kipango anasimulia kuwa baada ya kukatwa na kupitia kipindi cha mateso na maumivu makali ya jeraha, hatimaye mwanawe alianza safari mpya ya kutumia mguu bandia aliopatiwa na taasisi ya MOI mwaka 2016.

"Alikuwa akilalamika mara kwa mara kuwa anaumia, lakini kadiri siku zilivyokuwa zinasonga, aliuzoea, ingawa haikuwa rahisi kama tunavyofikiria," anasema.

Anasema mwaka jana, Hospitali ya CCBRT ilimpatia mguu mwingine ambao akiulinganisha na awali, sasa una sura ya matumaini zaidi.

"Mwanangu mbali ya ndoto yake ya kuwa mwanariadha, anapenda sana mpira kama unavyomuona na mpira wake. Hata akiwa nyumbani hupenda kucheza mpira, kupiga danadana hayo ndiyo maisha yake.

"Pia, kukimbia ndiyo ndoto aliyokuwa nayo tangu awali na hajaibadilisha anapenda kuitimiza," anasimulia Kipango.

Kipango anasema, kiwango cha ufaulu wa mwanawe umeshuka shuleni, mara baada ya ajali hiyo, akifafanua: "Kabla ya ajali alikuwa akifanya vizuri kwenye masomo yake.

"Kipindi anapata ajali alikuwa darasa la pili, lakini baada ya ajali, ufaulu wake umeshuka sana. Ile ajali ilimwathiri kwa kiwango kikubwa, ufaulu wake siyo mzuri sana."

### MAONI YA BABA

Kipango anasema umasikini kwenye familia nyingi, umechangia ndoto za vijana hao kutotimia. Anaendelea: "Kama unavyojua familia zetu ni za kimaskini, Muda mwingi huwa tunatumia kutafuta riziki na kurudi nyumbani."

"Mara nyingi unakuta watoto wameshalala au mwenyewe unakuwa umechoka hata muda wa kukaa na watoto unakosa," anasema.

Anaendelea: "Binafsi sina ajira, najitafutia. Kwa hiyo wakati mwingine nakosa hata muda wa kukaa na watoto, ila ninapoupata ingawa ni 'mchache' tunaelekezana mawili matatu.

> **Mara kwa mara Abdul huniambia kuwa anapenda kuwa mwanariadha. Namuombea kwa Mungu ndoto yake itimie, ndicho nachoweza kusema kwa sasa.**

"Mara kwa mara Abdul huniambia kuwa anapenda kuwa mwanariadha. Namuombea kwa Mungu ndoto yake itimie, ndicho nachoweza kusema kwa sasa."

Pia, mzazi huyo wa Abdul, anaiomba serikali iendelee kuwasaidia walemavu na wapatia vifaa bandia kila inapowezekana ndivyo matumaini mapya kwao yanapoonekana. Ushauri wake ni kwamba, vifaa hivyo ni vyema viondolewe kodi ili visiuzwe kwa bei kubwa.

"Mguu huu wa bandia aliouvaa Abdul nimeambia unauzwa sio chini ya milioni sita. Abdul ameupata kwa msaada wa CCBRT. Ukweli ni kwamba ingehitajika niununue. Sidhani kama ningeweza.

"Naishukuru CCBRT, kwa sababu nikimwangalia mtoto wangu kwa sasa, licha ya kwamba amewekewa mguu wa bandia, lakini unamsaidia kutembea kama watu mwenye miguu miwili. Mungu awabariki sana," anahitimisha.

***• Mzazi wa Abdul Kipango, anapatikana kwa simu: (+255) 0787 432696***



Wawindaji wakiwa na chatu waliyemuua. **PICHA: MTANDAO.**

## Teknolojia yawezesha kunasa chatu mkubwa 'kupitiliza'

HIFADHI ya Taifa ya Big Cypress iliyoko Florida, Marekani, imemnasa chatu mkubwa mwenye urefu wa mita 5.2, kwa kutumia teknolojia mpya ya kuwanasa viumbe wavamizi.

Nyoka huyo ndiye mkubwa zaidi kuwahi kunaswa kwenye hifadhi hiyo na alikuwa na uzito wa kilo 63.5, pia akiwa na 'mimba' ya mayai 73.

Chatu hao wanaelezwa kuwa wavamizi kwenye eneo hilo, wanatishia kwa kiasi kikubwa maisha ya viumbe wa asili wa Jimbo la Florida.

Watafiti katika hifadhi hiyo, waliwategeshea vifaa maalum madume ya chatu, ili kuwatafuta majike yanayopandwa na kukaribia kutaga.

"Timu ya watafiti ilimfuatilia dume moja lililofungwa kifaa hicho na kumnasa jike huyo karibu yake," imeeleza taarifa ya hifadhi hiyo kupitia mtandao wa habari.

Pamoja na kuondoa nyoka wavamizi, hifadhi hiyo inatumia matokeo ya tafiti zake kujifunza tabia za nyoka na kutengeneza njia mpya za kukabiliana nao.

Chatu wanachukuliwa kuwa viumbe wavamizi jimboni Florida, tangu walipoonekana kwa mara ya kwanza katika viunga vya Everglades, katika miaka ya 1980.

Aina hiyo ya nyoka ina asili ya Bara la Asia, lakini baadhi ya chatu katika jimbo hilo, wanaaminika kuachiwa kutoka kwenye umiliki wa watu waliokuwa wanawafuga.

Chatu wengi katika jimbo hilo, walitoroka kwenye vituo vya utafiti na uzalishaji, baada ya kutokea kimbunga kiitwacho Andrew, mwaka 1992.

Jimboni Florida, hakuna wanyama wa asili mwituni wanaowinda chatu na kwa maana hiyo, inaondoa uwezekano wa kupunguza idadi yao, hali inayofanya katika sura ya pili kutajwa inachangia kupotea kwa wanyama wengi. **BBC**

AFYA

SIKU YA AFYA DUNIANI

# WHO: Wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume

• Tofauti imejikita katika mtindo wa maisha



Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus.

**Na Veronica Romwald**

UTAFITI unaeleza kuna pengo la miaka 18 katika kipindi cha maisha ya watu kati ya nchi masikini na tajiri, huku majumuisho ya kijinsia yakionyesha wanawake wanaishi umri mrefu kuliko wanaume, hasa katika nchi zilizoendelea.

Ripoti hiyo imetolewa Aprili 4 mwaka huu na Shirika la Afya Duniani (WHO), ikiwa wiki ya maadhimisho ya Siku ya Afya Duniani, ambayo hufanyika April 7, kila mwaka.

Kaulimbiu ya mwaka huu, inasisitiza afya kwa wote, suala linalotiliwa mkazo sasa na shirika hilo, ili kufikia lengo namba tatu, kati ya malengo 17 katika orodha ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs).

Huenda ripoti hiyo ikapokelewa kwa furaha na wanawake kuliko wanaume. Hata hivyo, bado dunia na hasa nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo zina kazi kubwa ya kufanya.

Hiyo ni katika kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza na ajali za barabarani, ambazo kasi zake zinaonekana kuongezeka na kuchangia idadi kubwa ya vifo duniani.

> **Kati ya (wagonjwa) 150 hadi 200 walikuwa wanajijua, lakini walikuwa hawatumii dawa vile inavyopaswa na hivyo kuhatarisha maisha yao zaidi.**

**HALI HALISI**

Ripoti ya WHO, inabainisha kwamba magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanakadiriwa kusababisha vifo vya watu milioni 41 kila mwaka, sawa na asilimia 71 ya vifo vyote. Robo tatu ya vifo hivyo, yaani watu wapatao milioni 32 wanatoka katika nchi za uchumi wa kati na chini au kwa lugha nyingine, nchi masikini.

Shirika hilo linaeleza magonjwa yasiyoambukiza husababisha vifo vya awali ya kitaalamu 'premature death' na uzoefu unaonyesha hasa kutoka kundi la wenye umri wa kati ya miaka 30 hadi 69.

Pia, zaidi ya asilimia 85 ya vifo hivyo, vinatokea katika nchi zenye uchumi wa kati na chini.

Kupitia takwimu ya WHO, inakadiriwa maradhi ya moyo yanachangia vifo vya watu milioni 18; saratani vifo vya watu milioni tisa; kisukari vifo milioni 1.6; na magonjwa ya mfumo wa hewa, vifo milioni 3.9. Jumla yake, magonjwa hayo yanachangia asilimia 80 ya vifo vya mapema.

**ILIVYO NCHINI**

Akizungumza katika Mkutano wa Tatu wa Umoja wa Mataifa, uliofanyika mwaka jana, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anasema magonjwa yasiyo ya kuambukiza, yanachangia asilimia 34 ya vifo nchini kila mwaka.

Utafiti uliofanyika katika wilaya nne kati ya mwaka 1994 na 2002, unaonyesha asilimia 18 hadi 24 ya vifo vilivyokuwa vimetokea, vilitokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Pia utafiti wa viashiria vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza uliofanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) mwaka 2012, ulionyesha ongezeko la viashiria vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Profesa Mohamed Janabi, anasema kwamba magonjwa ya moyo hivi sasa ni tishio duniani na anafafanua:

"Inakadiriwa husababisha vifo vya watu milioni 18 duniani. Hiyo ni sawa na asilimia 31 ya vifo vyote. Idadi hii ni mara tatu zaidi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa Ukimwi, ambao unakadiriwa kusababisha vifo milioni tano kila mwaka.

"Aidha, inakadiriwa asilimia 75 ya vifo vinavyotokana na magonjwa ya moyo hutokea barani Afrika na kwamba idadi kubwa ya vifo hutokea huko Latini Amerika na sehemu za Bara la Asia."

Anasema, tangu mwaka 2015 taasisi hiyo ilipoanza kazi rasmi kwa mujibu wa sheria, waliona wagonjwa wa nje 23,000; mwaka 2016 waliona wagonjwa wa nje 53,000; mwaka 2017 waliona wagonjwa zaidi ya 60,000; na 2018 waliona zaidi ya wagonjwa 76,365.

"Ndani ya kipindi hicho, tumeweza kuwafanyia upasuaji wagonjwa 3,330. Mgonjwa mwenye umri mdogo alikuwa na miaka minne na mwenye umri mkubwa alikuwa miaka 82.

"Ukijumuisha na wale ambao tumewahudumia, lakini hawakuhitaji upasuaji, tuliona wagonjwa zaidi ya 250,000 katika kipindi cha miaka mitatu," anasema Profesa Janabi.

Anaongeza: "Katika maadhimisho ya Siku ya Moyo Duniani yaliyofanyika Septemba 26, 2018, walifanya kambi ya uchunguzi afya ya moyo bila malipo.

"Walijitokeza watu 801 kupima afya, watu 400 kati yao walikutwa wana shinikizo la juu la damu, 200 kati yao walikuwa hawajijui," anasema Profesa Janabi na kuongeza:

"Kati ya (wagonjwa) 150 hadi 200 walikuwa wanajijua, lakini walikuwa hawatumii dawa vile inavyopaswa na hivyo kuhatarisha maisha yao zaidi," anasema.

**WANAUME HATARINI**

Ripoti hiyo mpya ya WHO inasisitiza kundi la wanaume ndilo lipo katika hatari zaidi ya vifo, kutokana na magonjwa yasiyo yakuambukiza na ajali za barabarani kuliko wanawake.

Inaelezwa, kati ya sababu 40 za vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyo ya kuambukiza, 33 huwagusa zaidi wanaume na kuwapunguzia umri wa kuishi, kuliko wanawake.

Ripoti inataja mwaka 2016, uwezekano wa mtu mwenye umri wa miaka 30 kupoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kabla ya umri wa miaka 70 ilikuwa asilimia 44, wanaume wakiwa kwenye hatari zaidi kuliko wanawake.

Inaelezwa, kiwango cha vifo vya kujiua (suicide) katika mwaka 2016 kwa wanaume kilikuwa juu kwa asilimia 75, idadi ya majeruhi na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani kwa wenye umri kuanzia miaka15 nayo ni mara mbili zaidi kwa wanaume kuliko wanawake.

Pia, ripoti hiyo inabainisha pia kiwango cha vifo vitokanavyo na kuuawa ni mara nne zaidi kwa wanaume kuliko wanawake.

**KWA NINI WANAUME?**

Ripoti hiyo inataja sababu mbalimbali zilizochangia kuwapo kwa tofauti hiyo, kati ya wanawake na wanaume. Baadhi ni za kibaiolojia, kurithi, mazingira na upatikanaji wa huduma za afya.

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Ummy

INAENDELEA UK.20

AFYA

## DARASA LA PROF. KAISI:

# Kazi, dawa, mavazi ya wanaume kizuizi cha mimba kilichojificha

Na Beatrice Moses

• Shida kubwa wanaume ni wabishi • Aainisha staili kibao kukabili shida • Alia alichokitoa Ulaya kimebaki sandukuni

***WIKI mbili zilizopita ilikuwa sehemu ya kwanza ya simulizi ya daktari huyo bingwa katika huduma za kinamama na uzazi na juhudi zake mbalimbali alizoleta kufungulia upatikanaji huduma hizo nchini na nafasi ya kipekee, wilayani Newala, miaka 47 iliyopita. Endelea na simulizi yake ya kitaalamu, inayofafanua ubingwa wake kuwezesha uzazi ulioshindikana.***

WANAUME wengi wanajiamini kuwa na uwezo wa kutungisha mimba. Ni hali inayowafanya kugoma kwenda kupimwa hospitali, pale wanaposhindwa au kuchelewa kutungisha mimba kwenye ndoa zao.

Ni dhana inayosadikika kuchochewa na mfumo dume wa baadhi ya jamii kuamini kwamba, mwanamke iwapo hashiki mimba basi ndiye mgumba.

Ni hali inayotajwa kushawishi baadhi ya wanawake kupoteza uaminifu kwenye ndoa, hivyo 'wanachepuka' kusaka mimba. Hatimaye hupata na kuzaa watoto, huku wakiendelea kuishi na wenzi wao.

Mwaka 2012, iliripotiwa asilimia 44 ya wanaokwenda katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupima vinasaba (DNA) kwa ajili ya kujua uhalali wa watoto kwa baba, wamethibitishiwa kuwa watoto si wa kwao.

Katika takwimu za mwaka 2012 kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ziliainisha kuwa kati ya wanaume 90 waliokwenda kupima DNA, 40 ambao ni sawa na asilimia 44, walibainika siyo baba halali wa watoto.

Inaelezwa kitaalamu, hilo linaepukwa iwapo jamii itaelimika na kutambua kuwa matatizo ya uzazi yanaweza kujitokeza kwa jinsia zote mbili.

### KUTOKA PROFESA KAISI

Daktari bingwa wa uzazi na magonjwa ya wanawake, Profesa Malise Kaisi, anasema, haungi mkono wanawake wanaoamua 'kuchepuka' ndoa zao kusaka mimba, badala yake anawataka watumie mbinu mbadala kuelimisha wanaume.

**KUMRADHI**
Alhamisi iliyopita, hatukuweza kutoa mwendelezo wa simulizi za mtaalamu, Profesa Melise Kaisi, kama tulivyoahidi katika jarida la siku 14 zilizopita, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wetu. Samahani kwa usumbufu. **Mhariri**




> **Hapo nikalazimika kutumia mbinu ya kumdanganya kuwa siyo majibu yake, kisha nikamsihi aje tena siku inayofuata.**

Mbadala huo anaufafanua kwamba ni kuwasukuma wanaume wajitokeze kwenda kuwaona wataalamu na kupimwa, ili kupata tiba husika.

Profesa Kaisi, ni mtaaluma aliyechangia kuzalisha madaktari wengi kupitia mafunzo vyuoni, pia ametibu katika sehemu tofauti.

Anabainisha kuwa matatizo ya uzazi yapo yanayowahusu wanaume pekee, pia yapo yanayowahusu kinamama, dhana inayoweka tofauti ya imani potofu ya baadhi ya jamii, kuona mwanamke ndiye tatizo la kutoshika mimba.

Tatizo la uzazi linatokea kwa mwanaume yeyote hata kama awali alishampa mimba mwanamke, pia kwa mwanamke naye inawezekana, aliwahi kupata ujauzito, lakini akakumbwa na ugumba kutokana na sababu mbalimbali.

Profesa Kaisi anapinga fikra za baadhi ya wanajamii kuamini kuwa, mwanamke ndiye mwenye matatizo ya uzazi kama hashiki mimba.

Msisitizo wake ni kwamba, mwanaume na mwenza wake wanapaswa kwenda kupimwa ili kupata msaada wa kitabibu kutoka kwa wataalamu.

### USHUHUDA

Daktari huyo ana simulizi ya ushuhuda kwamba, kulikuwapo na mwanaume mwenye tatizo, lakini baada ya kupimwa, mwanamke alionekana ndiye aliyekuwa sawa.

"Wakati huo mwanaume huyo alikuwa ameshanitambia kwamba yupo 'normal' (kawaida) kwani anaweza kujamiiana hata round (mizunguko) tatu.

"Nilipompima na kumpa majibu, alitaka kujiua mbele yangu. Hapo nikalazimika kutumia mbinu ya kumdanganya kuwa siyo majibu yake, kisha nikamsihi aje tena siku inayofuata," anasema.

Profesa Kaisi anaeleza kwamba alifanikiwa kuzungumza naye taratibu na kumwelewesha, kisha, akamwambia ukweli, ambao aliupokea na kupewa tiba. Baada ya muda wakafanikiwa kupata mtoto.

### SHIDA YA WANAUME

Profesa Kaisi anasema, tatizo la uzazi kwa wanaume linakuwa katika sura kwamba, licha ya wao kumudu kufanya tendo la ndoa, hawawezi kutungisha mimba kutokana na kiwango kidogo cha uzalishaji na utoaji wa mbegu za uzazi, zisizo na nguvu.

"Hapo ndipo wanaume kadhaa huchanganyikiwa kwa kujiona kuwa kwa sababu ana uwezo wa kujamiiana na kwenda 'mishindo' mitatu au zaidi, hivyo ana uwezo pia wa kutungisha mimba," anasema Profesa Kaisi.

Anafafanua kuwa ni matatizo yanayosababishwa na mambo mengi, ingawa wapo wanaume waliowahi kutungisha mimba, kisha akakumbwa na ugumba kutokana na mazingira ya kazi anazofanya, ajali na magonjwa.

Profesa Kaisi, anaeleza kuna matumizi ya baadhi ya dawa za kitabibu, iwe za hospitali au za asili, dawa za kulevya na ulevi kwa ujumla, zinaathiri uwezo wa utendaji wa kujamiiana na uzalishaji mbegu za kiume.

Anasema, eneo la kuzalisha hutakiwa kuwa na joto la wastani, hivyo kuna aina ya mavazi ambayo si salama kuvaliwa na mwanaume, kama vile nguo za kubana, hasa kwa wanaoishi maeneo ya joto, kufanya kazi za mapishi au mitambo inayotoa mvuke mkali.

Anasema madhara hayo yana tiba yake, ambazo hufanyika kupitia mbinu ya kuwasaidia wasioweza kupeana mimba katika hali ya kawaida.

### NJIA YA IVF

Daktari huyo bingwa anaitaja njia mojawapo kwa jina la kitaalamu IVF. Anasema, hiyo inasaidia utungishwaji mimba kwa njia ya kupandikiza mbegu za mwanaume ndani ya yai la mwanamke na kuwekwa kwenye tumbo la uzazi la mwanamke baada ya saa 40.

Profesa Kaisi anafafanua: "Kitu kilichonivutia mimi nilipokwenda Holland (Uholanzi) mwaka 1977 kufanya mambo ya ugumba. Nilitoka huko nikiwa nimejifunza upasuaji wa mirija.

"Kuna mwanamke mmoja aligombana na mume wake, kisha akashikwa na shinikizo la damu la juu, ikapanda na akakataa kulazwa. Mtoto akafia tumboni nikamfanyia upasuaji," anaeleza.

Anasema, alifanikiwa kuanza kufanya IVF kutokana na ushirikiano mzuri aliopata kutoka daktari wa Ujerumani, aliyemwezesha kupata dawa bure, licha ya kwamba zilikuwa gharama kubwa.

"Yaani 'kiboksi' kidogo shilingi milioni 25 na wote tuliowafanyia hatukuchukua fedha. Lakini, walipotangaza (radio ya kigeni) kwamba kwa mara ya kwanza Tanzania imezalisha mtoto wa kwanza kwa njia ya IVF, maneno mengi yalianza kusemwa.

INAENDELEA UK.20

AFYA

# WHO: Wanawake wanaishi zaidi kuliko wanaume

INATOKA UK.18

Mwalimu, anasema anaunga mkono maudhui ya ripoti hiyo, akitaja vigezo vya nchini ni wanaume wengi wanavuta sigara, wanywaji pombe na hata ulaji usiofaa.

"Hivi ni visababishi vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, wengi hujihusisha navyo kuliko wanawake. Hivyo, kujiweka kwenye hatari, ndiyo maana tunaweka msisitizo jamii kubadili mtindo wa maisha," anasema Waziri Ummy.

Uwezekano wa mtu mwenye umri wa miaka 30 kupoteza maisha kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kabla ya miaka 70 ilikuwa asilimia 44, 2016, wanaume wakiwa kwenye hatari zaidi kuliko wanawake.

**CHANGAMOTO**

Ripoti ya WHO inaainisha changamoto iliyopo kwa kundi la wanaume ni kwamba wengi hawatafuti mapema huduma za uchunguzi kama ilivyo kwa wanawake.

Inatolewa mfano katika nchi zinazokabiliwa na maambukizi ya Ukimwi kwa wingi, wanaume wengi wanabaki nyuma, hawajitokezi mapema kufanya uchunguzi kujua hali zao.

Wakati mwingine wanaelezwa wanachelewa kuanza matibabu kufahamu iwapo wana maambukizi ya Ukimwi na wanaishia kufariki mapema, vivyo hivyo, kwa upande wa magonjwa mengine kama vile kifua kikuu (TB).

**MKURUGENZI WHO**

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, amenukuliwa akisema, uchambuzi huo wa ripoti kulingana na kigezo cha jinsia, umri na hali ya kipato ni muhimu katika uhakikishaji kuwa hakuna anayebaki nyuma kufikia lengo 'Namba Tatu' la SDGs.

> **Moja ya malengo yetu WHO, ni kuona watu zaidi ya bilioni moja wote wanafikiwa na huduma za afya duniani ifikapo 2023.**

"Nyuma ya kila idadi katika Takwimu za Afya Duniani ni mtu, familia, jamii au taifa. Kazi yetu ni kutumia taarifa hizi, kufanya maamuzi ya msingi ya ushahidi ambayo inatufanya tuwe na ulimwengu wenye afya, salama, na ulio bora zaidi kwa kila mmoja wetu," amenukuliwa Dk. Tedros.

**WANAWAKE**

Inaelezwa katika nchi za kipato cha chini (masikini), pengo la uhai kati ya mwanamke na mwanaume si kubwa mno, kutokana na changamoto ya upatikanaji huduma za afya za uhakika.

Katika nchi hizo, inakadiriwa mwanamke mmoja kati ya 41 hufariki dunia kutokana na sababu za uzazi, ikilinganishwa na mwanamke mmoja kati ya 3,300 katika nchi zenye uchumi wa juu.

Aidha, zaidi ya asilimia 90 ya nchi hizo za chini zinakabiliwa na uhaba wa wataalamu wa afya. Hata hivyo, mtazamo kuhusu huduma za afya hutofautiana kati ya makundi hayo.

**CHA KUZINGATIA**

Katika kuadhimisha Siku ya Afya Duniani, chapisho hilo la WHO linasisitiza takwimu hizo zinaonyesha umuhimu wa kuboresha upatikanaji huduma za afya ya msingi duniani, kufikia lengo Namba Tatu la Dunia.

"Moja ya malengo yetu WHO, ni kuona watu zaidi ya bilioni moja wote wanafikiwa na huduma za afya duniani ifikapo 2023," amenukuliwa Dk. Tedros.

Anaongeza: "Hii inamaanisha kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, hasa katika ngazi ya jamii na kuhakikisha huduma hizo zinapatikana, zinafikiwa kwa gharama nafuu, na zinafaa kwa kila mtu, bila ya kujali jinsi zao."

Katika hilo, Waziri Ummy ana msisitizo: "Serikali kupitia wizara, inasimamia kwa dhati suala la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya jamii. Hivi sasa kuna ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya, zahanati na hospitali kote nchini."

**UCHUNGUZI**

Pia, ripoti inabainishwa kwamba kiwango cha kuishi duniani kiliongezeka tangu mwaka 2000 na kisha kiwango kikaongezeka tena, mwaka 2016 kilipanda kwa miaka 5.5, yaani kutoka miaka 66.5 hadi 72.

Hata hivyo, matarajio bado yanaelezwa kuathiriwa zaidi na hali ya kipato, katika nchi za uchumi wa chini ziko pungufu kwa tofauti ya miaka 18.1, kulinganisha na za kipato cha juu.

Inaelezwa, kuna wastani wa mtoto mmoja kati ya 14 wanaozaliwa katika nchi za kipato cha chini, hufariki dunia kabla ya kufikisha umri wa miaka mitano.

Inaelezwa kuwa ni mara ya kwanza WHO kutoa ripoti ya uchunguzi huo mpya, unaolinganisha jinsia, ambao umetoa ufahamu juu ya afya na mahitaji ya watu duniani kote, japo nchi nyingi nazo bado zinajitahidi kutoa taarifa tofauti za kijinsia.

"Tofauti hizi zilizobainika zitaharakisha ufumbuzi wa haraka kukabili pengo lililopo, kukusanya, kuchambua na kutumia mbinu bora zaidi, itasaidia kuboresha afya na ustawi wa watu, sera ya afya lazima ziendelezwe kwa takwimu thabiti za kuaminika, katika kila nchi," anajumuisha mwandishi mkuu wa ripoti hiyo, Dk. Richard Cibulskis.

# Kazi, dawa, mavazi ya wanaume kizuizi cha mimba

INATOKA UK.19

"Kupitia njia hiyo ya IVF kwa kushirikiana na daktari mwenzangu, tulifanikiwa kutungisha mimba 11, lakini miongoni mwao tatu tu ndiyo zilileta matokeo mazuri. Watoto wao hao sasa wana miaka 18.

"Nimewaambia wazazi wao wasiwaeleze watoto ambao mimi nawaona kama wajukuu zangu, wasiwaambie kama walizaliwa kwa njia ya IVF. Kwa sasa ni wakubwa wana umri wa miaka 18," anasmulia uzoefu wake.

Anasema kuna mama, aliyepata mimba iliyokuwa ya mapacha, lakini ilipofika miezi sita, watoto wakatoka lakini hawakuishi.

"Jambo la kushangaza ni kwamba, licha ya kuwa na uchungu wa kupoteza mwanawe, yule mama alisema lakini afadhali nimeonja ladha ya kubeba mimba," anaeleza.

Anasema walikwama kuendelea na upandikizaji huo, baada ya mtu aliyekuwa anatuma dawa kutoka nchini Ujerumani kupata ajali na kufariki dunia.

"Hivyo mashine za IVF zipo tu kwa muda mrefu sasa hazijatumika na zinauzwa kwa gharama kubwa, licha ya kujaribu kutaka kuwafundisha madaktari vijana, walivunjwa moyo kwa vitisho vya maneno," anasema.

**IVF&JAMII**

Anasema, awali ilionekana ni msaada kwa wanawake wanapohamishwa mirija, lakini kwa sasa inasaidia wanaume ambao kiwango cha mbegu kipo chini au anasema 'kinasoma ziro.'

"Tunachofanya kwa wanaume hao ni kuchukua mbegu moja tu au mbili, tunatumia njia inaitwa 'Intra Cytoplasmic Sperm Injection' au (ICSI) inazalisha, zinakuwa nyingi na zinawezeshwa kutunga mimba," anasema.

Anasema, hata hivyo kwenye IVF kuna changamoto inayomhitaji mtu wa kati, ambaye ni mtaalamu wa viumbe. Profesa Kaisi analifafanua hilo kuwa: "Wataalamu hao wanapatikana miongoni mwa madaktari wa wanyama.

"Wale wana uwezo wa kuangalia na kutambua yai na kukwambia kwa hili mtoto akizaliwa anaweza kuwa na mtindio wa ubongo. Hayo ni mambo ambayo hata mimi siyaelewi kabisa."

Kwa mujibu wa Profesa Kasi anayewataja wataalamu hao wa kati ni muhimu, amnakiri kuwa binafsi licha ya kwamba alifundisha katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), hawakuwahi kufikiria kuanzisha kozi ya kuzalisha wataalamu hao ambao anawaona kuwa ni muhimu kuwapo.

Anasema, katika jamii kuna wanawake ambao wana matatizo ya aina hiyo ya kutotoa mayai, hivyo inalazimika kupandikizwa ya mtu mwingine.

Hatua hiyo anaieleza, inawapa maswali ikiwamo kama inaweza kuleta changamoto kisheria na hasa wenye mayai kuamua kudai mwanawe iwapo utaratibu mzuri wa kukwepa mhusika kujua aliyewekewa mayai yake.

Anasema, kuwa njia nyingine ambayo siyo ya gharama kubwa, ingawa haitumiki sana nchini na haifahamiki, kwamba mbegu ya mwanaume hutumbukizwa moja kwa moja kwenye tumbo la mwanamke husika akiwa katika siku za kupevusha yai.

Anafanyaje kazi?

"Nilipofanikiwa kufanya upandikizaji nilishambuliwa sana, niliambiwa kuwa najifanya Mungu, lakini nilishangazwa na madai hayo kwa sababu pia nilikuwa nafanya upandikizaji wa mirija," anasema Profesa Kaisi.

Anasema licha ya kuwa daktari, kila anachotenda ndani ya kazi zake, humtanguliza Mungu, akimaanisha uwezo alio nao ni rehema zake.

"Biblia inasema Mungu atatupa maarifa. Kiapo cha udaktari kwamba nitamhudumia mgonjwa kwa kadri ya uwezo wangu wote ili kumsaidia," anasema.

Anaeleza kanuni yake ya kazi kwamba, muda wote ana kanuni kwamba kabla ya kufanya kazi ya upasuaji, amekuwa akisali kwanza, hatua ambayo anaamini kwamba inampa mafanikio.

"Hivyo, hao walionishambuliwa kwa sababu ya IVF, nimewaachа walivyo kwa kuwa wapo watu wamewekewa maini ya watu wengine waliokufa kwa ajali. Hivyo wanaishi na maini ya marehemu, je, madaktari waliowawekea wana makosa?" Anahitimisha kwa swali.

• **Alhamisi ijayo pata sehemu nyingine ya undani wa simulizi ya bingwa huyo wa tiba ya wanawake na uzazi.**



# Vijana wasomi watupiwa lawama masomo waliochagua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI kubwa ya vijana nchini waliohitimu vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi wameshindwa kupata ajira kutokana na kukosekana kusoma aina ya kozi zinazohitajika kwenye soko la ajira.

Mkurugenzi Mwakilishi wa Taasisi ya Vyuo Vikuu vya Nje ya nchi, Tony Kabetha, aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati wa mafunzo maalum kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na maofisa elimu katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wanaojengewa uwezo wa kuwashauri vijana masomo wanayostahili kusoma wanapojiunga na elimu ya juu.

Kabetha alisema kuwa vijana wengi waliohitimu elimu ya juu wapo mitaani bila ajira kutokana na kusoma masomo yasiyohitajika kwenye soko la ajira na wala tatizo sio ukosefu wa ajira.

"Tatizo sio ukosefu wa ajira kwa kuwa zipo na ni nyingi tu ndani na nje ya nchi, isipokuwa vijana wetu waliohitimu elimu ya juu hawakusoma masomo yanayohitajika kwenye soko la ajira na ndio sababu wapo mitaani bila ajira," alisema Kibetha.

Alisema kuwa tatizo la vijana hao lilianza tangu walipohitimu elimu ya msingi ambako hawakushauriwa vizuri masomo yenye mustakabali mzuri kwa ajira na badala yake waliachwa tu wasome masomo wanayoyapenda.

"Kuna vijana wamehitimu digrii ya 'Human Resource' (Rasilimali Watu) hawana ajira na wanatembea kutafuta ajira ya kuajiri watu wakati wao wenyewe hawana ajira! Hii inaonyesha kuwa wakati wakisoma hawakushauriwa ipasavyo wasome masomo gani yatakayowasaidia kuajiriwa kirahisi," alisema Kabetha.

Alisema kuwa ili kukabiliana na changamoto hiyo, Taasisi ya Uwakilishi wa Vyuo Vikuu vya Nje (UAR) imeamua kutoa elimu kwa walimu na wazazi ili wawashauri vizuri vijana kabla hawajaamua kusoma masomo ya elimu ya juu.

Alisema kuwa mpango huo utakwenda sambamba na kuwashauri vijana kuhusu vyuo vinavyofaa kusoma na kwa gharama nafuu, ili kuwaepusha na changamoto nyingine ya uwepo wa vyuo vikuu feki ndani na nje ya nchi.

Kabetha alisema kuwa sio vyuo vyote vinavyojitangaza kwenye mitandao ya kijamii ni vyuo halisi, bali kuna vyuo vingi feki vinajitangaza mitandaoni na endapo vijana watajiunga navyo kupitia mitandao hiyo, watajikuta wakijuta baadaye.

# Mfanyabiashara atinga kortini kuuza mbegu feki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Udhibiti wa Mbegu nchini (TOSCI), imemfikisha mahakamani mfanyabiashara wa pembejeo, Fortunatus Lutanikwa, mkazi wa Uyole jijini Mbeya, kwa tuhuma za kuwauzia wakulima mbegu feki na kughushi nembo ya taasisi hiyo na za kampuni zinazozalisha mbegu nchini.

Mfanyabiashara huyo alipandishwa kizimbani juzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya ambako alisomewa mashtaka matatu ya kuuza mbegu feki, kuuza pembejeo bila kuwa na leseni na kughushi nembo ya Tosci na kampuni zinazozalisha mbegu.

Akimsomea mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, Paul Ntumo, Wakili wa Serikali, Hannarose Kasambala, alisema mshtakiwa alikamatwa akiuza mbegu hizo feki kinyume cha Sheria ya Mbegu Namba 18 Kifungu cha 13(1) na Kifungu cha 26(1) na (2).

Kakili Kasambala alisema mshtakiwa alikamatwa na maofisa ukaguzi wa mbegu wa TOSCI Januari 29, mwaka huu, akiwa dukani kwake maeneo ya Uyole jijini Mbeya na kwamba siku hiyo alikutwa akiuza mbegu feki za aina mbalimbali, huku akiwa ameghushi nembo ya Tosci na kampuni za mbegu.

"Mshtakiwa alikutwa na aina tano za mbegu feki ambazo ni mahindi, karotio, alizeti, bamia na matango akiwa anawauzia wananchi dukani kwake maeneo ya Uyole," alisema Wakili Kasambala.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, Lutanikwa alikana kutenda makosa hayo akidai kuwa hajawahi kutenda makosa hayo aliyosomewa ndani ya mahakama hiyo. Baada ya mtuhumiwa kukana makosa hayo, Wakili wa Serikali Kasambala aliiambia Mahakama kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika na upande wa mashtaka upo tayari kwa kuanza kutoa ushahidi wake na akaiomba mahakama isikilize ushahidi huo.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Mbeya, Paul Ntumo, alikubali ombi la Wakili wa Serikali na akautaka upande wa mashtaka kuanza kuwasilisha ushahidi wake.

Mkaguzi wa Taasisi ya Tosci kutoka Makao Makuu Morogoro, Emmanuel Mwakatobe, alipanda kizimbani na kuanza kutoa ushahidi, ambapo alieleza kuwa walipata taarifa za siri kutoka kwa baadhi ya wananchi wakimlalamikia mfanyabiashara huyo kuwa anawauzia mbegu feki.

Akiongozwa na Wakili Kasambala, Mwakatobe walifika jijini Mbeya kufanya ukaguzi baada ya kupata malalamiko hayo na kwenda moja kwa moja katika duka la mfanyabiashara huyo wakiongozana na maofisa wa Jeshi la Polisi.

Mwakatobe aliieleza Mahakama kuwa baada ya kufika kwenye duka la mshtakiwa ambako walikamata gunia moja la mahindi yaliyopakwa rangi nyekundu yakiuzwa ndani ya duka hilo kama mbegu.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa soko jipya la Magomeni, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wadau waomba kulindwa vyanzo vya maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa Usimamizi wa Bonde la Ziwa Nyasa wameiomba serikali kuongeza udhibiti wa uharibifu wa mazingira na kuweka ulinzi wa kisheria wa vyanzo vya maji nchini, ili kuepusha taifa kukumbwa na tatizo la uhaba wa rasilimali za maji katika siku zijazo.

Wito huo ulitolewa na wadau hao kwenye uzinduzi wa Jukwaa la Wadau wa Bonde la Ziwa Nyasa ulifanyika jana mjini Tukuyu wilayani Rungwe.

Mmoja wa wadau hao, Salum Kilanga, alisema kutokana na hali halisi ya uharibifu wa mazingira na hasa vyanzo vya maji ilivyo nchini, ipo haja kwa serikali kubuni mbinu na kutafuta njia mbadala za kuhakikisha uharibifu wa mazingira unadhibitiwa.

Kilanga alipendekeza kuanzishwa kwa miradi mingi ya ufugaji nyuki kwenye vyanzo vya maji kama njia mojawapo ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na kuwaongezea wananchi kipato.

"Kasi ya uharibifu wa mazingira ni kubwa nchini, ipo haja kwa serikali kubuni mbinu za kuokoa mazingira hasa katika maeneo yenye vyanzo vya maji, mbinu mojawapo ni kuanzisha ufugaji nyuki kwenye maeneo hayo, ili kuongeza ulinzi wa maeneo hayo lakini pia miradi hiyo itawaongezea wananchi kipato," alisema Kilanga.

Ofisa Madini wa Mkoa wa Rukwa, Abraham Nkya, alisema kuwa sheria ya madini nchini inamruhusu Kamishna wa Madini kutoa leseni ya uchimbaji wa madini mahali popote ikiwamo kwenye vyanzo vya maji.

Nkya aliiomba serikali kutafuta namna ya kuzifanya idara zake kama vile idara ya madini na sekta ya maji kuwasiliana ili kuepusha leseni za uchimbaji wa madini kutolewa katika maeneo yenye vyanzo vya maji.

Aidha, Nkyas aliwashauri wakurugezi wa bodi za maji kuainisha maeneo yenye vyanzo vya maji, kuyapima na kuyamiliki na kisha kupeleka taarifa kwa Kamishna wa Madini ili asitoe leseni ya uchimbaji wa madini kwenye maeneo hayo.

Mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa Jukwaa hilo la Wadau wa Ziwa Nyasa alikuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Prof. Kitila Mkumbo ambaye alisema kuwa maji ndiyo rasilimali pekee inayopungua kwa kasi nchini ikilinganishwa na rasilimali nyingine.


Alisema kuwa taarifa za kitafiti zinaonyesha kuwa Tanzania inatarajiwa kuwa na idadi kubwa ya watu inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 300 ifikapo mwaka 2050, ambapo changamoto kubwa itakuwa ni maji ya kukidhi mahitaji ya watu hao.

"Wapo watu wanadhani Tanzania ina maji mengi na kwamba maji hayo yapo tu, si kweli hata kidogo na pengine maji ndiyo rasilimali haba kuliko zote na hali hii itajidhihirisha miaka michache ijayo kama hatua za kuilinda hazitachukuliwa," alisema Prof. Kitila.

Alisema kuwa taarifa hizo za kitafiti zinaonyesha kuwa ifikapo mwaka 2050, Tanzania itakuwa na changamoto kubwa mbili na kwamba changamoto ya kwanza ni uhaba wa maji na ya pili itakuwa ni elimu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi Ngwisa Mpembe, alisema Tanzania haijafikia kiwango cha kuwa na viwanda vinavyoathiri mazingira kiasi cha kusababisha uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji, isipokuwa adui mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji ni shughuli za kibinadamu zinazofanyika kwenye vyanzo hivyo.

Alisema kuwa endapo jamii itaelimishwa na kukatazwa kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji, hali ya upatikanaji wa maji nchini itaendelea kuwa nzuri kwa muda mrefu.





# Pinda ateuliwa mdhamini Chama cha Biblia

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAJUMBE wa mkutano mkuu wa Chama cha Biblia Tanzania wamempitisha kwa kauli moja jina la Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda kuwa mmoja wa wadhamini wa chama hicho.

Katika mkutano huo uliofanyika jijini hapa na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka mikoa yote nchini pamoja na ajenda zake ulipitisha jina la Pinda kuwa mdhamini.

"Wajume naomba kuwajulisha kuwa tulituma wenzetu kwenda kuonana na mheshimiwa Pinda kuhusu kumuomba awe mdhamini wetu, alipoonana nao alisema kama aliweza kufanya kazi katika serikali kwanini ashindwe kutumika kwenye kazi ya Mungu,"alisema Malekana.

Baada ya kauli hiyo wajumbe wa mkutano walilipuka kwa furaha na kulipitisha kwa kauli jina hilo kuuungana na wadhamini wengine kusaidia kuongoza chama hicho.

Malekana alisema chama hicho kina wadhamini watano na Pinda anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Askofu Valentino Mokiwa baada ya kumaliza muda wake.

Aliwataja wadhamini wengine wa chama hicho kuwa ni pamoja, Waziri Mkuu mstaafu Jaji Joseph Warioba, Mama Anna Mkapa, Askofu Gervas Nyaisonga na Askofu Sylvester Gamanywa.

Aliongeza kuwa majukumu ya wadhamini wa chama hicho ni kuhakikisha wanasimamia mali za chama hicho pamoja na kuhakikisha wanasaidia kulea chama hicho.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Alfred Kimonge alisema wanatarajia kujenga jengo la ghorofa tano eneo la Mji mpya jijini hapa ili kukuza uchumi na kupunguza utegemezi.

Alibainisha kuwa hatua za awali ikiwamo kuwasiliana na mamlaka za jiji na wataalamu wa michoro na usanifu majengo zimefanyika kabla ya kuendelea na mchakato wa ujenzi.

Aliwajulisha wajumbe kuwa hatua inayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi huo kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mikopo yenye masharti nafuu.

# Wakazi 518 walalamikia kuporwa viwanja bila fidia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI 518 wa Nzuguni B nje kidogo ya Jiji la Dodoma wameilalamikia Halmashauri kuchukua maeneo yao bila kuwapatia fidia wala viwanja mbadala kama walivyokubaliana.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wao na viongozi wa kata ya Nzuguni walisema kuwa mashamba yao yamechukuliwa na Jiji, lakini hakuna fidia iliyotolewa kulingana na ukubwa wa maeneo yao.

Peter Mguto, alisema kuwa alikuwa anamiliki shamba lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 2, lakini viongozi wa jiji wamempatia kiwanja kimoja ambacho pia anatakiwa kukilipia ndani ya siku 30.

Mguto alisema kuwa kutokana na ukubwa wa mashamba yao wanapaswa kukaa kwa pamoja na halmashauri ya jiji ili kukubaliana namna ambayo itakua na usawa kila upande.

"Kuna watu hapa wanamashamba ya hadi hekari 17 lakini leo hii jiji wanatoa kiwanja kimoja tu harafu eneo lote wanabaki nalo wao, hii siyo haki tunaomba serikali itusaidie katika hili"alisema Mguto.

Aidha, alisema kuwa wanaiomba halmashauri ya jiji kutumia mfumo ambao umekuwa ukitumika katika maeneo mbalimbali ambapo mmiliki wa shamba anapewa asilimia 70 na wao kuchukua asilimia 30 ya eneo lote.

"Kuna mtu anamiliki shamba lake lenye ukubwa wa hekari 17, lakini leo hii anapatiwa kiwanja kimoja tu na kuambiwa kuwa anatakiwa kukilipia ndani ya siku 30 bila kujua hawa watu ni maskini na pesa yenyewe ni zaidi ya Sh. 500,000, sasa mkulima ataipata wapi ndani ya muda huo," alihoji Mguto.

Alisema kutokana na mgogoro huo wa kudumu kutoka mwaka 2004, seriklai inatakiwa kuingilia kati ili wanachi wa kipato cha chini wasipokonywe haki yao ya kumiliki ardhi.

Naye Agatha Joseph, alisema kuwa pamoja na kuhakikiwa mashamba yao na kupewa karatasi ambazo zinaonyesha kuwa wao ndiyo wamiliki halali lakini mpaka hivi sasa bado hawajapatiwa viwanja hivyo.

Akijibu malalamiko hayo, Mwenyekiti wa Serikali ya mtaa Nzuguni B, Chares Mathias alisema pamoja na uhakiki kukamilika bado kumekuwa na kasoro ambazo zinasababisha sitofahamu hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo wao bado wataendelea kufutilia hadi ngazi za juu ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wanachi wao.

Diwani wa kata ya Nzunguni, Aloyce Luhega, alisema kuwa mpaka sasa vimekwisha gawiwa viwanja 255 na kuwatoa hofu waliobaki kuwa watapewa maeneo mangine katika Halmashauri ya jiji la Dodoma.




Meneja wa Benki ya NBC Kanda ya Kati, James Ndimbo (kulia), akikabidhi zawadi ya pikipiki kwa mkazi wa Dodoma, Twaha Saleh aliyojishindia katika kampeni ya Shika Ndinga inayodhaminiwa na benki hiyo, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma hivi karibuni.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajitoa shughuli za mashirika yasiyo ya serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema kuanzia sasa haitaingilia utendaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali na badala yake kazi hiyo itafanywa na bodi ya uratibu wa taasisi zisizokuwa za serikali.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu wakati akizindua bodi ya taasisi zisizokuwa za kiserikali jijini Dodoma.

Waziri Ummy alisema wanachotakiwa kwa sasa ni kufanya kazi kwa bidii kwa sababu serikali macho yao yako kwao.

Alisema bodi hiyo inapaswa kufanya kazi kwa uwazi ili kufanikisha maendeleo katika mashirika hayo.

Alisema kwa upande wa Serikali bodi hiyo ina mwakikishi ambaye atasaidia katika kukuza maadili ya kimsingi ikiwamo kutoa taarifa sahihi.

Alisema anaamini bodi hiyo inafanya kazi kubwa kutokana na kwamba imejidhatiti kwamba, lazima wainue na kukiendeleza kile walichokikuta katika bodi zilizotangulia.

Aidha, aliitaka bodi hiyo kuwa waadilifu kwa kufanya kazi kwa kutenda haki ili kila mmoja aridhike na maamuzi.


Aliwaagiza kujifunza utendaji wa kuratibu mashirika yasiyo ya kisetikali ili kufika mbali katika utendaji wao.

"Naomba mzingatie hayo kwa sababu Tanzania siyo kisiwa kiasi kwamba hatutakiwi kujifunza kutoka nchi nyingine," alisema Ummy. Alisema serikali ya awamu ya tano, inatambua mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali, kwa sababu wanafanya kazi kubwa vijijini.

Alisema anazikumbusha NGO kuacha kutumika kwa maslahi binafsi na badala yake zitatue matatizo.

Naye Katibu Mpya wa bodi hiyo Dk. Neema Mwanga alisema wanashukuru kuteuliwa kwao na wataitendea kazi nafasi waliyopewa.

Alisema watashirikiana na serikali kuhakikisha wanafika mbali katika maendeleo ya nchi.






Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kiwanda cha Kamal Steels, Ajah Jha (wa tatu kushoto), akifafanua jambo kwa Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Temeke, Amon Kakwale (wa pili kushoto), wakati wa hafla ya kukabidhi msaada wa nondo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za polisi za Kigamboni Kibada, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Msaidizi wa Kamanda huyo, ACP Awadhi Haji na baadhi ya watumishi wa kiwanda hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasisitiza kuimarisha miundombinu ya barabara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu iliyopo nchini ili kuimarisha huduma za maendeleo na kukuza sekta ya utalii.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa watembeza watalii uliofanyika mjini Zanzibar, Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Muhammed Ramia, alisema serikali inatambua kero za miundombinu iliyopo hususani ya barabara.

Alisema utatuzi wa matatizo hayo utasaidia kwa kiasi kikubwa kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi na watalii ambao wanatembelea Zanzibar.

Alisema sekta ya utalii imekuwa muhimu katika kukuza uchumi wa nchi na kwamba fedha zinazopatikana zitasaidia kuiweka Zanzibar katika mazingira ya kuvutia kwa wageni.

Balozi Ramia alitoa wito kwa watembeza watalii hao kufuata sheria za nchi pamoja na kuengeza bidii katika kuwahudumia wageni katika kutangaza vivutio vilivyopo ili kuimarisha upatikanaji wa mapato katika sekta hiyo. Aidha, Balozi Ramia pia aliwataka watembeza watalii hao kuendelea kushirikiana na taasisi zingine zikiwemo zinazokusanya mapato ili kudhibiti matumizi ya fedha. "Pia muwe na utaratibu wa kufanya mikutano mara kwa mara ili kujadili matatizo yanayowakabili,"alisema.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamadi Yussuf Masauni alisema serikali itahakikisha inaimarisha ulinzi na usalama kwa wageni wanaotembelea Zanzibar.

Alisema zaidi ya wafanyakazi 800 wameshamaliza mafunzo hivyo watasaidia kuondoa changamoto za uhaba wa wafanyakazi husussani katika vituo vya usafiri wa bandari na anga.

Naye mwenyekiti wa jumuia ya watembeza watalii Zanzibar, Hassan Ali Mzee, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili matatizo mbalimbali yanayowakabili ili yaweze kupatiwa ufumbuzi.

Alisema sekta ya utalii imekuwa tegemeo kubwaa katika kuimarisha uchumi wa nchi lakini bado watembeza watalii wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali hususan katika ulipaji wa kodi.

Aidha, mwenyekiti huyo alizitaka taasisi zinazosimamia masuala ya utalii kuwa tayari kujiunga na jumuiya hiyo ili waweze kunufaika na haki zao za msingi.

Akiwasilisha mada juu ya matatizo yanayoikabili sekta ya utalii Zanzibar mwanachama wa jumuiya hiyo, Ali Amour, alisema bado kuna baadhi ya matatizo ikiwemo miundombinu mibovu kwa baadhi ya barabara jambo linalosababisha wageni kupata shida wakati wakiwa safarini.

# Watoto wa kike watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Zanzibar, Tunu Juma Kondo, amewataka watoto wa kike kuchangamkia fursa za elimu ili kupata wasomi wanawake wenye sifa za kuwa viongozi wa kitaifa kikanda na kimataifa.

Alitoa kauli hiyo, katika ziara yake, Wilaya ya Kaskazini 'A' huko Gamba Mkoa wa Kaskanizi Unguja.

Alisema elimu ndiyo nyenzo pekee ya kuwakomboa kiuchumi na maendeleo wanawake nchini.

Alieleza kwamba kwa sasa watoto wa kike wanatakiwa kujengewa mazingira rafiki ya kupewa elimu bora itakayowasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Alisema wanawake wanaopewa fursa mbali mbali za uongozi, utendaji na utaalamu wa fani mbali mbali katika jamii wamekuwa mfano wa kuigwa katika utendaji na uchapakazi wao hivyo hicho ni kipimo sahihi cha uadilifu uliotukuka kwa kundi hilo.

Alisema kwamba matarajio ya UWT Zanzibar ni kuona wanawake wanajitokeza kwa wingi kushindana na wanaume katika kuwania nafasi mbali mbali za uongozi katika chaguzi mbali mbali za kisiasa ikiwamo uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema kila mwanamke anatakiwa kuchukua hatua ya kuwalinda na kuwasimamia watoto wa kie dhidi ya vitendo vya udhalilishwaji ili waweze kutimiza malengo yao bila kukatishwa na baadhi ya watu wanaokwamisha juhudi za kundi hilo kijamii.

Alieleza kwamba katika umoja huo atafanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo mahsusi ya jumuiya hiyo.

Alisema ni lazima viongozi na watendaji wa umoja huo wafanye kazi kwa bidii ili kutekeleza kwa vitendo maelekezo ya ibara ya tano ya katiba ya CCM ya mwaka 1977 toleo jipya la mwaka 2017, inayoeleza namna CCM inavyotakiwa kushinda kwa kishindo kwa uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na uchaguzi mkuu.

Aidha, aliwataka wanawake wa umoja huo kulipa ada kwa wakati ndani ya umoja huo ili kulinda haki zao za kuwa wanachama hai na wenye sifa za kuchagua na kuchaguliwa.

Kwa upande wa wanajumuiya hiyo wa Wilaya ya Kaskazini walisema kuwa wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaongeza wanachama wapya ili kuongeza jeshi la kufanikisha ushindi wa CCM katika uchaguzi mkuu ujao.

# Waziri aagiza mkandarasi kuchukuliwa hatua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kumchukulia hatua za kisheria mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo ya amali cha Makunduchi kutokana na kushindwa kutimiza masharti ya ujenzi wa kituo hicho.

Akizungumza wakati alipofanya ziara ya kushtukiza kuangalia maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wake, alisema ujenzi wa kituo hicho umekuwa wa kusuasua na wamekuwa wakiidanganya Serikali kutokana na ahadi wanazoweka.

Alisema haiwezekani ujenzi wa kituo hicho kuwa umeanza sambamba na kituo cha amali cha Daya kilichopo Pemba ambacho nacho kimepiga hatua kubwa katika kumalizika.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipoamua kujenga vituo hivyo katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba ilikuwa na lengo la kusogeza elimu ya amali (ufundi), karibu na wananchi ili kupata fursa za kujiendeleza na kujikwamua na umaskini.

Aidha, alisema wizara haipo tayari kuona juhudi hizo zinapotea kwa uzembe wa watu wachache ambao wanaweza kukosesha maendeleo hayo kwa jamii.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Idris Muslim Hija, alisema mkandarasi wa kituo hicho hajali kazi yake pamoja na zile za Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Kwa upande wake msimamizi wa ujenzi wa kituo hicho cha Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja Omar Hashim Mfangavu, alisema kuwa kuchelewa kwa kazi hiyo kunatokana na kuchelewa kwa baadhi ya vifaa ikiwamo mabati.

## Abdel Fattah al-Sisi kutawala hadi 2030

**CAIRO,** Misri

WABUNGE nchini Misri wameifanyia marekebisho Katiba ya nchi hiyo, ambapo imemruhusu Rais Abdel Fattah al-Sisi kuendelea kusalia madarakani hadi mwaka 2030.

Lakini wapinzani wake wamekosoa uamuzi huo wa bunge na kusema kuwa Misri inaingia katika utawala wa kidikteta. Mbali na mabadiliko hayo, wabunge wamempa Rais Al Sisi mamlaka makubwa ya kudhibiti idara ya Mahakama, lakini jeshi kuendelea kuwa na madaraka makubwa katika siasa za nchi hiyo ya Afrika ya Kaskazini.

Hata hivyo, mabadiliko hayo yanatarajiwa kupigiwa kura ya maoni na wananchi wa Misri, na tarehe ya zoezi hilo inatarajiwa kutangazwa muda wowote. Rais Al Sisi, ambaye alichaguliwa mwaka 2018, muhula wake wa miaka sita ulitarajiwa kumalizika mwaka 2024, lakini iwapo mabadiliko hayo yataungwa mkono, anaweza kuchaguliwa tena kwa muhula mwingine wa miaka sita.

Rais Al Sisi aliingia madarakani mwaka 2013, baada ya kuongoza mapinduzi ya kijeshi kumpindua Rais aliyekuwa amechaguliwa wakati huo Mohamed Morsi. **RFI**

## Mabilioni yakusanywa kukarabati kanisa lililoungua

**PARLIS,** Ufaransa

TAKRIBANI dola bilioni moja zimeshakusanywa kutoka kwa watu mbalimbali duniani, kwa lengo la kulifanyia ukarabati kanisa kuu la mjini Paris, Notre Dame lililoharibiwa kwa moto.

Wataalamu wa ujenzi wameshapeleka gari la kubebea vifaa vya ujenzi pamoja na mbao katika eneo la tukio. Maofisa wa zimamoto nao bado wanachunguza hasara iliyopatikana na kuona kama nguzo hazijaathirika kufuatia mnara wa kanisa kuporomoka na kuharibu paa.

Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa amezidisha shinikizo alipotangaza muda wa miaka mitano kukamilisha shughuli za kulikarabati kanisa hilo lililojengwa karne ya 12.

Rais Macron jana aliongoza kikao maalum cha Baraza la Mawaziri kuzungumzia ajali hiyo ya moto ambapo wataalamu wanaamini ni ajali iliyosababishwa na kazi za ukarabati.

Hakuna mtu yoyote aliyefariki wala kujeruhiwa kutokana na tukio hilo baada ya maofisa wa zimamoto kuwahamisha haraka waumini waliokuwa wakihudhuria misa. Watu wasiopungua 30 wameshahojiwa na polisi kuhusiana na tukio hilo.

Mjumbe maalum wa Rais Macron anayeshughulikia masuala ya kitamaduni, Stephane Bern, alieleza kuwa zaidi ya Euro milioni 880 (kiwango ambacho ni sawa na Dola milioni 995) zimeshakusanywa kwa siku mbili tangu tukio hilo la moto kutokea. **DW**

# Omar Bashir aswekwa jela baada ya kupinduliwa

**KHARTOUM,** Sudan

ALIYEKUWA Rais wa Sudan, Omar Al-Bashir, amepelekwa gerezani baada ya kukamatwa juzi usiku.

Bashir aling'olewa madarakani wiki iliyopita katika mapinduzi ya kijeshi jijini Khartoum baada ya kuiongoza nchi yake kwa miaka 30.

Taarifa zaidi kutoka vyanzo vya ndani ya familia ya Bashir vimethibitisha kuwa kiongozi huyo mwenye miaka 75 amekamatwa na kupelekwa jela.

Shirika la habari la kimataifa la Reuters lilieleza kuwa Bashir anashikiliwa kwenye gereza lenye ulinzi mkali la Kobar mjini Khartoum.

**Nchi ya Sudan kwa sasa ipo chini ya uongozi wa Baraza la Mpito la Kijeshi chini ya Luteni Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan.**

Kwa mujibu wa Reuters, Bashir anashikiliwa kwenye chumba cha peke yake gerezani na kuzungukwa na ulinzi mkali.

Kiongozi huyo alikuwa chini ya ulinzi mkali wa jeshi nyumbani kwake toka alipopinduliwa wiki iliyopita.

Nchi ya Sudan kwa sasa ipo chini ya uongozi wa Baraza la Mpito la Kijeshi chini ya Luteni Jenerali Abdel Fattah Abdelrahman Burhan.

Katika hotuba aliyoitoa siku ya Jumamosi, Jenerali Burhan aliapa kuung'oa utawala na kuahidi kuheshimu haki za binadamu, kusitisha marufuku ya kutotoka nje, kuwaachia huru wafungwa wa kisiasa, kuvunjilia mbali serikali zote za majimbo, kuwashtaki waliowaua waandamanaji na kukabiliana na rushwa.

Baraza hilo limewakamata baadhi ya waliokuwa maofisa wa serikali na kuahidi kutowatawanya waandamanaji.

Katika mkutano na waandishi habari siku ya Jumapili, msemaji wa baraza Meja Jenerali Shams Ad-din Shanto, alisema kwamba baraza la kijeshi lipo tayari kuidhinisha serikali yoyote ya kiraia itakayoidhinishwa na vyama vya upinzani.

Alieleza kuwa jeshi halitowaondoa waandamanaji kwa lazima, lakini alitoa wito kwa waandamanaji hao kuruhusu maisha yaendelee kama kawaida na waache kuweka vizuizi kinyume cha sheria. **BBC**



Aliyekuwa Rais wa Sudan, Omar Al Bashir ambaye aliondolewa madarakani na jeshi la nchi hiyo, kwa sasa amefungwa gerezani. **PICHA: REUTERS**

# Watu 150 wahofiwa kufariki dunia

**KINSHASA,** Congo

TAKRIBANI watu 150 hawajulikani walipo baada ya boti waliokuwa wakisafiria kuzama katika ziwa Kivu lililopo mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Rais wa Congo, Felix Tshisekedi, kupitia akaunti yake ya kijamii ya Twitter alisema kuwa amehuzunishwa kutokea kwa ajali hiyo.

"Nimehuzunishwa kuzama kwa boti hiyo katika ziwa Kivu. Hadi kufikia sasa idadi ya watu ambao hawajulikani waliko ni 150," alisema Rais Tshisekedi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa boti hiyo ilikuwa inatoka katika mkoa jirani wa Kivu Kaskazini mwa Congo na ilizama karibu na eneo la Kalehe.

Kadhalika, maiti tatu ziliopolewa, watu 33 wameokolewa huku abiria wengine 150 wakiwa hawajulikani waliko.

Rais Tshisekedi amesema kuwa anaifuatilia kwa karibu ajali hiyo ili kuwachukulia hatua watu wote waliohusika.

Matukio ya kuzama kwa boti nchini Congo yamekuwa yakitokea mara kwa mara. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Reuters mwaka uliopita, boti moja ilipinduka katika mto kaskazini mwa DR Congo na kusababisha watu 49 kufa maji.

Naibu Gavana wa Mkoa wa Mashambani wa Tshupa, Kaskazini mwa Congo, Richard Mboyo Liuka, alieleza kuwa boti hiyo ilizama na abiria wote jioni siku ya Jumatano.

Mwaka wa 2015, zaidi ya watu 100 walipotea baada ya boti mbili kugongana katika Mto Congo, kulingana na taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO).

Msemaji wa WHO katika mji mkuu wa Kinshasa, Eugene Kabambi, alisema kuwa boti hiyo ilipinduka karibu na mji wa Kwamouth wakati boti iliyokuwa imejaa kupita kiasi iliyokuwa ikielekea eneo la Inongo ilipogongana na boti moja iliyokuwa imebeba watu 150.

Julai 2011, zaidi ya watu 100 walifariki dunia baada ya boti mbili kugongana katika mto eneo la mkoa wa Equateur.

Miezi miwili awali, aliyekuwa Rais wa taifa hilo, Joseph Kabila, alimfukuza kazi waziri wake wa uchukuzi kufuatia visa vya mfululizo wa ajali za maboti viliyokuwa vikitokea nchini humo. **BBC**

# Bunge lataka wazee wa mahakama waondolewe

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kufanya maboresho katika Sheria ya Mahakama za Mahakimu ili kuondoa ulazima wa uamuzi wa mahakama za mwanzo kufanyika kwa kura za wazee wa mahakama au kuwaondoa wazee hao mahakamani.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka ujao wa fedha, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mohamed Mchengerwa, alisema kuna haja wazee wa mahakama wawapo kushauri tu.

Alisema ushauri wao usiwe wa lazima kiasi cha kuingilia uamuzi wa hakimu wenye kuzingatia sheria za nchi au serikali ione umuhimu wa kuwaondoa wazee hao au kwa namna itakavyoona inafaa bila kuathiri uamuzi wa hakimu.

"Msingi na ushauri wa kamati ni kwamba, pamoja na uwapo wa mila na desturi katika jamii zetu zenye kuhitaji wazee washauri katika baadhi ya mashauri ngazi ya mahakama za mwanzo, siyo mara zote ushauri wa walio wengi katika ngazi za mahakama za mwanzo unaendana na matakwa ya sheria.

Lakini pia, hatua hiyo itarahisisha utoaji haki kwa wakati katika mahakama za mwanzo ikiwamo kupunguza gharama za uendeshaji wa mahakama hizo," alisema.

Mchengerwa pia alisema kamati yake inaishauri Tume ya Utumishi wa Mahakama kuhakikisha inatatua changamoto ya watumishi kukaa kwenye kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu na stahiki zisizokidhi hali halisi ya maisha.

"Kamati inashauri majaji kwa kushirikiana na vyombo husika, waendelee kutekeleza utaratibu wao waliojiwekea wa kutembelea magereza pamoja na mahabusu nchini ili kujionea hali halisi ya mlundikano wa watuhumiwa na wafungwa kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa miongozo ya mahakama kuhusu kusikiliza na kumaliza mashauri mbalimbali kwa wakati," alisema.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mashimba Ndaki, alisema wilaya 27 kati ya 139 ndizo zenye majengo yanayomilikiwa na mahakama huku wilaya nyingine zikitumia majengo ya taasisi zingine.

Alisema mahakama inatakiwa kuendesha na kutekeleza shughuli zake kwa uhuru na bila vikwazo kwa kuwa ndiyo taswira inayochochea upatikanaji wa haki kwa wananchi.




Baadhi ya wafanyabiashara wakiingia kwenye kituo kipya kilichozinduliwa jana, kinachohamishika cha huduma za kubadilisha fedha za kigeni cha Benki ya Exim, nje ya Soko la Kariakoo, jijini Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Huduma ya fedha kigeni sasa kwa w'biashara

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wa Kariakoo, jijini Dar es Salaam wamesogezewa huduma ya fedha za kigeni, baada ya Benki ya Exim kuzindua kituo maalum kwa ajili ya kutoa huduma za kubadilisha fedha za kigeni (Bureau de Change) katika soko la hilo kuu.

Imeelezwa hatua hiyo ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo wa kusogeza huduma zake zaidi kwa wateja.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, mkuu wa huduma ya rejareja wa benki hiyo, Andrew Lyimo, alisema uamuzi wa kufungua kituo hicho kinachohamishika unafuatia ongezeko la mahitaji ya sasa ya wateja wanaotafuta huduma za uhakika za fedha za kigeni hususan katika eneo hilo ambalo ni kitovu cha biashara kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

"Benki ya Exim imekuwa ikihudumia wateja wengi kupitia tawi letu lililopo hapa Kariakoo na uamuzi wa kufungua huduma hii umekuja baada ya kugundua kuwa kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya huduma hii, hivyo tumeamua kuchukua hatua mapema ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo muhimu," alisema.

Aliongeza kuwa jukumu la benki hiyo litabaki katika kuwezesha jumuiya ya wafanyabiashara kukuza biashara zao, huku benki hiyo ikiwasogezea huduma kwa ukaribu zaidi.

"Tunaamini kupitia kituo chetu hiki kinachohamishika, jumuiya ya wafanyabiashara Kariakoo, itafurahia huduma zetu kwa kuwa wataweza kuuza na kununua fedha za kigeni papo hapo bila gharama yoyote," alibainisha.

Lyimo alisema huduma hiyo inaifanya benki hiyo izidi kuimarisha uwezo wake wa kutoa huduma na inadhihirisha kujitoa kwake kwa wafanyabiashara hasa wa kati na wadogo katika Jiji la Dar es Salaam na kitaifa kwa ujumla.

"Inafahamika kuwa Kariakoo ni eneo la biashara na ni kitovu cha waagizaji, wafanyabiashara na wasambazaji ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji huu wa uchumi," aliongeza.

# Wafanyakazi 59 kujitolea kutoka Marekani waapishwa

**Na Salome Kitomari**

KAIMU Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, amewaapisha wafanyakazi 59 wa kujitolea kutoka nchini mwake, ambao watafanyakazi katika sekta ya afya na kilimo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Ubalozi wa Marekani nchini, wafanyakazi hao watafanya kazi kwa miaka miwili na watapangiwa katika wilaya 35 nchini.

Patterson aliwaeleza wafanyakazi wapya wa kujitolea kuwa: "Kupitia programu hii mtaweza kuleta mabadiliko kwa Watanzania mtakaofanya nao kazi na hata kwenu ninyi wenyewe."

Alisema wataweza kuwa Wamarekani wa kwanza kukutana na kufanya kazi na wafanyakazi wenzao na majirani zao wa Kitanzania, na kwamba wataendelea kuwa wawakilishi wa watu wa Marekani na ubia wa muda mrefu kati ya Wamarekani na Watanzania.

Katika hafla hiyo mgeni rasmi alikuwa ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwita Waitara, na ilihudhuriwa na viongozi wa serikali, wafanyakazi wa kujitolea wa zamani, wawakilishi wa taasisi wabia na wanafamilia wa familia za Kitanzania ambazo wafanyakazi hao wa kujitolewa waliishi nazo.

Peace Corps ni taasisi ya Serikali ya Marekani iliyoanzishwa na Rais John F. Kennedy mwaka 1961 ambayo hivi sasa inahudumia zaidi ya wafanyakazi wa kujitolea 7,000 katika zaidi ya nchi 70 duniani.

Kwa zaidi ya miaka 50, Peace Corps imekuwa taasisi inayoendesha shughuli za mabadilishano ya kiufundi na kitamaduni zisizoegemea mrengo wowote wa kisiasa na kidini. Aidha, ina dhamira ya kukuza amani na urafiki duniani kwa kutekeleza malengo matatu ya kutoa wafanyakazi wa kujitolea wa Kimarekani watakaochangia kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi itakayohitaji wafanyakazi hao.

Pia, kukuza uelewa kuhusu Wamarekani miongoni mwa watu katika jamii zinazohudumiwa na wafanyakazi wa kujitolea na kuimarisha uelewa wa Wamarekani kuhusu dunia na watu wake.

Zaidi ya wafanyakazi wa kujitolea wa Peace Corps 3000 wamehudumu nchini toka mwaka 1961, wenye utaalamu katika nyanja mbalimbali ambao hupangiwa kufanyakazi katika jamii wakifundisha katika shule za sekondari (Hisabati, Sayansi na Kiingereza), wakitoa elimu ya afya na utunzaji wa mazingira.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: **MJINI MOROGORO**
Usimamizi wa Mirathi No. 96/2019

Ombi la **ISMAIL ABDUL** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu ABDUL ISMAIL

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 06/05/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 17/04/2019

115185002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ANN G. MAWALLA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.785 AMV** AINA YA TOYOTA HARRIER RANGI YA SILVER, CHASSIS NAMBA **SXU150006240,** ENGINE NAMBA **5SO78806056**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
**TAARIFA YA POLISI MB/RB/232/2019.**

215185602

**IN THE DELEGATE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE ADMINISTRATION CAUSE NO.33 OF 2019**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ERASTO ALBETUS ERASTO - DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MAX GALLUS LIKAPAKAPA**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby invited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of probate for letters of administrationis made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 15 day of May, 2019.
The will if any ofthe said deceased to be deposited and open for inspection of the court.
Dated 15thThis day of April,2019

Resident Magistrate
DODOMA

215184602

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

**NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SCHOLES MATATANI KWA KUBETI

**LONDON,** England

NYOTA wa zamani Klabu ya Manchester United, Paul Scholes, anatuhumiwa kukiuka sheria na kubashiri (kubeti) kwenye timu anayoimiliki.

Mchezaji huyo mstaafu wa timu ya Taifa ya England ametuhumiwa kwa kushiriki kubashiri matokeo ya michezo ya mpira wa miguu.

Kwa mujibu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha England, FA, Paul Scholes, amejihusisha na kubeti kwa kwa kipindi cha miaka minne hadi Januari mwaka huu.

FA imesema Scholes amekiuka kanuni za soka kwani alikuwa akifanya ubashiri huo hata wakati alipokuwa mmiliki mwenza wa timu ya Salford City.

Kwa muda wote huo Scholes alishiriki 'betting' mara 140 na endapo atakutwa na hatia atatozwa faini ya zaidi ya Sh. milioni 90.

Kwa mujibu wa Gazeti la Gurdian, msemaji wa FA alielezea tofauti iliyotumiwa sasa, ni kama mtu ni kocha kama mshiriki katika soka, maelezo yote yanayopangwa kuwa na wachezaji, mameneja, wamiliki, mawakala na yeyote anayefanya kazi ndani ya mchezo.

# Fernandes akomalia kujiunga Man United

**LISBON,** Ureno

KIUNGO wa Sporting CP, Bruno Fernandes, amedai kwamba yupo tayari kuchukua hatua inayofuata kwenye maisha yake ya soka na anatazamia kuhamia kwenye Ligi Kuu ya England au Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa kwenye kiwango cha juu katika Ligi Kuu ya Ureno, Primeira Liga, ambako amehusika kwenye mabao 27.

Mchezaji huyo wa Ureno alikaribia kuondoka msimu uliopita, lakini akaamua kubakia kwenye ligi hiyo.

"Mwaka jana, nilipokea ofa nyingi, zaidi ni kutoka England na kutoka Hispania, lakini nilihisi sikujiandaa kuondoka," alisema Fernandes akiiambia Sport TV.

"Sio kwa sababu ya magumu, lakini kwa idadi ya mechi nyingi England.

"Mwanzo wangu pale Sporting ilikuwa ni mara ya kwanza nilicheza mechi nyingi, nilifikiri nilihitaji mechi nyingi zaidi za kucheza.

"Na sasa najihisi kwamba nahitaji kupata changamoto mpya, kamwe zijawahi kuichezea timu yoyote England au Hispania."




# Allegri asisitiza haondoki Juventus

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri amesisitiza kwamba ataendelea kuwa katika nafasi yake ya ukocha wa klabu hiyo msimu ujao, licha ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya robo fainali.

Baada ya mchezo wa kwanza kumalizika kwa sare ya 1-1, Cristiano Ronaldo alifikisha bao la 126 kwenye michuano hiyo, lakini halikutosha kuwafanya Bianconeri hao kupata ushindi.

Baada ya Donny van de Beek kusawazisha, nahodha mwenye umri wa miaka 19, Matthijs de Ligt alifunga bao la ushindi katika dakika ya 67.

Na baada ya mchezo huo, Allegri aliseema: "Ajax kwa uhakika kabisa walistahili ushindi na walicheza vizuri na zaidi kipindi cha pili. Walikuwa na bahati kwani walisawazisha na walitubana vizuri.

"Nafikiri kipindi cha kwanza tulicheza vizuri, lakini kipindi cha pili hakikuwa upande wetu, tuliwaacha Ajax wakatawala kiungo."

Ajax imetinga nusu fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza katika miaka 22, baada ya kutoka nyuma kwa bao moja, na kushinda 2-1 dhidi ya Juventus ugenini katika Uwanja wa Allianz. Mchezo wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya 1-1, hivyo Ajax wanafuzu kwa jumla ya mabao 3-2.

Juventus hawatamsahau Matthijs de Ligt, aliyezamisha jahazi la vigogo hao wa Turin, katika dakika ya 67.

Ajax inasubiri mshindi wa mechi ya Manchester City dhidi ya Tottenham, wanaokipiga Jumatano hii, City ikiingia katika mchezo huo ikiwa nyuma kwa bao 1-0.

Kocha wa Juventus Massimiliano Allegri alisema: "Wametupa shida sana kipindi cha pili, na kuruhusu bao, Ajax wanastahili matokeo haya na kufuzu nusu fainali.

"Nimemueleza rais kwamba nabaki, sitajiuzulu na rais pia anataka nibaki. Tutakaa chini na kuzungumza kuhusu mustakabali wa timu hii."



## HABARI MICHEZO

# VALVERDE APOTEZEA USHANGILIAJI WA COUTINHO




**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde amekataa kuzungumzia staili ya ushangiliaji wa Philippe Coutinho wakati alipofunga bao la tatu kwenye ushindi wa 3-0 dhidi ya Manchester United juzi Jumanne.

Mabao mawili kutoka kwa Lionel Messi yaliipa Barcelona nafasi nzuri na Coutinho akaongeza la tatu kabla ya kushangilia kwa kufumba macho na kuziba masikio yake kwa vidole, ikiwa ni jibu la mashabiki ambao wanadai kiwango chake kimeporomoka.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Valverde alisisitiza kwamba yeye hakujikita kwenye ushangiliaji wa Coutinho kwani akili yake ilikuwa kwenye goli tu.

Aliongeza: "Sijui alikuwa anamaanisha nini. Jibu analijua yeye mwenyewe na si mwingine. Niliona akifunga bao zuri, lakini mengine yaliyojiri sijui. Kitu cha muhimu ni kwamba tulipata ushindi.

"Sisi tupo kwenye matarajio makubwa. Tunatakiwa kushinda kila kitu na tunajua nini ambacho kinachotakiwa, na haikuwa rahisi.

"Pia kuna asilimia ya uchezaji na mara zote tunacheza vizuri, kwamba jambo la msingi ni kubwa Coutinho mara zote anafunga. Sisi wote ni binadamu na wote tunataka ushindi."

Pia akamzungumzia Lionel Messi, ambaye alionyesha kiwango cha juu kwa kuiwezesha kupata ushindi huo.

Hata hivyo, Valverde alisisitiza kwamba kiwango hicho hakikumshangaza yeyote kwani ilitarajiwa hivyo.

## *Solskjaer: Barcelona itabeba ubingwa Uefa*

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anaamini kwamba Barcelona itatwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Kikosi cha Solskjaer, United kilitolewa na Barca kwenye mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa baada ya Lionel Messi kufunga mabao mawili kwenye ushindi wa 3-0 juzi, Jumanne.

Bao la shuti la Philippe Coutinho lilitosha kuizamisha Man United na hivyo kuwapa ushindi wa jumla wa mabao 4-0 na kuipeleka nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa.

Alipoulizwa kuhusu nafasi ya Barca kwenye ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku ikitarajiwa kucheza dhidi ya Liverpool au Porto, Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari: "Nafikiri Barcelona itashinda.

"Kwa ubora walionao pale mbele, hasa wachezaji wake watatu, wana nafasi kubwa ya kushinda. Wana (Ousmane) Dembele na Malcom, wachezaji ambao wanaingizwa kusaidia.

"Nitakuwa na wao, ingawa sijabeti. Lakini kwa upande wangu wao wana nafasi kubwa kwenye mashindano yote."

United sasa akili yake ni kupigania kupata nafasi ya kufuzu hatua ya nne bora kwenye Ligi Kuu ya England.



# Ajax yaweka historia Uefa ikitinga nusu fainali

**TURIN,** Italia

AJAX imekuwa timu ya kwanza kutoka kwenye raundi tatu na kufuzu kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwatupa nje Cristiano Ronaldo na Juventus.

Miamba hao wa Uholanzi wameng'ara Ulaya msimu huu, wakiwatoa mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Real Madrid na sasa Bianconeri kwa ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kampeni ya Ajax ilianzia mwishoni mwa Julai, baada ya kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, msimu uliopita, na hakuna timu inayofanana nayo kwenye historia ya kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ajax ilicheza na Sturm Graz, Standard Liege, Dynamo Kiev, AEK Athens, Bayern Munich, Benfica, Madrid na kuiondoa Juve na sasa imetinga nusu fainali ikisubiri bingwa kati ya Manchester City na Tottenham ambazo zilicheza jana.

Bao la kichwa la nahodha Matthijs de Ligt (pichani), liliipa ushindi wa 2-1 kwenye Uwanja wa Turin dhidi ya mabingwa hao mara nne wa Ulaya na kusonga mbele kwa uwiano wa mabao 3-2.

Beki huyo wa kati wa Uholanzi kwa sasa ana umri wa miaka 19 na siku 246, na kuwa mchezaji wa kwanza kijana kufunga kwenye hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 1996.



# DONDOO Z KA
# MAGAZETI Y YA




# MESSI ATANGAZA NDOO TATU BARCA

●●● Ahofu mbeleni kukutana na Ajax akikumbuka walichotendwa na Roma msimu uliopita na...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anaamini kuwa Barcelona imepiga "hatua kidogo" kuelekea kutwaa makombe matatu baada ya kuitupa nje Manchester United kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kutinga nusu fainali.

**Messi alicheka na nyavu mara mbili wakati wakishinda 3-0 katika Uwanja wa Camp Nou juzi na hivyo Barca kusonga mbele kwa tofauti ya mabao 4-0 dhidi ya kikosi hicho cha kocha Ole Gunnar Solskjaer, United.**

Na wakati wakiongoza kwa pointi tisa zaidi kwenye mbio za ubingwa wa La Liga huku wakisubiri kucheza mechi ya fainali ya Kombe la Mfalme [Copa del Rey] dhidi ya Valencia, Barca ipo katika njia sahihi ya kurudia mafanikio yao ya kushangaza ya kutwaa makombe matatu kipindi wakiwa chini ya kocha Luis Enrique msimu wa 2014-15.

Lakini Messi anataka mbio za ubingwa wa ndani wazimalize mapema zaidi kuliko kusubiri baadaye ili kuongeza nafasi ya kupigania kila kilicho mbele yao.

"Kama nilivyosema, ni mwenye furaha kwa ushindi," aliiambia Movistar. "Tumepiga hatua kidogo [kuelekea kutwaa makombe matatu]. Tunapaswa kufikiri kuhusu La Liga na kujaribu kuwa mabingwa haraka iwezekanavyo.

"Tutajiandaa kwa nusu fainali kwa namna mechi inavyostahili."

Ushindi wa Barca umekuja wakati Juventus ikitolewa na Ajax huko Turin, wakali hao wa Ligi Kuu Uholanzi ['Eredivisie'] walipata ushindi wa 2-1 juzi na hivyo kusonga mbele kwa tofauti ya jumla ya mabao 3-2.

Matokeo hayo yalishangiliwa na mashabiki wao katika dimba la Camp Nou, kufuatia Ajax kuwatoa mabingwa watetezi, Real Madrid katika hatua ya 16-bora kabla ya juzi kutupa nje Juve na Cristiano Ronaldo wao.

Messi anaamini matokeo hayo yanaonyesha ni kwa namna gani itakavyokuwa vigumu kuibuka bingwa wa michuano hiyo.

"Ninakwambia kila kitu," alisema kufuatia kipigo cha Juve. "Wao ni bora. Itakuwa ngumu.

"Tunao uzoefu wa Roma [kipigo cha mabao 3-0 msimu uliopita] - mechi yoyote itafanya kusonga mbele kuwa vigumu, mpinzani yeyote atakuwa mgumu."

## ZISIKUPITE

### SARRI, CONTE WATAJWA ROMA

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri na mtangulizi wake katika kikosi hicho, Antonio Conte, wanapewa nafasi ya kuinoa Roma. ***(Corriere Dello Sport - in Italian)***

### KUVAA VIATU VYA HAZARD

CHELSEA imekubali itampoteza mshambuliaji Mbelgiji Eden Hazard, 28, na sasa inataka kuziba nafasi yake kwa kumsajili winga wa Lille na Ivory Coast, Nicolas Pepe, 23. ***(Mirror)***

### ZIDANE SASA AMKATAA BALE

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ameiambia klabu hiyo imuuze winga wa kimataifa wa Wales, Gareth Bale, 29, hata kama inapoteza pesa. ***(Independent)***

### KUJITOSA KWA UMTITI

ARSENAL inapewa nafasi ya kumsajili beki wa kati wa Barca, Samuel Umtiti, 25, lakini Manchester United pia ipo tayari kuipata huduma ya beki huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(TuttoMercato, via Star)***

### KLOPP AMTEGA VINICIUS REAL

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, aliulizia kuhusu mshambuliaji kinda Mbrazil Vinicius Junior, 18, wakati iliihitaji huduma ya Msenegal Sadio Mane msimu uliopita. ***(El Chiringuito, via Metro)***

### BRANDT AWINDWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo tayari kumsajili winga wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Julian Brandt. ***(Bild, via Calciomercato)***

### RONALDO JR ATUPIA SABA

MTOTO wa mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, Ronaldo Jr. amefunga mabao saba katika kipindi kimoja [dakika 45] wakati kikosi cha Juve U-10, kikiichapa Maritimo. ***(AS)***

### MANE AFURAHIA MAISHA LIVER

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane, 27, amekuwa akihusishwa na Real Madrid, lakini amesema ni mwenye "furaha sana" hapo Anfield. ***(LFC magazine, via Mail)***

### SESSEGNON BADO ATEGWA

TOTTENHAM inaongoza mbio za kumsajili winga wa Fulham, Ryan Sessegnon, 18, shukrani kwa kocha Mauricio Pochettino kwa kufanya kazi na kipaji kingine cha England. ***(Sun)***

### COUTINHO NGUMU KUNG'OKA

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesema kiungo Mbrazil Philippe Coutinho, 26, ataruhusiwa kuondoka endapo tu dau la kuvunja mkataba wake, linalodhaniwa kuwa pauni milioni 355, litafikiwa. Manchester United na Chelsea zinaelezwa kuvutiwa na mchezaji huyo. ***(TVE, via Football 365)***

### WEIGL AGOMBEWA CITY, PSG

MANCHESTER City inakabiliwa na upinzani kutoka kwa Paris St-Germain wakati huu ikijaribu kumsajili kiungo Mjerumani Julian Weigl, 23, kutoka Borussia Dortmund. ***(France Football, via Sun)***

## HABARI MICHEZO

# Serengeti Boys yapoteza tena

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya Vijana chini ya Miaka 17, Serengeti Boys jana ilishindwa kupeperusha matumaini yao ya kukata tiketi ya kwenda kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Brazil, baada ya kufungwa mabao 3-0 na yosso wenzao wa timu ya Taifa ya Uganda.

Kwa matokeo hayo, sasa Serengeti Boys ni kama imepoteza matumaini ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia nchini Brazil kufuatia kupoteza mechi ya awali dhidi ya Nigeria kwa mabao 5-4.

Katika Kundi lao la A, Serengeti sasa inaburuza mkia ikiwa bila pointi huku Nigeria ikiwa tayari imefuzu kufuatia jana kuichapa Angola bao 1-0 na kufikisha alama sita.

Uganda ambayo mechi ya mwisho itamaliza dhidi ya Nigeria ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu sawa na Angola, lakini ikiizidi kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Alikuwa ni Kawoya Andrew aliyeanza kupeleka majonzi kwa Watanzania alipofunga bao la kwanza, baada ya krosi safi kutoka upande wa kulia mwa uwanja. Uzembe wa mabeki wa kati wa Serengeti Boys ikiongozwa na Alfonce Mabula, uliipatia Uganda bao la pili dakika ya 27 kwa shuti kali lililopigwa na Asaba Ivan.

Bao lililowanyong'onyesha kabisa Serengeti Boys pamoja na Watanzania waliojazana kwenye Uwanja wa Taifa lilifungwa na David Yiga kwa kichwa, baada ya kuunganisha kona kutoka Mashariki ya uwanja.

Katika mechi hiyo, Serengeti walipambana kufa na kupona kuhakikisha wanapata hata bao la kufutia machozi, lakini mabeki wa Uganda na kipa wao walikuwa makini na kuhakikisha mastraika wa Serengeti Boys walioongozwa na Kelvin John hawaleti madhara.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**




| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 31 | 23 | 4 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2. Azam | 31 | 19 | 9 | 3 | 49 | 18 | 66 |
| 3. Simba | 23 | 19 | 3 | 1 | 50 | 8 | 60 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Kinondoni MC | 31 | 9 | 15 | 7 | 32 | 22 | 42 |
| 7. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 8. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 9. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 10. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 19 | 26 | 39 |
| 11. Ndanda | 30 | 10 | 9 | 11 | 20 | 29 | 39 |
| 12. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 13. Mbeya City | 31 | 10 | 7 | 14 | 30 | 34 | 37 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 31 | 8 | 12 | 11 | 26 | 32 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# WAWA KUANZA KUJIFUA JUMATATU

**Na Somoe Ng'itu,** TANGA

BEKI wa kati wa kimataifa wa Simba, Paschal Wawa, anatarajia kuanza mazoezi mepesi Jumatatu baada ya maumivu ya misuli aliyokuwa nayo kupona, imeelezwa.

Wawa, beki huyo raia wa Ivory Coast aliumia katika dakika ya sita ya mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya wenyeji Simba dhidi ya TP Mazembe iliyochezwa Aprili 6, mwaka huu na kumalizika kwa suluhu.

Kutokana na maumivu hayo, Wawa ambaye amekuwa katika kikosi cha kwanza cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba aliukosa mchezo wa marudiano uliochezwa mjini Lubumbashi na pia jana dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini hapa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa hali ya beki huyo imeimarika baada ya kupumzika katika muda aliopewa na daktari wao.**

Rweyemamu alisema pia beki wao mwingine, Juurko Murshid na kiungo James Kotei wanaendelea vema, lakini hana uhakika kama watajumuishwa katika safari ya kuelekea mikoa ya Kanda ya Ziwa.

"Kocha Mkuu (Patrick Aussems) ndiye ataamua kama wote tutakwenda Kanda ya Ziwa, lakini ni baada ya kupata majibu kutoka kwa daktari wa timu kuhusu maendeleo yao," alisema meneja huyo.

Baada ya mechi ya jana, Simba inarejea jijini Dar es Salaam kuanza kujiandaa na safari ya kuifuata Kagera Sugar ambao watakutana Jumamosi kwenye Uwanja wa Kaitaba mkoani Kagera.




Mkurugenzi wa Utawala na Utekelezaji wa Kampuni ya SportPesa, Abbas Tarimba (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu ujio wa Klabu ya Sevilla ya Hispania nchini. Katikati ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla. Habari UK. 32. **PICHA: SPORTPESA**



# *Majibu waliosailiwa Yanga hadharani*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inatarajia kutoa majibu ya mchakato wa usaili wa wanaowania nafasi za uongozi katika Klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam leo, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Ally Mchungahela (pichani), alisema kamati yake ilitarajia kumaliza mchakato wa usaili pamoja na kusikiliza pingamizi zilizowekwa jana na leo itaweka wazi hatua nyingine inayofuata ya uchaguzi huo.

Mchungahela alisema anaamini mchakato wa uchaguzi huo utakamilika na hatimaye Yanga itapata viongozi wapya watakaoingia madarakani kwa mujibu wa katiba.

"Kila kitu kinakwenda vizuri, kamati yangu inafuata mwongozo wa kalenda yake na inawataka wanachama wa Yanga kuendelea kutoa ushirikiano ili kufanikisha uchaguzi wa klabu yao," Mchungahela alisema.

Yanga inafanya uchaguzi mkuu mapema mwezi ujao baada ya viongozi wake wote wa kuchaguliwa kutangaza kujiuzulu nafasi zao kutokana na sababu tofauti.

Hata hivyo, pamoja na changamoto ya safu ya uongozi wa Yanga kuwa pungufu, timu yao imekuwa ikifanya vema katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya Kombe la FA ambayo wameingia hatua ya nusu fainali.

# Michezo

Alhamisi Aprili 18, 2019

Nipashe




Serengeti Boys yapoteza tena

UKURASA 31



Lionel Messi akiachia shuti langoni mwa Manchester United, wakati wa mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou juzi na Barcelona kushinda 3-0 hivyo kusonga mbele kwa tofauti ya mabao 4-0. **HABARI UK. 29**

# Simba, Yanga kuivaa Sevilla ya La Liga Dar

## SportPesa yakamilisha mpango kuwaleta mabingwa hao mara tano wa Europa League...

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIKA kuhakikisha inazidi kutoa mchango mkubwa kwa soka la Tanzania kukua, Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa kwa kushirikiana na La Liga imetangaza kuileta nchini Klabu ya Sevilla ya Hispania kwa ajili ya ziara ya kimichezo inayokwenda kwa jina la "SportPesa Laliga Challenge" ambapo klabu kongwe, Simba ama Yanga moja itapata fursa ya kucheza mechi ya kirafiki na mabingwa hao mara tano wa Uefa Europa League.

**Sevilla, iliyotwaa mara moja ubingwa wa Hispania, kwa sasa inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa La Liga ikiwa na pointi 52 baada ya mechi 32.**

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma jana, Mkurugenzi wa Utawala na Utekelezaji wa Kampuni ya SportPesa, Abbas Tarimba, alisema kampuni yao kwa kushirikiana na uongozi wa La Liga, wamekubaliana kuileta timu hiyo nchini.

"SportPesa tunaendesha biashara yetu kwa kujihusisha na maendeleo ya soka kwenye nchi tunazoendesha shughuli zetu kwa kushirikiana na wadau husika huku tukitumia washirika wetu wa kimataifa kuleta maendeleo hayo.

"Mara ya mwisho dunia ilishuhudia Klabu ya Everton ikitembelea Tanzania kwa mara ya kwanza na muitikio ulikuwa ni wa kipekee. "Kutokana na SportPesa kuwa na ushirika na taasisi kubwa za soka duniani kama La Liga, tukaona basi ni vyema kuendeleza msisimko wa kimataifa kwa kuleta Klabu ya Sevilla nchini Tanzania ambayo inacheza kwenye ligi hiyo bora duniani."

Aidha, Tarimba alibainisha kuwa awali walipanga kuwa na mechi kati ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga ili mshindi wa mechi hiyo ndiye acheze dhidi ya Sevilla, lakini imeshindikana kutokana na kile alichoelezwa kuwa ugumu wa ratiba unaozikabili timu hizo kwa sasa.

Alisema mechi kati ya Sevilla na timu ya Tanzania watakayoichagua, itachezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Mei 23 ikiwa ni baada ya miamba hiyo kuwasili nchini Mei 21, mwaka huu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wilfred Kidao, alisema ujio huo wa Sevilla ni fursa pekee kwa wachezaji wetu na wadau wa sekta ya mpira nchini kujifunza.

"Unapopata nafasi ya timu yako ya nchi kucheza na timu kubwa kama hiyo ni jambo la heshima na lina faida nyingi kwa maana ya kujitangaza kwa sababu dunia nzima itajua kwamba Sevilla ipo Dar es Salaam, lakini pia wachezaji wetu watapata nafasi ya kujifunza kutoka kwa wenzao sambamba na kuonekana na kumulikwa na wataam wa kusaka vipaji duniani," alisema Kidao.

Katika mkutano huo uliohudhuriwa na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, alipongeza Kampuni ya SportPesa kwa kufanikisha ujio wa timu hiyo na kueleza kuwa kampuni hiyo ni mdau mkubwa wa michezo nchini.

Alisema ujio wa Sevilla nchini utaitangaza Tanzania duniani na hivyo kusaidia kuwatangaza hata wachezaji wa Tanzania watakaocheza dhidi ya timu hiyo Mei 23.

Naye Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla alisema wizara yake itautumia ujio wa timu hiyo kama fursa ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

# Kagere atabaki kileleni, Yanga yagongwa moja

**Na Somoe Ng'itu,** TANGA

MABAO mawili yaliyofungwa na Meddie Kagere yamemfanya kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora wakati Simba ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Coastal Union kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa jana na wakati huo huo Yanga ikigongwa 1-0 na Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

Ushindi huo umewafanya mabingwa hao watetezi wa ligi kufikisha pointi 60 baada ya kucheza mechi 23 huku vinara Yanga licha ya kipigo hicho cha jana wakiendelea kubaki kileleni na pointi zao 74.

Kagere sasa amefikisha mabao 16 sawa na Salim Aiyee wa Mwadui FC huku Heritier Makambo wa Yanga akifuata kwa mabao 15 katika orodha hiyo ya wanaowania Kiatu cha Dhahabu. Na Simba imekuwa timu ya kwanza kuifunga Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani msimu huu, huku klabu nyingine zikifungwa au zikiambulia sare ikiwamo Yanga.

Kagere alifunga bao la kwanza kwa njia ya penalti katika dakika ya 48 baada ya mwamuzi, Athumani Senkala kutoka jijini Arusha kutoa adhabu hiyo kutokana na kipa, Sudi Abdallah kumfanyia faulo, Emmanuel Okwi ndani ya eneo la 18.

Mnyarwanda huyo alizitingisha tena nyavu za Coastal Union katika mchezo huo ulioanza saa nane mchana kwa kupiga shuti kali baada ya kumalizia pasi safi kutoka kwa kiungo Mzambia, Clatous Chama dakika ya 68.

Hata hivyo, wenyeji Coastal Union wanaofundishwa na Juma Mgunda ndio walikuwa wa kwanza kupata bao katika sekunde ya arobaini ya mchezo huo kupitia kwa Raizini Hafidh ambaye aliwahi kupiga shuti la kushtukiza langoni wakati mabeki wa Simba, Erasto Nyoni na Yusuph Mlipili wakiwa bado hawajajipanga vema kulinda lango lao.

Simba iliamka zaidi katika kipindi cha pili na mabadiliko ya kwanza kabisa ya kuingizwa kwa Chama na kumtoa, Mzamiru Yassin kulifufua upya uhai wa Wekundu hao wa Msimbazi ambao Jumamosi iliyopita walitolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na TP Mazembe.

Kikosi cha Simba kiliondoka jijini hapa jana jioni kurejea Dar es Salaam na leo kitaanza safari ya kuelekea Bukoba kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Kwingineko katika Uwanja wa Jamhuri, bao la dakika ya 52 lililowekwa nyavuni na Rifati Hamisi lilidumu hadi mwisho wa mchezo wakati Yanga ikikubali kipigo cha 1-0 kutoka kwa wenyeji Mtibwa Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002